Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Tatu – Tarehe 23 Aprili, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha ya majina 11 hapa na swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali langu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wafugaji waliokuwa wamehamia katika Bonde la Ihefu walikaa muda mrefu na hatimaye Serikali ikachukua hatua ya kuwahamisha kiasi ya kwamba mali zao na familia zao zikaathirika sana.

Hivyo hivyo Serikali ilichukua hatua kwa wachimbaji wadogo wadogo waliokuwepo Kunduchi ambao nao walichukua mikopo na hatimaye Serikali ikawatimua na wakaathirika sana.

Leo Serikali baada ya *DECI* kuwa *registered* mwaka 2007, wakati Sheria ya Benki Kuu ya kusimamia vyombo vyote vinavyohusika na mambo ya fedha ilipitishwa mwaka 2006. Ni kwa nini Serikali ina Sera ya kuacha maovu yatokee na hatimaye ichukue hatua jambo ambalo linasababisha wananchi kupoteza rasilimali zao, utu wao na vilevile kunyanyasika kwa kiasi kikubwa? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme Serikali haina sera ya namna hiyo. Mimi nadhani kubwa katika suala hili la *DECI* kwa Bunge lakini na kwa Watanzania wote ni kujua tu kwamba mfumo wowote wa upatu ni kinyume cha sheria. Ni kosa la jinai. Kwa hiyo, kama ilivyo kwa sheria nyingine zozote zenye masuala kama haya ambayo ni ya kijinaijinai taratibu zake ni zile za kawaida. Unakosea unakamatwa unapelekwa Mahakamani unafunguliwa mashtaka. Huo ndiyo mfumo tunaoujua upo na kwa mtu anayefanya kinyume na sheria hii wala si suala la Serikali kwamba tumeruhusu.

Ni wajibu wa kila Mtanzania kujua kwamba kukiuka sheria ni kosa la jinai. Mimi nadhani hilo ndilo jambo la kwanza ambalo tunatakiwa tulijue. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwamba, kwa hili la *DECI* ninachoweza kusema ni kwamba ni vizuri Waheshimiwa Wabunge kujua kwamba jambo hili limeingia kupitia mkondo wa dhehebu la dini. Dhehebu la Dini *Jesus Christ* ambayo ndiyo ilikuwa inatumia kama ndiyo mkondo wake. Kwa hiyo, ni kitu kilikwenda kwa namna fulani kiumini umini na halikujitokeza moja kwa moja dhahiri kwamba ni chombo ambacho kinatumika na umma moja kwa moja. Ndiyo maana walipokwenda kuomba kibali Benki Kuu, ikawaambia kwamba kama mnachofanya mnasema mna mtaji wenu wenyewe na mnataka mtaji huo mtumie kukopesha wafanyabiashara wadogo wadogo na akinamama hatuna tatizo na hilo, kikubwa tuleteeni sasa *financial memorandum* yenu na mambo mengine yanayohusiana na sera zenu na mjue kwamba tutahitaji kila mwisho wa mwaka mtuletee *an audited account* ili tujue mambo yanakwendaje. Wakaondoka wakaenda lakini wakaonywa kwa maandishi kwamba tunachowasisitizia mfumo huu hauwaruhusu ninyi kuchukua amana yoyote kutoka kwa Mtanzania. Mkiingia kwenye amana tu uko utaratibu ambao lazima mrudi Benki Kuu kuja kufanya haya.

Sasa wenzetu hawa hilo hawakufanya, wakaenda wakafanya upatu badala ya kufanya kile walichokuwa wamesema watafanya. Ndiyo maana unaona kimya kimya halikuweza kugundulika mpaka baadaye vyombo vilipoanza kupata taarifa kutoka kwa Watanzania mmoja mmoja na ndiyo maana Serikali ikaingilia kati na kujaribu kusimamia hilo jambo kwa lengo zuri tu kwamba tutizame uwezekano wa kuona kama kuna fedha yoyote ambayo bado iko nje fedha hiyo tuisimamie vizuri angalau wale waliopanda hata kama hawatavuna. kile walichopanda waweze kurejeshewa. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kama anavyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sahihi inakuwaje Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Fedha akaenda akafungua tawi la *DECI* Morogoro Kilosa wakati anajua jambo hilo ni kinyume cha Sheria?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi hilo kwanza silijui. Lakini hata kama alikwenda akafungua hilo Tawi, hiyo haina maana kwamba ni baraka kwamba kosa hilo lihalalishwe liwe ni halali. Hapana. Inawezekana nae ali-*operate under ignorance* kama wengi ambavyo wali-*operate* chini ya kutokujua mfumo ulivyo. *It is unfortunate* kama Waziri wa Fedha naye aliona ni jambo jema akaenda akalifanya, ilitakiwa awe mtu wa kwanza kujua. Lakini kama ilivyo kwa mtu mwingine yoyote inawezakana aliteleza vilevile.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana nafasi zake za kuteua viongozi wa kuweza kumsaidia nafasi zake mbalimbali wakiwemo Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya.

Katika Wakuu wa Wilaya hawa kuna baadhi yao wanapangiwa Wilaya na Mikoa na wakishapangiwa hizo sehemu hawafanyi kazi vilivyo. Wanakuwa wanavuruga

wananchi pamoja na viongozi wa sehemu hiyo. Mheshimiwa Waziri Mkuu unalitamkiaje hilo suala?

**SPIKA:** Halijakaa vizuri.

**WAZIRI MKUU:** Halijakaa vizuri, wewe sema una tatizo na Mkuu wa Mkoa gani au Mkuu wa Wilaya gani, ili tujue.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Kwa mfano Wakuu wa Wilaya wa Bukoba na Mkuu wa Mkoa wa Kagera kwa tatizo walilolifanya sehemu mbalimbali za Misenyi na Bukoba Mjini. Je, unalitamkaje kwa kisiasa.

**SPIKA:** Tatizo ni nini Mheshimiwa?

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, tatizo wanavuruga wananchi pamoja na viongozi tulioko katika Jimbo hilo na nimeshauliza kwamba analitamkaje hilo swali.

**SPIKA:** Nashauri kwenye hili tupate hoja mahsusi ili tuweze kulishughulikia Kibunge. Kwa sababu hii ni tuhuma ambayo itakuwa ni ya jumla na tutakuwa hatuwatendei haki kama haianishwi vizuri ikaweza kufanyiwa kazi vizuri. Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Kwa kuwa operesheni mifugo inayoendelea sasa hivi maeneo mbalimbali ya nchi hii imefanyika kibabe sana na kwa kutumia mabavu zaidi badala ya kutumia elimu na kuhamasisha wananchi. Suala ambalo limepelekea wafugaji wengi kupoteza ng'ombe wao wengine kufilisika, kunyanyasika na hata wengine wakapoteza maisha. Serikali inafanya nini kutafuta suluhisho la kudumu la suala hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Sakaya kwa sababu ameliweka vizuri sana. Kwamba Serikali inafikiria kufanya nini kupata ufumbuzi ambao ni wa kudumu pengine kuliko taratibu nyingine ambazo tunaenda nazo hivi sasa. Tatizo la wafugaji na wakulima ni kubwa sana wala si dogo na sasa lina muda kidogo na kwa kweli limejitokeza katika sura mbalimbali. Ninachoweza kusema hapa kwa kifupi ni kwamba kama Serikali nilichofanya mimi mwenyewe ni kuamua kwamba pengine tufanye kazi ambayo ni ya kisera. Kwa hiyo nimeunda timu ambayo imekwenda kuzungukia mikoa karibu kadhaa hivi lengo ni kujaribu kukusanya maelezo ambayo yatatuwezesha kukaa chini sasa kama Serikali tuweze kuona ni mfumo upi utakaotusaidia kukabiliana na tatizo hili la wafugaji. Yako mambo mengi sana ndani ya tatizo hili lakini tunadhani tukishughulikia kipande kimoja kimoja haitatusaidia. Kwa hiyo, tutaitisha kikao cha mikoa yote ambayo inashughulika na wafugaji na tutaomba na Wabunge vilevile washiriki kikamilifu tujadili hili jambo kwa kina halafu tuje na mtazamo ambao nafikiri utapunguza kama si kumaliza kabisa tatizo kati ya wafugaji na

wakulima. Tukimaliza hili nadhani tunaweza tukapata maelezo mazuri zaidi ya namna ya kushughulikia jambo hili.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa baadhi ya maeneo ambayo wanahamisha mifugo hii ni maeneo ambayo Serikali inayatambua, vitongoji vimesajiliwa huduma za jamii zimepelekwa, kama shule, nyumba za walimu na malambo; lakini sasa hivi Serikali inawahamisha. Je, Serikali haioni umuhimu wa kusitisha zoezi hili vinginevyo kuendelea hivyo ni kuwaonea wananchi kwa sababu wako pale kihalali?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, itakuwa ni vigumu kwa Serikali nikiwa Dodoma hapa niseme simamisheni kwa sababu ya hoja uliyoisema. Mimi natoka Rukwa, nina wafugaji zaidi ya 100,000 na tunaishi nao vizuri sana. Hatuna tatizo hata kidogo. Tatizo ni kwamba utaratibu wa hawa wafugaji kuhamia eneo moja kwenda jingine tatizo linatokea pale tu anapokuwa ameingia kinyemela bila utaratibu kufuatwa. Akiingia kwa mtindo kwamba anajitafutia eneo ambalo yeye anaona linafaa. Ndiyo maana unakuta kunakuwa na ugomvi kati ya wale waliokutwa na hawa ambao wamekwenda kwenye maeneo haya. Ndiyo maana mimi nasema hatujawa na maeneo Mkoani Rukwa popote ambapo tumehamisha wafugaji wakaacha shule, wakafanya nini hata Kilosa pale hatunalo eneo la namna hiyo. Ndiyo maana mimi nasema kuna kesi ambazo tunazijua hapa na pale lakini hawa unaweza mmoja mmoja ukawashughulikia na tatizo likabainika.

Mimi sitaki twende na hilo, twende na wazo pana zaidi kujaribu kuona tatizo kwa ujumla wake tulikabili vipi ili mtu anapotaka kuhama tujue anakwenda wapi; ameomba kibali kimekubalika amepangiwa eneo lijulikane na ikiwezekana lipimwe tujue kwamba hili ni kwa ajili ya wafugaji.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kukuuliza swali kuhusu ubora na uimarishaji wa miundombinu katika Mkoa wa Kagera. Katika ahadi ambazo Serikali yetu imeahidi kuzitekeleza ifikapo 2010 ni pamoja na uimarishaji wa barabara za lami kutoka Mtukula, Muleba mpaka Lusahunga. Kazi hii ilikwishaanza kufanyika lakini baadaye ikasimamishwa kwa sababu Serikali ilisema haikuridhika na utendaji kazi na yule mkandarasi. Ukatuahidi kwamba hiyo barabara ingeendelea kutengenezwa mwaka jana mwezi wa kumi mpaka sasa hivi tunavyozungumza hali ya barabara kutoka Muleba kufika mpaka Kyamyoro hadi Baharamulo ni mbaya na haipitiki ipasavyo.

Lakini kabla hujafika Muleba na kuendelea mpaka eneo la Kyamyoro kuelekea mpaka Chato hapapitiki kabisa na magari wakati mwingine yanashinda pale na yana abiria, mizigo, malighafi za viwanda na magari kama mafuta hali ambayo kimsingi inarudhisha nyuma Mkoa wa Kagera kiuchumi. Kila tunapoulizwa swali hili tunapewa majibu yanayotusogeza kwenye matumini lakini matumaini yasiyoweza kufikiwa.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujua ni kauli ipi ya Serikali na mpango upi uliopo wa kuitengeneza barabara hii haraka iwezekanavyo ukizingatia kwamba hivi

tunavyozungumza magari hayapiti na yakipita ni kwa tabu na mimi nimeathirika kwa hilo wakati nakuja hapa Bungeni juzi. Kwa hiyo, nasema kitu ambacho nimekishuhudia mimi mwenyewe ninapokizungumza nina uhakika nacho na hivi nimeambiwa hata leo na jana mvua inaendelea kuathiri barabara. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kauli yako?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana naye na kwa kweli nasikitika pamoja naye, nia ya Serikali katika jambo hili ni nzuri sana na ndiyo maana tulianzisha ule mradi mkubwa. Nataka nimhakikishie tu kwamba bahati nzuri na mimi nimekuwa nikilifuatilia jambo hili na nikuhakikishie kwamba Serikali inajipanga vizuri matatizo kama haya yanapotokea na inabidi wakati mwingine Serikali kuchukua hatua fulani ambazo wakati mwingine zinarejesha jitihada ambazo tulikuwa tumeanza nazo. Lakini nikuhakikishie kwamba Serikali inalijua na tunalifanyia kazi tutahakikisha kwamba jambo hili linakamilika mapema kama tulivyokuwa tumeahidi.

**MHE. JUMA S. N'HUNGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Swali langu mimi litahusu hali ya uchumi duniani. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba hivi sasa dunia inayumba katika hali ya uchumi na Tanzania sio kisiwa bila shaka nasisi inaweza ikatugusa hali hiyo. Ninazo habari kwamba mazao yetu kama pamba na mazao mengine yameshuka bei duniani. Baadhi ya taasisi zetu za fedha zimeshawahi kutoa mikopo kwa vyombo mbalimbali hasa vyama vya ushirika. Baadhi ya vyama vya ushirika vimeshanunua mazao hayo ambayo bei yake imeshuka. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba tutaathirika kwa kiasi fulani. Je, Serikali yetu ina mkakati gani wa kuona kwamba tatizo hilo tunaliepuka.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa N'hunga anachokisema ni kweli na palihitaji kwa kweli mtu kuulizwa sana juu ya jambo hili. Ni mtikisiko ambao unatugusa wote na mtakumbuka Bunge lililopita Serikali ilifanya jitihada Gavana wa Benki Kuu *(BOT)* akajaribu kutusaidia kujua upana wa tatizo na hatua mbalimbali ambazo Serikali imejipanga kuchukua. Lakini mimi nadhani kubwa hapa ni kwamba kila Serikali lazima itafute mbinu ya kukabiliana na tatizo hili la kiuchumi kwa maana ya maslahi ya nchi yake.

Kwa hiyo, tumemwomba Gavana wa Benki Kuu aandae taarifa ambayo itaainisha namna tunavyotarajia kukabiliana na jambo hili, itawasilishwa Serikalini hivi karibuni, tukishaijadili tutakuwa tumepata ufumbuzi wa baadhi ya maeneo ambayo tunafikiri tukabiliane nayo hasa lile la pamba ambalo ni kubwa sana. Lakini vilevile pengine Bunge hili tusifaulu lakini tutajitahidi tuhakikishe Bunge lijalo mapema mwanzoni pengine tupate taarifa hiyo tena kutoka kwa Gavana wa Benki Kuu ili muweze kujua Serikali kupitia hii *rescue package* imeamua mambo gani, itafanya nini kwa lengo tu la kushirikisha Bunge ili sisi wote pamoja tuweze kusukuma jambo hili kwa uelewa mmoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nataka kuwakumbusha kwamba kwa taratibu za Kibunge maswali yanatakiwa yawe ni swali bila dibaji ndefu kama inavyojitokeza hivi sasa. Dibaji hizi zinanyima haki Wabunge wengine. Wapo wabunge 11 sasa kila mmoja

akianza na dibaji najua Kiswahili ni lugha yetu, tunaipenda ni tamu unapenda usikike lakini lenga kwenye swali ndiyo utaratibu wa Kibunge.

**MHE. CHARLES N. MWERA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Kutokana na uhaba wa chakula ambao umeikabili nchi yetu, Serikali ni kawaida yake kuweka *barriers* sehemu za mipakani ili chakula kisivuke kwenda Kenya. Ni sababu gani za msingi zinazosababisha Serikali kuweka *barrier* katika Mto Kirumi chakula kisiende Wilayani Tarime na kusababisha vyakula vya nafaka kama mchele, mihogo pamoja na mahindi kupanda bei.

Je, viongozi ambao wako madarakani wanachukuliwa hatua gani za kinidhamu wanapokuwa wanawakosesha wananchi chakula kwa misingi hiyo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, suala la chakula Wilayani Tarime huwezi tu ukalirahisisha kiasi hicho kwa maana ya kwamba chakula chote kinachovuka pale Kirumi kinakwenda Tarime. Kubwa hapa ambalo tunalisema ni nini. Kama Serikali tunajua kwamba chakula kinavushwa kwenda Kenya kwa wingi sana kwa sababu ya mpaka ulivyo wazi na haujasimamiwa kwa kiasi kikubwa.

Kwa hiyo wakati nakubaliana na wewe kwamba inawezekana tukawa na matatizo ya hapa na pale katika maeneo ya Tarime ni vizuri vilevile ukaona upande wa pili wa Serikali kwamba ni lazima tuendelee kulinda ule wasiwasi wa chakula kutumia mwanya huo huo lakini kikawa kinavuka zaidi kwenda upande wa pili na tukajikuta pengine tume-*draw* vyakula karibu sehemu kubwa kwenda upande wa pili na sisi tukaathirika zaidi. Ndiyo maana unakuta kidogo tunakuwa waangalifu, hatukatazi *completely* hapana. Tunakuwa waangarifu sana kwamba kama kuna mahitaji ya chakula Tarime tulenge kweli maeneo ambayo chakula kitakwenda. Ndiyo maana unaona tunachukua hiyo tahadhari.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi naungana na wezangu kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Kwa kuwa ulinzi na usalama ni katika mambo ya Muungano na mara nyingi huwa ikiripotiwa wavuvi wetu wanaotumia vidau na raia wengi huwa wanafariki au kupata hasara au kupotea bila kupata msaada wowote kutoka kwenye vikosi maalum hasa baharini kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ndiyo wanapata maswahibu hayo. Mheshimiwa Waziri Mkuu Je, Serikali ina mkakati gani?

**SPIKA:** Mikakati kufanya kitu gani?

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Serikali ina mpango gani kiulinzi kupitia vikosi maalum kusaidia wananchi kunusurika na janga hilo?

**SPIKA:** Yaani baada ya ajali?

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Kuzuia na hata pale inapotokea kuokoa wale watu wanaopata matatizo baharini.

**SPIKA:** Basi kuokoa ni baada ya ajali.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Ndiyo Mheshimiwa Spika.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, pengine tuliweke kwamba, Serikali kwa upande wake kama tunao mfumo wa namna ya ku-*rescue* mambo yanapotokea baharini kama vile tunavyozungumza yakitokea hewani au sehemu nyingine yoyote jibu litakuwa ndiyo na hapana. Ndiyo kwa maana kwamba pale ambapo imetokea katika mazingira ambayo yanaipa Serikali nafasi au fursa ya kuweza kuwahi katika eneo la tukio na kuweza kuokoa hatua hizo zinachukuliwa.

Lakini yapo mazingira ambayo ni magumu hata kwa Serikali kuweza kubaini au kuwezesha pale mapema ili kusaidia kuokoa watu. Sasa katika mazingira kama haya inakuwa katika zile ajali ambazo zinasema ni bahati mbaya sana hatukuwa na namna nyingine ya kufanya.

Lakini niseme tu kwamba pengine kama Serikali ni kweli tuwe na mfumo mpana zaidi wa namna ya kusimamia masuala ya baharini kiulinzi, kiusalama si kwa maana ya ajali tu lakini kwa maana pana vilevile ya ulinzi kwa ujumla wake. Ndani yake pengine tunaweza tukawa na mifumo mizuri ambayo inaweza ikatusaidia kuwezesha mambo kama haya yanapotokea tuweze kuwa karibu na kuweza kuchukua hatua za kuokoa maisha ya watu.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ni heshima kubwa ambayo kama Mbunge unaweza kujivunia kupata nafasi hiyo. Swali langu ni kwamba je, Waziri Mkuu atafikiria kwa makini kuunda jopo la wataalam ndani ya nchi ambao wamebobea katika fani za uchumi na ustawi wa jamii katika kuangalia mtikisiko wa uchumi duniani ili wafanye kazi wakati wote tukizingatia nchi kama Marekani au za Ulaya sasa hivi kwamba hawana kazi nyingine na kila mara wana mikutano kama ule wa *G. 20* kuangalia suala hili la uchumi. Vurugu hizi ambazo wamezianzisha wao zitatuhusu sisi zaidi ambao wamejiunganisha na uchumi huu kwa njia moja au nyingine.

Je, Waziri Mkuu pia yupo tayari kuhakikisha kwamba Wabunge tunapata fursa hata ya siku mbili kujadili tu suala hili ili tuweze kuwaeleza wananchi matokeo yanayoweza kuwapata na ambayo wameshaanza kuyapata katika sekta za utalii, uvuvi, kilimo na nyinginezo.

Je, Waziri Mkuu unaweza hilo ukalikubali?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali kwamba Benki Kuu kwa sasa ndiyo wanafanya hiyo kazi ya kutazama hali ya uchumi na mwelekeo na matatizo yanayotokana na mtikisiko wa kiuchumi kwa sasa. Lakini kama nilivyosema Benki Kuu wameagizwa waandae taarifa na kuiwasilisha Serikalini ambayo

itatazama ni mikakati gani iwekwe au itakuwa imewekwa kukabiliana na hii hali ya kiuchumi tunayokwenda nayo na kile tulichokiita kitu kama *a rescue package.*

Serikali itaijadili hiyo taarifa na ndiyo maana nikashauri kwamba pengine baada ya majadiliano hayo hata hili la Mheshimiwa Mongela linaweza likajitokeza kama itaonekana ni vizuri likawepo. Lakini kama na Bunge kulishirikisha katika jambo hili nimekiri kwamba tutajitahidi tuhakikishe kwamba baada ya taarifa hiyo tulete jambo hili Bungeni kama tulivyofanya mwanzoni na kwa pamoja tuwe na uelewa mmoja. Kwa hiyo tutajitahidi kufanya hilo na hili jingine ulilotushauri tutaliwasilisha Serikalini tuone kama inawezekana.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imeonyesha nia dhahiri ya kupambana na rushwa na masuala ya utawala bora na kwa kuwa hivi sasa sehemu kubwa ya kitengo kinacholalamikiwa kati ya vitengo vinavyolalamikiwa katika masuala ya rushwa ni suala zima la ardhi, ugawaji wa viwanja na mashamba kwa sababu utaratibu wake, unajaza na unangojea uambiwe, unaweza kukaa hata miaka kumi. Kwa kuwa hivi sasa Dodoma, *CDA* imeonyesha utaratibu mzuri wakati walipokuwa wanagawa viwanja vyao hivyo vya Itega na vingine kwa kutangaza, watu walikwenda na Waheshimiwa Wakubwa au Wabunge walilazimika nao kuwekewa maeneo yao. Hii ni njia ya kuzuia rushwa. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni sasa ni busara utaratibu huu uliofanywa na *CDA*, aidha iwekwe sheria au iwekwe kanuni kwamba Halmashauri zote zifanye utaratibu huu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Zainab Gama kwa kuona kwamba *CDA* walichokifanya kimeonekana kukubalika na kupendwa na wengi. Kwa hiyo ni jambo la kuigwa na linaweza kabisa likaenezwa maeneo yote kwa sababu ni jambo jema. Baadhi ya Mikoa walijaribu kufanya hiyo kazi kama Mwanza pale, lakini pengine tutakachojaribu kuimarisha ni hii dhana kwamba mkishapima ili watu wajue kwamba kuna viwanja na viko vya ngazi gani, liwekwe bayana kwamba tuna viwanja kadhaa, yeyote anayetaka sasa anaweza kuja na kuomba. Lijulikane, liwekwe wazi, nadhani ndiyo *point* kubwa ambayo unaizingatia pale katika kupunguza rushwa na kugawana gawana vitu ambavyo wakati mwingine havina maana sana. Kwa hiyo, mimi nafikiri tutalisimamia, tutafanya hivyo, tutatoa maelekezo ili kila Halmashauri itumie utaratibu wa kutangaza kila viwanja vinapokuwa vimepimwa tayari. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge huo ndio mwisho wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Namshukuru sana. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 29

**Biashara ya Dawa za Kulevya na Bangi Nchini**.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali na taasisi zake zinazohusika na uuzaji wa biashara ya madawa ya kulevya inajitahidi sana kupiga vita biashara hiyo:-

(a) Je, Serikali inajua kuna matangazo ya bangi ambayo hutangazwa hapa nchini kwa kutumia michoro ya jani kwenye nguo, kofia na *Stickers?*

(b) Je, Serikali haioni kwa wale wanaotangaza biashara hiyo wanachochea utumiaji wa bangi nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, lenye sehemu (a), na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina taarifa ya kuwepo matangazo ya bangi ambayo hutangazwa hapa nchini kwa kutumia michoro ya jani kwenye nguo, kofia, *stickers* na kadhalika. Hata hivyo, kutokana na uingizwaji wa nguo chakavu na bidhaa nyingine hapa nchini kutoka nchi za nje, inawezekana kabisa michoro hiyo ikawepo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali kwamba michoro na matangazo kama hayo yanachochea au kuleta mwamko au kumvutia na kumhamasisha mtu kutumia dawa za kulevya kama bangi na dawa zinginezo. Kutokana na hali hiyo, Serikali imeshaanza mchakato wa kushughulikia tatizo hili lenye kuhamasisha utumiaji wa bangi na aina nyingine za dawa za kulevya kwa umakini ikiwa ni pamoja na kuandaa rasimu ya sera ya kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya.

Aidha, wadau wa udhibiti wa biashara haramu ya dawa za kulevya wanaendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwezo kukemea hali hiyo pamoja na kuangalia uwezekano wa kuifanyia marekebisho sheria ya kuzuia Biashara haramu ya dawa za kulevya Namba 9 ya 1995 ili hali hiyo iweze kudhibitiwa. Iwapo marekebisho hayo yatapitishwa, hatua kali dhidi ya wahusika wote zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria tajwa.

**MHE. MWAKA ABDULRAHAMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inajitahidi sana kupiga vita dawa za kulevya. Je, Serikali imejiandaaje kuwapatia tiba na elimu waathirika wa dawa za kulevya nikimaanisha kwa upande wa vituo na ma-*doctor*?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zingine za kujaribu kuwatibu waathirika wa dawa za kulevya, Serikali kwa kuanzia imeunda Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya. Lakini pia imeanzisha Vitengo vya Matibabu katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili na pia Hospitali ya Mirembe hapa Dodoma.

Na. 30

**Funzo Kutokana na Uchaguzi wa Marekani**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa, tarehe 4 na 5 Novemba, 2008 chombo chetu cha Habari cha *TBC* kilitumia muda mwingi sana kutangaza moja kwa moja mchakato mzima wa uchaguzi wa urais wa Marekani:-

(a) Je, Tanzania imejifunza nini katika uandikishaji wa wapiga kura, upigaji wa kura, uhesabuji wa kura, utangazaji wa matokeo na yaliyofuata baada ya kutangazwa kwa mshindi?

(b) Kutokana na kujifunza huko, Tanzania inakusudia kufanya marekebisho gani katika uchaguzi ujao wa mwaka 2010?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salimu Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kufuatia uchaguzi wa Marekani uliofanyika tarehe 4 Novemba, 2008 Tanzania imejifunza mambo yafuatayo:-

(i) Uchaguzi wenye kuleta mafanikio mazuri ni ule unaofanyika katika mazingira ya amani na utulivu na ambao maandalizi yake yanafanywa kwa uhakika na umakini sana.

(ii) Utaratibu wa kuandikisha wapiga kura nchini Marekani unatofautiana sana kutoka jimbo moja hadi jimbo jingine, kwani kuna majimbo ambayo mpiga kura anajiandikisha kabla ya siku ya uchaguzi na kuna yale ambayo mpiga kura anajiandikisha na kupiga kura papo hapo, na bado kuna mengine ambayo yanaruhusu njia zote hizo.

Hii ni kutokana na kuwepo kwa teknolojia ya juu sana inayowezesha kufanya hivyo. Aidha, kwa utaratibu wa Marekani hakuna kitambulisho cha mpiga kura na hili linatokana na maendeleo ya teknolojia na kila mwananchi kuwa na utambulisho maalum.

Ili kuweza kupiga kura mpiga kura anaenda kituoni na kutaja jina na akionekana kwenye kopyuta jina lipo, hivyo anapiga kura. Kama jina halimo anatakiwa kutoa utambulisho kama leseni au ankara ya ulipaji bili za maji au umeme katika eneo analoishi.

(iii) Zoezi la kupiga kura na kuhesabu kura nchini Marekani huchukua muda mfupi sana kutokana na matumizi ya mashine za kupiga kura na kuhesabu. Upo pia utaratibu kwa marekani wa kupiga kura kabla kwa wale walio nje ya Marekani *(early voting or absentee voting).*

(iv) Utaraibu wa wazi katika kutoa matokeo ya uchaguzi yanayovyopatikana.

(v) Utaratibu wa Rais kuchaguliwa kwa *electral votes* badala ya *popular votes*, ambao unaondoa haki halisi ya wapiga kura kwa sababu mgombea anaweza kushinda kwa popular *votes* na asiwe Rais. kwa maana nyingine mtu anaweza kusema Rais wa Marekani hachaguliwi na raia wa Marekani wote isipokuwa anachaguliwa na *Electral College.*

Mheshimiwa Spika, Tanzania imejifunza kutokana na uzoefu wa nchi mbali mbali duniani na siyo Marekani pekee katika kuboresha mfumo na mchakato wa uchaguzi. Marekebisho ya sheria uchaguzi yamekuwa yakifanyika mara kwa mara ili kuwezesha uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kuwa huru na wa haki zaidi. Marekebisho ya mwisho yalifanyika mwaka 2005 na mengine yanatarajiwa kufanyika kabla ya uchaguzi wa mwaka 2010 na baadhi ya mambo tuliyojifunza Marekani na kwingineko yanaweza yakaingizwa katika marekebisho hayo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Moja, katika mambo tuliyojifunza katika uchaguzi wa Marekani ni kutotumia majeshi katika uchaguzi wao. Lakini Tanzania katika uchaguzi wa mwaka 2005 ilipeleka wanajeshi wengi sana Zanzibar, inasemeka baadhi yao hata kutoka nchi jirani, jambo ambalo liliwatia hofu sana wapiga kura, inasemekana baadhi ya wapiga kura hawakwenda kupiga kura. Je, Serikali sasa iko tayari kuwatangazia Watanzania kwamba katika uchaguzi ujao wa 2010 haitarejea kosa hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tumejifunza katika uchaguzi wa Marekani ni kwamba hakukuwa na ubaguzi wa aina yoyote hata ikafanya mtu wa kwanza mwenye asili ya Afrika Obama kuwa Rais wa Marekani.

Lakini katika uchaguzi uliopita 2005 hapa Tanzania, tatizo la asili na kabila la mtu lilijitokeza, kwamba baadhi ya watu hawakuwa na sifa za kuwa watawala wa nchi hii kwa sababu ama ya asili yao au kabila lao. Je, Serikali italiondoa vipi tatizo hili la aibu hapa nchini hasa baada ya kujifunza kutoka Marekani?

**SPIKA:** Hili la pili siyo wazi. Swali la nyongeza la pili lina mafumbo mafumbo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri swali la kwanza uweze kulijibu. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli sina uhakika kama kweli majeshi yalitumika katika kusimamia uchaguzi kwa sababu katika nchi yetu hali ya ulinzi na amani inashughulikiwa na Jeshi la Polisi. Lakini, kama aliwaona wanajeshi wengine katika

Jimbo lake au kwingineko, wanajeshi hao basi walikuwa wanatekeleza haki yao ya kupiga kura kama raia wengine. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Tanzania kidogo una tofauti na wan chi zingine kwa sababu kuna Tume mbili za Uchaguzi. Kuna Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Katika mazingira haya basi,kama kuna massuala ambayo yanaigusa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, basi dukuduku na masuala hayo yaelekezwe kunakohusika, na kwa yale yanayohusu Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano, Bunge hili ndio mahala pake. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Waziri anafahamu kwamba muda mrefu Tume ya Uchaguzi ya Taifa, *Agent* wake ni Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na kwamba chaguzi zote ambazo zimesimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar vile vile zilikuwa zinasimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Muungano na kwa sababu hiyo basi, wale Wabunge wa Jamhuri ya Muungano ambao wanasimamiwa na Tume ya Taifa ya Muungano vile vile walikuwa wakisimamiwa na Tume ya Zanzibar.

Kwa hiyo, siyo kweli kwamba uchaguzi wa Zanzibar unasimamiwa tu na *ZEC* peke yake, kwa Wabunge unasimamiwa na *NEC* na *ZEC* pamoja, una habari hizo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Tume ya Uchaguzi Zanzibar ni wakala wa Tume ya Uchaguzi yaJamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa chaguzi za Wabunge Zanzibar. Mheshimiwa Mbunge aelewe kwamba wakala ni wakala, hawezi akapora madaraka ya mwenyewe. Sheria inayotumika ni sheria ya uchaguzi ya mwaka 1985 ambayo imepitishwa na Bunge hili.

Kwa hiyo, naamini kwamba uchaguzi wa Wabunge wote unasimamiwa sawa sawa japokuwa kwa upande wa Zanzibar, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ndiyo wakala wa Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano, lakini sheria inayotumika ni moja. *(Makofi)*

Na. 31

**Barabara ya Tunduma – Sumbawanga**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE (K.n.y. MHE. ELIETA N. SWITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Tunduma – Sumbawanga imo katika mpango wa kujengwa kupitia fedha ya *Millenium Challenge Cooperation (MCC).*

Je, barabara hiyo itajengwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elieta N. Switi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukiri kuwa ni kweli barabara ya Tunduma – Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 224 itajengwa kupitia mpango wa *Millenium Challenge Cooperation*. Kwa sasa zoezi linaloendelea ni kufanya mapitio ya usanifu wa barabara kwa maana ya kupata *design* iliyokamilika, kuelewa gharama za ujenzi, kupata tathmini ya hali ya mazingira, kufahamu mpango wa fidia na makazi mapya pamoja na kukamilisha nyaraka za kuitisha zabuni kulingana na miongozo ya *MCC*. Kazi hii inafanywa na Kampuni ya Kihandisi *M/S Africon Ltd.* kutoka Afrika Kusini. Zoezi hili lilianza mwezi Aprili, 2009 na linatarajiwa kukamilika ifikapo Agosti, 2009. Baada ya kukamilika kwa zoezi hili ambalo ni muendelezo wa usanifu wa awali uliofanywa na *TANROADS*, zabuni za Wakandarasi wa ujenzi zitaitishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii ni ndefu, ujenzi wake umegawika katika sehemu tatu kama ifuatavyo:-

Barabara ya Tunduma Ikana (Km. 64) na barabara ya Ikana – Laela (Km. 64). Zabuni za ujenzi kwa barabara hizi mbili zitatolewa mwezi Septemba, 2009 na mkataba wa ujenzi unatarajiwa kusainiwa Februari, 2010 na hivyo ujenzi kuanza Machi 2010 na kukamilika Februari, 20012. Barabara ya Laela – Sumbawanga (Km. 96), zabuni zitatolewa mwezi Septemba, 2009, mkataba wa ujenzi utasainiwa Desemba, 2009 na ujenzi kuanza Januari, 2010 na kukamilika ifikapo Septemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuona kuwa barabara hii pamoja na miradi mingine inayogharimiwa na Serikali ya Marekani chini ya mpango wa *MCC* inakamilika mapema iwezekanavyo. Aidha, napenda ifahamike kuwa utekelezaji wa mpango wa *MCC* ni wa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2008/2009.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninaomba nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ajue kuwa wananchi wa Rukwa wanapata tabu sana. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya Tunduma – Sumbawanga, kwa kipindi hiki mvua imenyesha sana na barabara imeharibika mara tatu. Wananchi wa Mkoa wa Rukwa sasa hivi wanapata tabu sana, kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga watu wanachukua siku tatu.

Je, Serikali ina mikakati gani ya dharura ya kutengeneza ile barabara kwa vile sasa hivi imeachwa kabisa, wala haina hata greda ambalo unaweza kusema litengeneze mashimo yaliyo katika ile barabara?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa wamechoka kusikia kila siku mipango ambayo inapangwa ambayo haitekelezwi.

Je, Serikali ni lini inawaambia wananchi wa Rukwa magreda yatakaa siku gani katika barabara yaanze kutengeneza?

**SPIKA:** Ni marudio ya swali lile lile. Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, maswali mawili ya nyongeza ambayo ni lile lile moja!

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kama alivyojibiwa swali la msingi, taratibu zinaendelea kwa ujenzi wa barabara ya Tunduma – Sumbawanga.

Lakini kwa hii taarifa ambayo sasa hivi Mheshimiwa ameitoa ya hali mbayaya barabara kule, nitawasiliana na Mamlaka, *TANROADS* Mkoa ili iangalie taratibu za haraka za kuwezesha walau barabara hiyo kupitika kwa dharura kwakipindi hiki kigumu.

Lakini, uendelezi wa ujenzi utaendelea chini ya *MCC* kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu.

Na. 32

**Gari Zenye Usajili wa Zanzibar Kuzuiliwa Bandarini**

**MHE. ISSA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na kero ya muda mrefu juu ya magari yenye usajili wa Zanzibar kuzuiliwa Bandarini Dar es salaam hadi itolewe *certificate* ya usajili wa gari; na kwa kuwa magari yanayotoka Dubai, Japan, yanapolipiwa ushuru huruhusiwa kuondoka na gari bandarini bila ya *Certificate* ya Usajili wa gari hilo:-

(a) Je,kwa nini gari zinazotoka Zanzibar huwa zinazuiliwa?

(b) Je, kwa nini gari zinazotoka Dubai, Japan huwa zinatolewa bandarini bila *Certificate* ya Usajili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mbunge wa Mpendae, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, gari zinazotoka Zanzibar huwa hazizuiliwi bandarini Dar es salaam, bali zimewekewa utaratibu maalum wa kutambua kwamba zimesajiliwa Zanzibar. *TRA* huhakikisha kwamba *Certificate of Customs Clearance* inapatikana katika kipindi kifupi ili mwenye gari anapokamilisha taratibu za kiforodha aweze kuruhusiwa kutoa gari lake bandarini na kutumia namba za usajili za Zanzibar.

Kutokana na utaratibu huo, vibao vya namba za usajili Zanzibar huwa having’olewi bandarini wakati gari linapoingizwa Tanzania Bara. Utaratibu huu

umewezesha gari zenye namba za usajili wa Zanzibar kuweza kutembea katika barabara za Tanzania Bara bila *Foreign Vehicle Permit*, ikiaminika kwamba wenye gari wana kibali cha miezi mitatu toka Shirika la Magari Zanzibar au wamo mbioni kupata namba za usajili Tanzania Bara. Utaratibu huu hutumika kwa gari zilizosajiliwa kwa kutumia Sheria ua Usajili wa magari wa nchi nyingine.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa gari zinazotoka Dubai, Japan au nchi nyingine, vibao vyote vya Namba za usajili vinavyokuja katika gari hizo huwa vinang'olewa mara shehena iliyobeba gari hizo ifikapo bandarini. Baada ya taratibu zote za kiforodha kukamilika, magari hayo hutolewa bandarini na Namba za *garage* ambazo zimelipiwa bima kwa ajili ya kuzifikisha gari hizo zinapotakiwa kwenda. Hairuhusiwi kabisa mmiliki wa gari kutembeleza gari lake likiwa na namba za *garage*.

Baada ya kupata *Certificate of Customs Clearance*, gari hizo huruhusiwa kutembea katika barabara za Tanzania Bara ndani ya mwezi mmoja, kipindi ambacho wamiliki wa gari hizo hutakiwa wawe wamekamilisha taratibu zote za kupata namba za usajili toka katika mamlaka ya usajili wa magari Tanzania Bara. Taratibu hizi hazitumiki kwa gari zinazotoka Zanzibar kuja Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ambapo sheria zetu za usajili wa gari kati ya Tanzania Bara na Zanzibar bado ni tofauti, utaratibu unaotumika sasa wa kuondosha gari zenye namba za usajili za Zanzibar ziingizwapo Tanzania Bara ni nafuu kuliko ule unaotumika wa kuondosha gari zitokazo nje ya Tanzania.

Pamoja na jitihada hizi, Wizara yangu ipo tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge katika kupokea ushauri wowote juu ya uboreshaji wa uingizaji na uondoshaji wa gari kutoka Zanzibar kuja Tanzania Bara kwa kupitia bandari zetu.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majawabu yake, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, Waziri atatueleza nini kwa zile gari zilizowekwa zaidi ya wiki moja bandari ya Dar es salaam ambazo zimekamilisha taratibu zote za usajili, atatueleza nini katika hatua hiyo?

La pili, ningalipenda atueleze kwa zile gari ambazo zimetolewa ushuru katika mtandao wa *scudo plus plus*, kwa nini zinazotoka Zanzibar zikifika Dar es salaam hulipiwa ushuru mara ya pili? Naomba jawabu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, suala lake la kwanza anasema kuna gari ambazo zimeishakamilisha taratibu na ziko pale zaidi ya wiki moja. Nataka nimhakikishie kwamba gari ambayo imekamilisha taratibu zote za kiforodha na za kiusajili, zinatakiwa zitoke katika kipindi hicho kwa sababu katika maeneo ambayo magari yale yapo forodha wanayahitaji ili kuweka mizigo mingine.

Lakini kama hili ni tatizo ambalo linamsumbua, nataka nimhakikishie kwamba nitalifuatilia ili kuweza kuona kwamba gari iliyokamilisha taratibu inatoka katika kipindi kilichokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, suala lake la pili anasema kwamba kuna gari ambazo zimeishalipiwa ushuru kupitia Zanzibar, lakini zinapokuja Tanzania Bara huwa zinatozwa ushuru wa ziada. Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu ambao unafanyika ni kwamba, kuna mawasiliano ya mtandao ambao uko Tanzania Bara. Mawasiliano hayo ndiyo yanayotupa *information* za kutosha kwamba gharama ya gari lile ni kiasi gani. Sisi tunachojaribu kukifanya hivi sasa ni kuhakikisha kwamba mawasiliano yale nayo tunayafikisha Zanzibar ili gari litakapofika Zanzibar liweze kutozwa ushuru pale pale Zanzibar kupitia mtandao ambao uko Zanzibar na hatimaye likifika Tanzania Bara liwe halitozwi tena ushuru na gari lile linafanya *procedure* nyingine na liweze kutoka kama kawaida.

Na. 33

**Mapato Yanayokusanywa na COSOTA**

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuza:-

Kwa kuwa *COSOTA* ni chombo kinachosimamia kazi za sanaa na chenye wajibu wa kukusanya mrahaba kutoka kwenye redio, televisheni, *Supermarkets* na kadhalika:-

(a) Je, ni wasanii wangapi wamejiunga na *COSOTA?*

(b) Je, tangu *COSOTA* ianzishwe imekusanya mapato kiasi gani toka vyombo husika?

(c) Je, ni wasanii wangapi wanachama ambao wanafaidika na mirahaba hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *COSOTA* ilianza kufanya kazi zake mwaka 2001 kwa mujibu wa Sheria ya Hakimiliki Na.7 ya mwaka 1999, na mpaka sasa ina wanachama wapatao 1566, kati yao watunzi na wasanii ni 809, watunzi na waigizaji 220, watunzi wa kazi za maandishi 315 na wachapishaji/wazalishaji 42.(b)Mheshimiwa Spika, *COSOTA* ilianza zoezi la kukusanya mirahaba mwaka 2006 baada ya kupitishwa kwa kanuni za utoaji leseni za maonyesho ya umma na utangazaji ya mwaka 2003. Kuanzia Mei, 2006 hadi Juni, 2008, *COSOTA* imekusanya Shilingi 306,327,040.33 kutokana na maonyesho ya umma yaani kwenye mabaa, *supermarkets*, migahawa, mahoteli na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mirahaba kutoka vyombo vya utangazaji bado haujaanza. *COSOTA* iko kwenye majadiliano na vyombo vya utangazaji hasa redio na televisheni ambavyo vitatumia kazi za wasanii ili kuona jinsi vyombo hivyo vitakavyoweza kuanza kutoa mirahaba.

(c)Mheshimiwa Spika, mpaka sasa *COSOTA* imetoa migao sita ya mirahaba kwa wanachama wake wapatao 956. Katika wanachama hao, wanachama wa fani ya muziki ni 784 na fani ya maigizo ni 172.

Juhudi za pamoja kati ya *COSOTA*, wasanii, wazalishaji wa kazi za wasanii na wananchi kwa ujumla zinahitajika ili kuwalinda na kuongeza kipato cha wasanii nchini, pia kuvutia wawekezaji zaidi katika sekta ya usanii na muhimu zaidi Serikali kuweza kukusanya mapato yake kwa njia ya kodi bila matatizo.

Hivyo, namwomba Mheshimiwa Mlata ambaye amekuwa mtetezi mahiri wa maslahi ya wasanii wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge wote, muendelee kutupatia ushirikiano kama ilivyo kawaida ya Bunge hili tukufu hadi malengo haya mazuri yafikiwe.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyonyeza.

Kwa kuwa katika majibu yake Naibu Waziri mwenyewe amekiri wazi kwamba vyombo vya utangazaji bado havijaanza kutoa mirahaba kwa kazi za wasanii na wakati ule ule ninavyofahamu vyombo hivi vimekuwa vikilipa mirahaba kwa kazi za wasanii wa nje. Na kwa kuwa vyombo vya utangazaji vipo chini ya mamlaka ya utangazaji Tanzania.

(a)Je, Waziri atakubaliana nami kwamba Serikali itoe agizo kwa mamlaka ya utangazaji Tanzania kuwabana vyombo vya utangazaji ili kuweza kulipa mirahaba kwa kazi za wasanii wakati wanapoenda ku-*renew* leseni zao.

(b)Kwa kuwa, utaratibu wa *COSOTA* wanapotoa taarifa kwa wasanii na mgao wa fedha umekuwa si mzuri kwa sababu hata wengine bado hawana taarifa na wengine hawajapata pesa hizo. Je, Wizara yake sasa iko tayari kuiagiza *COSOTA* ili iweze kuwafuata wasanii waliopo mbali ambao hawajaweza kupata taarifa na wao ni wanachama ili waweze kupata akaunti zao na kuwawekea pesa zao kwenye akaunti kuliko kuzifuata Dar es Salaam.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko naomba kumjibu Mheshimiwa Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, maswali yake mawili ya nyongeza kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala hili la haki miliki na haki shiriki kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni suala ambalo geni zaidi katika nchi yetu kuliko masuala mengine ambayo tumeyazoea ya kibiashara na ndiyo maana haya ambayo Mheshimiwa

Mlata anayasema tunakubaliana naye kimsingi kwamba ni muhimu kabisa vyombo vya utangazaji, redio na televisheni viwalipe mrahaba wasanii wa Tanzania ili kuwazuia wasije wakakimbilia huko nje ambako wana uhakika wa kulipwa mirahaba hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile upo umuhimu wa kutoa taarifa kwa wasanii popote pale walipo badala ya wao kufuata malipo yao Dar es Salaam ni suala la msingi.

Jambo ambalo tunafanya na ambalo Wizara inafanya ni kwamba imeanza utaratibu wa kukutana na wadau mbalimbali katika sekta zote ambazo zinahusiana na mambo ya biashara, viwanda, masoko katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wetu wa kazi kuna taarifa kwamba tutakutana na wadau wote wanaohusika na suala hili la hakimiliki na hakishiriki na hasa suala hili la wasanii wa muziki na wengineo, ili kwa pamoja tukae tuweze kuweka mawazo yetu pamoja na kuazimia ni jambo lipi lifanyike, kuliko kutoa tu tamko la kuamuru wafanye inaweza isifanyike kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anapenda.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia kwamba hilo la ushirikishwaji tutalifanya na tutapenda sana kupata mawazo yake na mawazo ya Wabunge wengine ambao wanapenda suala hili ili kwa pamoja tufikie muafaka mzuri, wasanii wa Tanzania waweze kubaki hapa nchini na Serikali iendelee kupata mapato yanayotokana na kazi zao.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *COSOTA* ni chombo kinachosimamia kazi za wasanii na kwa kuwa wasanii hao ili wafanye kazi zao vizuri wanahitaji elimu. Je, katika eneo hili la elimu *COSOTA* inawasaidiaje wasanii wa Tanzania ili kuinua mapato yao na kuondokana na umaskini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, biasha na Masoko, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Bakari, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jibu lake ni hili ambalo nilikuwa nazungumzia hapa kwamba upo umuhimu wa kuwakutanisha wadau wote ambao wanahusika na suala hili, tutakapoongea hatutaongea tu suala la malipo tutaongea vilevile ni namna gani ya kuwapa elimu wapi wafahamu kwamba wakifanya kazi zao za kisanii, ni wapi watakwenda kudai, utaratibu gani wahakikshe kwamba wanapata mapato ambayo ni ya haki na vile vile ni utaratibu gani ambao wataweka kuhakikisha kwamba ukusanyaji wa mapato hayo hauwi na gharama kubwa kuliko hata mapato yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala la elimu napenda kumhakikishia Mheshimiwa Faida tutalizingatia katika mchakato mzima kuhakikisha kwamba wasanii wetu na hata

watumiaji wa kazi za kisanii wanafahamu nini kifanyike kwa ajili ya kurahisisha zoezi zima la biashara ya kazi ya msanii.

Na. 34

**Uonyeshaji wa Picha Zisizofaa Kwenye TV**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa *TV* nyingi nchini zimekuwa zikionyesha picha nyingi ambazo hazifai kuonekana na watoto wetu na watu wazima ambao ni *allegic* na picha hizo kama maiti zilizoharibika kupita kiasi ambapo picha zingine hushtua watu:-

Je, kuna kitengo kinachopitisha picha hizo kabla ya kuzitoa hadharani?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kukiri kupitia Bunge lako Tukufu kwamba baadhi ya vituo vya televisheni hapa nchini vimekuwa vikionyesha picha ambazo hazifai na ambazo hazipaswi kuonwa na watoto wetu na hata watu wazima vile vile kutokana na picha hizo jinsi zilivyo.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini vipo vyombo vilivyoundwa na Serikali katika kusimamia sheria zinazozuia urushaji wa vipindi na uonyeshaji wa picha bila kuzingatia maadili na maslahi ya Taifa. Vyombo hivyo ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) yenye jukumu la kusimamia shughuli za mawasiliano na sekta ya utangazaji kwa mujibu wa sheria Na. 12 ya mwaka 2003 iliyounganisha Tume ya Mawasiliano (*TCC*) na Tume ya Utangazaji (*TBC*). Aidha, Kamati ya Maudhui imeundwa kwa madhumuni hayo hayo. Chombo kingine ni Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza yenye jukumu la kukagua filamu kwa mujibu wa sheria Na. 4 ya mwaka 1976, sehemu ya *IV*, Kifungu cha 14(2) kinachohusu maonyesho ya filamu.

Mheshimiwa Spika, napenda ifahamike kwamba uonyeshaji wa picha zisizofaa kwenye *TV* ni uvunjaji wa maadili, kanuni na sheria za utangazaji. Vituo vyote vya televisheni nchini hutakiwa kuzipitisha picha zote kabla ya kuzirusha hewani.

Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano ina mitambo ya kufuatilia maudhui yanayorushwa na vyombo hivyo vya habari. Mamlaka imekiri kupokea malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu uonyeshaji wa picha zisizofaa na nyingine zinazokinzana na maadili ya dini na utamaduni wa Watanzania. Mamlaka imechukua hatua zifuatazo kwa vituo ambavyo vimekwenda kinyume na taratibu za utangazaji nchini:-

(i) Tangu mwaka 2007, Kituo cha *ITV* kilionywa mra mbili, Kituo cha *TBC One*, mara tano, *Star TV* mara moja na *Channel Ten* mara mbili.

(ii)Pamoja na kuandika barua za onyo, Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania katika ziara ya kutembelea vituo vya televisheni vya *ITV* na *TBC*, ilisisitiza umuhimu wa kufuata sheria na kanuni za utangazaji na kuvionya vyombo ambavyo vinarusha picha zinazokiuka maadili na kanuni za utangazaji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Wizara inapenda kuchukua fursa hii kuvikumbusha vituo vya televisheni nchini kuzingatia kanuni na sheria za utangazaji ili kuepusha kurusha picha zenye maudhui yasiyofaa kwa jamii hususan watoto wadogo.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika ahsante, majibu ya Naibu Waziri yanaridhisha lakini ninalo swali dogo tu la kuuliza.

(a)Mheshimiwa Spika, katika vituo vinavyoongoza kwa kuonesha picha zisizofaa ni *TBC ONE* ambacho ni chombo cha Serikali, Serikali inasema nini chombo chake kudhalilisha wananchi?

(b) Mheshimiwa Spika, vyombo vya *TV* kwa karibuni vimekuwa vinatumiwa kama chombo cha kuonyesha watu wenye magonjwa ya ajabu ajabu, imekuwa kama ni miradi, picha zile hazipendezi kuangalia machoni, na ni watu wagonjwa sana, wakiomba watu wawafadhili ili wakatibiwe, aidha Muhimbili au kupelekwa nje.

Hata kule Dar es Salaam kuna mwingine ukipita barabarani anakuonyesha kidonda ambacho ni zaidi ya miaka miwili anatembea nacho na hospitali tunazo, ninachouliza Serikali ni kwamba hivi kweli picha hizi kuoneshwa kwenye *TV* watu wanaomba wakati sisi viongozi tunapelekwa nje kutibiwa, tunashindwa kutibia hawa watu wachache ambao wanaomba misaada kwenye *TV* mpaka wanadhalilisha nchi na hizi picha hazifai?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa habari, Utamaduni na Michezo napenda kumjibu Mhehsimiwa Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, maswali yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili la kwanza napenda nitoe elimu na niseme si kweli kwamba *TBC ONE* inadhalilisha Serikali, pamoja na kuweka vyombo vya kudhibiti kuonesha picha ambazo si nzuri kwa umma. Lakini ni vizuri Waheshimiwa wakaelewa kwamba unaposoma taarifa ya habari sasa hivi katika dunia hii ya utandawazi taarifa ya habari inaweza ikaoneshwa kwa njia ya *internet* toka huko inakotoka na hiyo picha inatoka kama inavyotoka na *TBC* wote tukubaliane hapa kwamba ni chombo ambacho sasa hivi ndiyo kinaongoza kuonyesha taarifa ya habari nzuri Tanzania.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata ile kampuni ambayo inapima viwango katika Afrika ya Mashariki na Kati imeipa *TBC* namba one. Hilo ni moja lakini la pili tuko katika dunia ya utandawazi katika dunia ya utandawazi hakuna kinachofichika, vitu vingi vinaonekana katika vyombo vingine si *TBC* peke yake. Kwa hiyo, mimi nataka nisikubaliane naye kabisa kwamba *TBC* inadhalilisha Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni suala ambalo linafanyika dunia nzima si Tanzania peke yake na Tanzania si kisiwa ni nchi kama nchi nyingine zozote. Njia rahisi ya kutatua tatizo ni kuonekana kwenye umma na ndiyo maana mtu anapokuwa na tatizo anakwenda kulionesha ili kuweza kupata msaada. Ukikaa nalo wewe mwenyewe nani atajua kwamba una tatizo, ndiyo maana kuna magazeti, televisheni na vyombo vingine, ndiyo maana yake.(*Makofi*)

Na. 35

**Matumizi Mabaya ya Taa za magari na Askari Kutokuwepo barabarani usiku**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, mafunzo ya kuendesha magari nchini hufanyika wakati wa mchana na kwamba madereva wanafunzi hukosa kujua matumizi ya taa za magari na kusababisha baadhi yao kutumia taa za kuonea mbali na *sport lights* mijini muda wote usiku:-

(a) Je, Serikali inaonaje dosari hii na itarekebisha vipi?

(b) Je, kwa nini askari polisi wa barabarani (*Traffic Police)* hawaonekani barabarani usiku mijini hadi pale wanapoitwa kwa matukio ya ajali?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshmiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na tabia ya baadhi ya madereva kukiuka matumizi ya taa za magari nyakati za usiku kama kifungu cha 39 (c) (4)-(6) cha sheria ya usalama wa barabarani Na. 30/1973 (R.E 2002) kinavyoelekeza.

Tabia hii tunaamini kwamba haitokani na mfumo wa mafunzo yanayotolewa na vyuo vyetu kwani madereva wanaposomea udereva hufundishwa kanuni zote ikiwemo matumizi ya taa za kuona mbali (*full lights and sport lights*). Hata hivyo Wizara yangu itafuatilia suala hili la matumizi mabaya ya taa za magari.

(b)Mheshimiwa Spika, Askari Polisi wa kikosi cha usalama barabarani wamekuwa wakifanya kazi zao kwa masaa ishirini na nne kwa mujibu wa wa muuongozo

wa Jeshi la Polisi unavyoelekeza. Kazi hizo ni pamoja na kuzuia matukio ya ajali na kuhudumia walioathirika na matukio ya ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, katika kuzuia matukio ya ajali barabarani wamekuwa wanaongoza magari wakati wa msongamano inayotokana na ubovu wa Miundombinu ya barabara zetu na wingi wa magari kwani kwa kawaida ilipaswa madereva watii alama za barabarani ikiwemo taa na alama zilizochorwa barabarani na kwenye mataa. Inapotokea kuwepo na tatizo la msongamano wa magari wamekuwa wanafanya kazi hasi usiku.

Lakini pia askari hao wanakuwa katika vituo vya polisi muda wa saa 24 kuhudumia wananchi kadri wanavyopokea taarifa za matukio ya ajali.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Wazirinapenda kuuliza swali moja lakini kabla sijauliza napenda kupongeza juhudi zinazofanywa katika kudhibiti matukio ya ajali barabarani.

Mheshimiwa Spika, sijui kama Waziri anaelewa kwamba kumezuka tabia ambayo karibu inataka kuharibu sifa hiyo nzuri nayo ni hiyo ya kuvizia madreva, *Traffic Police* wanajificha kwenye vichaka wanatokea kwa ghafla na wakati mwingine wanaweza kusababisha ajali. Je, Waziri analijua hili na kama analijua anasemaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru kwa pongezi ambazo amezitoa kwa Jeshi la Polisi wa Barabarani kwa kazi wanayoifanya, kuhusu suala la askari Polisi ambao wanakaa na kujificha katika vichaka na kuvizia wakati magari yanatokea hilo nimelipokea na tutalifanyia kazi kuhakikisha kwamba kweli naelewa kwamba inapotokea ghafla inaweza ikasababisha madhara mengine.

Hiyo ni kweli na kwa kuwa tumelipokea tutalifanyia kazi na tutahakikisha kwamba mambo kama haya hayaendelei, nakushukuru.

Na. 36

**Mpango wa Kuzalisha Umeme wa Upepo**

**MHE. ABDULKARIM E. SHAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilikwishatenga kiasi cha shilingi milioni 35 kwa ajili ya utafiti wa mpango wa kuzalisha umeme kwa upepo (*Windmill study*) na kwamba utafiti huo umefanyika zaidi ya miaka miwili iliyopita.

(a) Je, ni lini mradi huo utaanza ili kuondokana na tatizo sugu la ukosefu wa umeme katika Wilaya ya Mafia?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuanza mradi huo katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 na ufanyike katika upande wa tarafa ya Kaskazini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Shah, Mbunge wa Mafia, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mehsimiwa Spika, ni kweli katika Bajeti yangu ya mwaka 2006/2007 Serikali ilitenga shiingi milioni 35 kwa ajii wa mradi wa utafiti wa upepo kisiwani Mafia.

Fedha hizo ilikuwa zitumike kufunga vifaa vya kukusanyia takwimu a upepo na kufanya upembuzi kuona iwapo kasi ya upepo ingetosheleza kuzalisha umeme kwa ajili ya mji wa Mafia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti kiasi hicho cha feha hakikikuweza kupatikana kama ilivyopangwa, hivyo utafiti huo haukufanyika kutokana na sababu nilizozitaja hapo juu. Hata hivyo, kilichofanyika ambacho Mheshimiwa Mbunge amekishuhudia ni uchunguzi wa awali kuona mwenendo wa upepo kisiwani humo.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida utafiti kuhusu upepo hufanyika kabla ya kujenga mitambo ya kuzalisha nishati, hususani ya umeme kwa madhumuni ya kujiridhisha na uwepo wa upepo wa kutosha na kasi inayokubalika kiteknolojia na kiuchumi. Kwa kuzingatia umuhimu wa utafiti huu kwa kisiwa cha Mafia, Serikali kupitia *TANESCO* imewasilisha kwa wakala wa Nishati Vijijini *REA* maombi ya fedha za utafiti wa mradi wa umeme wa upepo katika kisiwa hicho.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya umeme katika mji wa Mafia mpaka sasa ni *MW* 1.25 kwa upande wa uzalishaji umeme kituo cha kufua umeme kina mitambo miwili ya wartsila yenye uwezo wa kuzalisha *KW848* kwa pamoja ikiwa katika hali nzuri. Hivi sasa mitambo yote miwili inazalisha *kW* 800, hivyo kupelekea kuwepo na upungufu wa umeme Mafia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kama ilivyokwishaelezwa hapa Bungeni tarehe 21/4/2008 wakati wa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Serikali kupitia *TANESCO* bado ina nia ya kuzalisha umeme kwa kutumia mzunguko wa upepo *Wind mills*. Hivyo utekelezaji wa mradi umeanza na utafiti unaendelea. Aidha, kama hatua ya awali wataalamu kutoka *REA* walitembelea Mafia hivi karibuni kubaini maeneo yanayofaa kwa uwekaji wa mitambo ya kupimia upepo na pia kubaini vyanzo vingine vya Nishati, utafiti huu wa awali umefanywa maeneo ya kusimi mwa kisiwa karibu na kijiji cha Kilindoni na maeneo ya Kaskazini karibu na kijiji cha Bweni.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kuanza mradi huo katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 pindi matokeo ya upimaji tabia ya upepo yatakapobainisha maeneo muafaka katika kisiwa kwa uzalishaji umeme kwa kutumia chanzo hiki cha Nishati pamoja na kiasi cha fedha kinachohitajika kupatikana.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua adha wanayopata wananchi wa Mafia ya kutokuwa na umeme wa uhakika. Namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa mafia kuwa na subira wakati Serikali ikilishughulikia suala hili kwa karibu.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Naibu Waziri amezungumzia suala la umeme unaozalishwa kwa upepo, moja ya maeneo yanatoa upepo mwingi na unaokwenda kwa kasi ni maeneo ya Mkoa wa Singida na bajeti ya mwaka jana Wizara ilieleza juu ya azma ya kuanzisha mradi wa umeme wa upepo uendao kasi Mkoani Singida.

Je, utaratibu huo wa kupeleka mradi Mkoani Singida umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utafiti wa Nishati kwa kutumia upepo tangu mwaka 2003 na katika maeneo ambayo yamefanyiwa utafiti huo maeneo ya Kitítimo Mkoa wa Singida ni maeneo ambayo yamebainika kuwa na *potential* kubwa, kwa kawaida ili ibainike kwa kweli hapa pana uwezo mkubwa wa kuzalisha upepo, ni lazima pawe na *paterns* za upepo ambazo ni zaidi ya mita nane kwa sekunde, kwqa bahati nzuri maeneo mawili Tanzania yamebahatika kuwa na uwezo huo ambayo ni maeneo ya Kitítimo Singida na maeneo Makambako Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *East Power Pool East Africa* wameshakuja Serikalini na wameleta *proposal* zao ya kwamba wanaweza kuzalisha umeme kwa kuunganisha kwenye *grid* kwa uwezo wa *megawatts* kuanzia 30 mpaka 50.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi mazungumzo yanaendelea ikiwa ni *pamoja* na kubaini umeme huo utakapozalishwa utauzwa kwa kiasi gani kuingia kwenye *grid TANESCO* na ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mazungumzo hayo yamefikia kwenye hatua nzuri na tunaendelea kuyafanyia kazi kwa bidii kabisa kwa sababu *megawat* kuingia kwenye *grid* ni uwezo mkubwa na ni nishati ya bei nafuu kidogo.

Na. 37

**Wanafunzi Kujihusisha na Siasa na Migomo**

**MHE.USSI AMME PANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa, imeonekana kuwa katika baadhi ya Vyuo Vikuu nchini kuna wanafunzi ambao hujihusisha zaidi na mambo ya siasa badala ya masomo hatimaye kusababisha migomo:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusuiana na tatizo hilo la migomo vyuoni?

(b) Je, kwa nini Serikali haitoi tamko rasmi la kuzuia wanafunzi kujihusisha na vyama vya siasa wanapokuwa vyuoni?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Amme Pande (Mtoni) naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa baadhi ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya umma wamekuwa wanajihusisha na migomo ambayo imeathiri sana masomo na hata kusababisha vyuo kufungwa mara kwa mara.

Hii imetokana na wanafunzi kutokuwa wavumilivu wakati matatizo yao yanaposhughulikiwa na mamlaka husika na kutotaka kufuata taratibu za kuwasiliasha madai yao kwa mamlaka husika na wengine kutaka kujijengea umaarufu na sifa za kuweza kuendelea kuchaguliwa kuwa viongozi wa Serikali za wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya ya maelezo hayo naomba nijibu swali la Mheshimiwa Ussi Amme Pandu, kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali inasikitishwa sana na inalaani vitendo vya utovu wa nidhamu pamoja na migomo inayofanyika vyuoni mara kwa mara. Migomo hii si kwamba inaleta usumbufu kwa Walimu na Wanafunzi tu bali hata husababisha gharama zisizo kuwa za lazima kwa Serikali, Vyuo, Wazazi na wanafunzi wenyewe.

Kwa kuwa kila Chuo Kikuu kina hati idhini *Charter* yake, na kina sheria ndogo ndogo zinazoongoza taratibu na kanuni za nidhamu chuoni; Serikali inavitaka Vyuo Vikuu kusimamia utekelezaji wa taratibu na kanuni hizo kikamilifu na kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanafuata sheria zote za chuo kama hati idhini inavyoolekeza.

Serikali kwa kushirikiana na vyuo itaendelea kuwaelimisha wanafunzi juu ya madhara ya migomo na kuendelea kuwachukulia hatua wale wote wanaobainika kuhamasisha na kuongoza migomo vyuoni. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, sheria Na. 9 ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 ibara ya 51 hairuhusu mwanafunzi kushiriki au kuendesha shughuli za kisiasa akiwa ndani ya eneo la chuo. Hii ni pamoja na kuendesha mikutano ya siasa, kusajili wanachama na kufungua matawi ya vyama vya siasa ndani ya eneo la chuo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwakumbusha wanafunzi Vyuo Vikuu umuhimu wa kutojihusisha na shughuli za Vyama vya Siasa ndani ya Vyuo.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Spika Ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kumwuuliza swali mmoja la nyongeza kama ifuatavyo, kwa kuwa Sheria Namba 9 ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 ipo lakini kwa bahati mbaya haifuatwi, na wanafunzi wanaendelea kuwa na mambo ya Siasa na hatimaye kusababisha migomo na kuchafua ile sura nzima ya Vyuo Vikuu. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kutoa tamko rasmi wanafunzi kuachana na vitendo hivyo?

**SPIKA**: Nadhani kwenye majibu ndivyo Serikali imekwishafanya hivyo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika nakushukuru, kwa kuwa tumeshuhudia Chama cha Mapinduzi kikiwapa uanachama Wanafunzi kadi za uanachama ndani na nje ya nchi na kwa kuwa pia haki ya wanafunzi katika mambo wanayojifunza chuoni ni pamoja na somo la Siasa na kwa kuwa mgomo si kosa la jinai.Je, Waziri haoni kwamba kwa kuanzisha matawi ya chama ndani ya vyuo na kwa kuwa somo la siasa ndani ya vyuo yanawapa haki wanafunzi pale wanapoona haki haitendeki waweze kutumia migomo kama haki yao ya kudai haki zao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENSIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja lenye (a) na (b) la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, hakuna tawi lolote la chama cha siasa ambalo limefunguliwa ndani ya vyuo. Matawi yaliyokuwepo kabla ya vyama vingi baada ya kuanzisha siasa ya vyama vingi matawi yote yalihamishwa kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tawi lake limehamishiwa Ubungo. Kwa hiyo, shughuli zote za vyama vya siasa yanafanyika nje ya Vyuo husika. (*Makofi*)

(b) Suala la migomo siyo suluhu ya kutatua matatizo, ni kweli ni haki kugoma lakini inapobidi ni vizuri kutumia njia za mazungumzo na wanachuo wote wana fursa hizi kuanzia katika Serikali zao, kwenda katika ushauri wa wanafunzi na kuja Wizarani. Kwa hiyo, migomo siyo suluhu katika kutatua matatizo na nafikiri ndugu zangu tukubaliane hivyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali sasa umefikia ukomo lakini tumalize hii Wizara ya Miundombinu.

Na. 38

**Mradi wa Barabara ya Kagoma – Lusahunga Kupitia Muleba**

**MHE. WILSON M. MASILINGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ziara yake Wilayani Muleba aliagiza usimamizi na utekelezaji mzuri wa mradi wa barabara ya lami kutoka Kagoma hadi Lusahunga kupitia Muleba Mjini:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika kumpata mkandarasi mpya ili ujenzi uendelee?

(b) Je, Serikali imepata hasara ya fedha kiasi gani kutokana na kusimamishwa kwa ujenzi wa barabara hiyo ya lami kuanzia Kagoma Muleba - Biharamulo hadi Lusahunga?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Barabara ya Kagoma – Muleba – Lusahunga kwa kiwango cha lami unagharimiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Serikali ya Tanzania. Mchakato unaendelea wa kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii baada ya mkadarasi wa awali kusitishwa. Wakala wa Barabara (*TANROADS*), wameshakamilisha tathmini ya zabuni za kazi hiyo *(evaluation of tenders).* Hivi sasa Wakala wa Barabara unaendelea kufanya mawasiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) ili kupata kibali *(No Objection)* ambacho ni lazima kitolewe na Benki hiyo kabla ya kusaini mkataba na mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, labda niongezee tu kwamba, kwa taarifa tuliyoipata asubuhi hii; *no objection* ilipatikana jana jioni na kwa hiyo, mkataba huu utasainiwa wakati wowote kuanzia sasa. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haikupata hasara yoyote ya fedha kutokana na kusimamishwa kwa ujenzi wa barabara hiyo kwa kuwa mkandarasi aliyesitishwa anawajibika kimkataba kulipia gharama za ziada za kumaliza kazi za ujenzi wa barabara hiyo. Aidha, Serikali imeshikilia dhamana *(Performance Bond and Advance Payment Guarantee),* alizoweka mkandarasi pamoja na mitambo na vifaa vyote vya kazi vilivopo katika eneo la kazi.

Hata hivyo, gharama inayotokana na kuchelewa kumaliza kwa muda uliopangwa isingeweza kuepukika, kwa sababu mkandarasi aliyeondolewa asingeweza kumaliza kazi ndani ya muda huo.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii ilitarajiwa iwe imemalizika lakini matatizo yakajitokeza; je, Serikali haioni busara barabara ikakatwa vipande vipande ili wapewe wakandarasi wengi iweze kujengwa na kwisha upesi wananchi waweze kufaidi jasho lao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ina urefu wa kilomita 292 na ilikatwa vipande vitatu. Vipande viwili vya kwanza

vilishakamilika, yaani kile cha kutoka Mhuto mpaka pale Kagoma. Kwa hiyo, hiki kipande cha tatu ndiyo cha mwisho, ambacho mkandarasi alishaanza kazi na baada ya kusuasua akasimamishwa, hivi sasa huyu aliyepatikana ndiyo atamalizia kipande cha tatu. Kimsingi, baada ya kuona mradi huu ulikuwa mrefu, ulishafanyiwa utaratibu wa kukatwa vipande kama anavyopendekeza Mheshimiwa Mbunge.

Na. 39

**Utengaji wa Fedha kwa Ajili ya Ujenzi wa Barabara**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa utengenezaji wa barabara ni muhimu kwa maendeleo ya taifa letu:-

(a) Je, katika bajeti ya mwaka 2007/2008 hadi kufikia 31 Julai, 2008 ni kiasi gani cha fedha za maendeleo kilichotolewa kwa Wizara ya Miundombinu na kiasi kilichobaki kwa michango ya ndani na wahisani?

(b) Je, katika Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2008/2009 hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2008 ni kiasi gani kimepokelewa katika Wizara hiyo?

(c) Je, Serikali imepata fedha kiasi gani kwa ujenzi wa kazi za maendeleo ya barabara kutoka kwa wahisani wa nje na kwa barabara zipi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b), (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara ya Miundombinu ilipanga kutumia fedha za maendeleo jumla ya shilingi 459,513,874,080; kati ya fedha hizo shilingi 225,291,000,000 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi 234,222,874,080 zilitarajiwa kutoka kwa wahisani. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2007/2008, jumla ya shilingi 257,040,802,971.1 zilikuwa zimekwishapatikana; ambazo ni sawa na asilimia 56 ya lengo. Kiasi chote kilichobaki cha shilingi 210,586,777,438 ni fedha kutoka kwa wahisani na kwa hiyo kufikia tarehe hiyo fedha zote za ndani ziilkwishatolewa.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2008/2009, Wizara ya Miundombinu ilipanga kutumia shilingi 531,996,280,000; kati ya fedha hizo shilingi 335,286,660,000 zikiwa ni fedha za ndani na shilingi 196,709,620,000 zilitarajiwa kutoka kwa wahisani. Hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2008 jumla ya shilingi 55,048,400,000 kutoka Bajeti ya Maendeleo zilipokelewa; ambayo ni sawa na asilimia 10.3 ya lengo. Aidha, hadi mwezi Machi, 2009 Wizara imeshapokea jumla ya shilingi 283,380,248,003 za maendeleo, ambayo ni sawa na asilimia 53.3; kati ya fedha hizo, shilingi 189,593,780,000 ni fedha za ndani na shilingi 93,786,468,003 ni fedha za wahisani.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 hadi mwezi Machi, 2009, Serikali imepata jumla ya shilingi 92,141,808,003 kutoka kwa wahisani wa nje kwa ajili ya kazi za maendeleo ya barabara. Barabara zilizopata fedha hizo ni Singida – Shelui, Uvinza – Ilunde – Malagarasi, Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga, Barabara ya Nelson Mandela, Nyanguge – Musoma, Arusha – Namanga, Dar es Salaam – Mbagala, Msimba – Ruaha – Mbuyuni – Ikokoto – Mafinga, Singida – Babati – Minjingu, Chalinze – Segera – Tanga na Masasi – Mangaka.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kupanga kiasi kikubwa cha fedha katika bajeti kwenye sekta hii ya miundombinu kutoka mapato ya ndani badala ya kutegemea fedha za wahisani.

(a) Katika mwaka wa 2007/2008, Wahisani hawakutoa zaidi ya shilingi bilioni 210 walizoahidi, lakini katika mwaka huu wa 2008/2009 wamekwishatoa zaidi ya shilingi bilioni 93. Je, ni sababu zipi zilizopelekea wahisani kujitoa ghafla katika kuchangia katika kipindi cha mwaka uliopita?

(b) Katika mpango wa ujenzi wa barabara upo mradi unaoitwa PMMPR ambao upo kwenye zaidi ya mikoa mitatu. Bahati mbaya Mkoa wa Tanga ambao upo kwenye mpango, haukupata fedha kabisa katika kipindi kilichopita. Je, Wizara inasema nini kuhusu Mradi huo hasa kwa Mkoa wa Tanga na hususan Barabara ya Muheza kwenda Amani ambayo imeathirika sana kutokana na kukosekana kwa fedha hizo? *(Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuzipongeza jitihada za Serikali za kupanga bajeti ambayo inapelekea kwenye utegemezi zaidi, badala ya kutegemea wahisani, suala ambalo kusema kweli ndio lengo letu na tuhakikishe kwamba tunafika mahali bajeti yetu iwe inajielekeza kutegemea kwetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, hivyo sababu ambayo inaonekana waziwazi kwamba tusipokuwa na bajeti ambayo inajitegemea, wahisani watakaposhindwa kutimiza ahadi zao, miradi yetu mingi itakwama. Sasa ni sababu zipi zilizosababisha wahisani hawa wasiweze kutekeleza wajibu wao? Sababu hizo zinaweza zikawa zipo kwenye maeneo mbalimbali; mfano, uwezo wa wafadhili, mimi binafsi nisingeweza kuwaeleza kwa sababu wafadhili hawa wapo maeneo mengi. Kwa hiyo, pengine niseme tu kwamba, kwa hivi sasa maadam wanaendelea kutoa ahadi zao kama ilivyokusudiwa, tuendelee tu kuwaomba kwamba watimize wajibu wao kama ambavyo walitarajia kufanya.

Kuhusu Mradi huu wa EMMRP ambao ulikuwa unatekelezwa katika Mikoa mitatu na Tanga ikiwemo, tutaendelea kufuatilia tuone kwa nini fedha hizi za Mkoa wa Tanga kwenda Muheza hazikuweza kufika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, sasa matangazo. Naanza na wageni. Wageni wa Mheshimiwa Raphael Mwalyosi ni wawili ambao ni Madiwani; kuna Mheshimiwa Medelina Mlelwa, Diwani wa Viti Maalum Madope, naomba asimame, yule pale karibu. Mheshimiwa Godfrey Mhagama, Diwani wa Kata ya Madope kule Iringa. Karibuni sana. *(Makofi*)

Wapo viongozi wanane wa Wizara ya Mambo ya Ndani ambao ni Kamishna Mkuu wa Magereza, Ndugu Augustino Nanyalo; yule pale karibu sana Kamishna Mkuu. Halafu mwingine ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Ndugu Matwani Kapamba, yule pale ahsante sana. Kaimu Kamishna Mkuu wa Uhamiaji, Ndugu Kathibeth Sambaligula, yule pale. Yupo pia Kamishna kutoka Idara ya Magereza, Elias Mkuku, yule pale. Kamishna wa Zimamoto na Uokoaji, Bwana Zebu Shija, yule pale. Kaimu Kamishna wa Uhamiaji, Ndugu Nombo, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Bibi Agnela Nyoni, yule pale, ahsante sana. Mkurugenzi wa Idara ya Wakimbizi, Bi. Judith Mtawali yule pale. Ndugu O. E. Malisa, Mkurugenzi wa Adhabu Mbadala. Nadhani tunahitaji semina juu ya mambo haya ya vyeo Serikalini ambavyo hatujavielewa vizuri; Mkurugenzi wa Adhabu Mbadala. *(Kicheko*)

Pia yupo Ndugu George Muhale, Mhasibu Mkuu wa Wizara wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Bwana Dickson Maimu, Mratibu wa Mradi wa Vitambulisho. Natumaini mnaharakisha ule mchakato, maana tunasikia vitambulisho mwaka hadi mwaka wala hatuvioni. Vilevile yupo Bwana Augustino Shiyo, Mkurugenzi wa Malalamiko. Ahsante sana. (*Makofi*)

Pia kuna Bwana F. W. P. Mushi, Kaimu Mkurugenzi wa Sheria na Usajili wa AZAKI *NGOs*. Ahsante sana. Karibuni sana ndugu zetu Watumishi Waandamizi wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Tunashukuru mnakuja kuona shughuli za Bunge mkiwa hapa Dodoma.

Wapo waandishi wa habari wawili kutoka Taasisi ya Intercom, ambao ni Bwana Simon na Clementine. Haya majina naona ni ya watu wa nje. Wametoka nje wanaendelea na shughuli nyingine.

Nafurahi kuwaona kwenye *Gallery* wanafunzi 40 kutoka Al-haramain Islamic College Dar es Salaam. Naomba msimame pamoja na walimu. Karibuni sana, tunafurahi sana kizazi kipya kinapokuja hapa Bungeni, kwa sababu tunaendeleza utamaduni wa nchi yetu wa kufahamu vizuri mambo ya uongozi ya ndani. Karibuni sana, tunawatakia mema katika masomo yenu. (*Makoti*)

Sasa matangazo ya kazi; Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati ya Miundombinu kwamba, leo kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo saa 5.00 asubuhi, Ukumbi wa Pius Msekwa, eneo la *Speaker's Lounge*. Hawakuniomba idhini lakini nawasamehe. *Speaker's Lounge* huingii tu unafurahia siku moja unakwenda tu

basi, lazima Spika awe na taarifa kwa sababu na mimi ninaweza kuwa na wageni halafu tukagongana pale, lakini kwa leo sina lolote pale basi labda mliotea. Kwa hiyo, endeleeni.

Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ameniomba nitangaze kwamba, kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi Namba 231, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala.

leo Mheshimiwa Dkt. Willibrod Peter Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ameniomba nitangaze kwamba, saa 5.00 asubuhi Kamati ya *LAAC* watakutana na Ujumbe kutoka Bunge la Namibia.

Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Naelewa sana Dkt. Willibrod Slaa na harakati zake ambazo zimesimama katika upotoshaji, lakini ndiyo hivyo. Hata hivyo, yeye bado ni Mwenyekiti Rasmi wa *LAAC* na ana haki ya kuitisha Mikutano hii. Kwa hiyo, saa 5.00 Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, watakutana katika Ukumbi Namba 219 Jengo la Utawala. *(Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mwenyekiti wa *CPA* Tawi la Tanzania, anaomba Waheshimiwa Wabunge wote, kwa sababu sisi sote ni Wajumbe wa *CPA*, tukutane saa saba mchana kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa *CPA*, Tawi la Tanzania. Kwa hiyo, saa saba mchana Mkutano Mkuu wa Tawi la *CPA* pale Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, mkutane saa 6.00 mchana katika Ukumbi Namba 227 ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Sophia Simba, kwa nafasi yake kama Mwenyekiti wa UWT, ameomba Wabunge wote Wanawake kutoka Chama cha Mapinduzi, mkutane saa 7.10 Ukumbi wa Msekwa. Sasa sijui *Speaker's Lounge* kuna Miundombinu; kwa hiyo, nadhani kama ni mkutano mfupi wataangalia kuna kumbi nyingi pale katika Jengo la Pius Msekwa ili kuweza kutimiza azma za mikono yote hiyo. Sasa pale itakuwa ni miwili. Miundombinu wapo *Speaker's lounge*, *CPA* wanaingia kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa.

Nadhani Wabunge Wanawake wa CCM, wanaweza kumwona Katibu, Ndugu John Joel, atasaidia katika upangaji ili wahudhurie mkutano huo.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea taarifa kutoka Serikalini, Mheshimiwa Rais, ameridhia kwa Hati ya Dharura Miswada miwili ya Wizara ya Maji; kwa hiyo, nitaomba kesho tukutane Kamati ya Uongozi kwa muda ambao nitautangaza ili tuweze kuzingatia ratiba kwa kuwa tutakuwa na hii Miswada miwili ambayo imekuja kwa hati ya dharura. Hayo ndiyo matangazo ya leo. Sasa nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Mbolea wa Mwaka 2008

*(The Fertilizers Bill, 2008)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana Mheshimiwa Naibu Spika, alipokuwa anasimamisha shughuli za Bunge, aliwatangazia kwamba, bado tunaendelea na kweli tunao wachangiaji watano kwa mjadala unaozungumzia Muswada wa Mbolea. Nitawataja ili waweze kujua kwamba wapo katika nafasi gani. Tutaanza na Mheshimiwa Paul Kimiti, atafuatiwa na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa John Momose Cheyo na atamalizia Mheshimiwa Susan Lyimo, ambaye simwoni humu ukumbini, lakini nadhani atasikia. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Paul Kimiti.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii niwe wa kwanza kuchangia Muswada huu ambao ni muhimu sana kwa maendeleo ya wakulima wetu.

Niungane na Wabunge wenzangu kwa kutoa salamu za rambirambi, kwa kumpoteza mwenzetu Faustine Kabuzi Rwilomba, ambaye alikuwa Mbunge wa Busanda. Nina imani kabisa, kwa nia hiyo hiyo, wananchi kutoka Jimbo la Busanda watamchagua Mbunge ambaye anafanana fanana na Marehemu Faustine Rwilomba.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba utulivu mnapotoka wengine mnatoka na kelele.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, pia nataka nitumie nafasi hii, kuwapa pole wenzetu wote waliopatwa na ajali mbalimbali katika kipindi hiki na bila kumsahau Mheshimiwa Naibu Spika, ambaye hivi majuzi alifiwa na kaka yake. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninampongeza kwa sababu mbili; hapa katikati kulikuwa na magazeti yalikuwa yakimnukuu ya kwamba, hotuba zake nyingi hasa katika kipindi hiki anachanganya sana Kiingereza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ungemwachia Mheshimiwa Waziri Mkuu, asikilize pongezi ambazo anapewa hivi sasa. Endelea Mheshimiwa Paul Kimiti.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, magazeti mengi yalimnukuu kwamba, anatumia sana Kiingereza kuchanganya na Kiswahili na mimi nilikuwa nahusika sana kuona kama leo atafanya makosa hayo. Kwa taarifa yake, nimeridhika kuanzia mwanzo hadi mwisho amesema Kiswahili fasaha vizuri sana. Hiyo inaonyesha utii, magazeti yamemsema amekubali na amejirekebisha; ni mfano mzuri wa kuigwa,

tunapoambiwa tumefanya makosa tusikaidi tujirekebishe, ndiyo dalili ya maendeleo mazuri. Hivyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ulikwisha kumpongeza sana katika kujibu. Mimi ni kiongozi wa siku nyingi katika Wizara hii ya Kilimo. Nimeanzia Kilimo mwaka 1962 kama Bwana Shamba Kijijini, nilikaa Urambo Farm 16, nikaenda Kasulu, nikaa Janda Kijijini nikatoka huko nikaenda Kahama nikakaa Isangehe na Songomera kama Bwana Shamba wa Kijiji. Nilitoka hapo baada ya kusoma nikaendelea kuwa mwalimu wa Mabwana Shamba, nikawa Mkuu wa Vyuo vya Kilimo na mwisho nikawa Waziri wa Kilimo

Mheshimiwa Spika, ndogo hiyo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Hongera sana.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, sasa kwa msingi huo, nina hakika ya kuzungumzia kuhusiana na suala hili. Mwaka 1962 kwa taarifa yenu wakati Sheria hii inaundwa kwa mara ya kwanza, baada tu ya Uhuru, Baba wa Taifa alitamka maneno mawili; kwanza, alisema ili tuendelee tunahitaji vitu vine; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Akasema lazima tuanze na vitu viwili; kwanza, rasilimali watu, halafu ya pili ni ardhi; haya mengine uongozi bora tutajua mbele ya safari.

Alisema hayo kwa sababu ili uweze kufanikiwa lazima uhakikishe kwamba si suala la wingi wa watu ni suala la watu wa aina gani, wana elimu kiasi gani na umewaandaa kiasi gani. Ndiyo maana kitu cha kwanza alichofanya Baba Taifa ni kuanzisha Chuo Kikuu. Ninakumbuka baada ya uhuru akajenga Chuo Kikuu, ingawa alitumia pale Lumumba kwa kuanzia; ni hatua ya kwanza.

Alipokuja kwenye ardhi akasema, ardhi yetu bila kutumia mbolea hatatufika mahali popote. Kwa msingi huo, akaona sheria ya kwanza kuhusiana na ardhi iwe ya mbolea, ndiyo hii ambayo tunaijadili. Mwaka 1962, mwaka mmoja baada ya kupata uhuru tukasema, mbolea sasa iwe *priority* namba *one.* Naisema hiyo kwa sababu duniani kote hakuna kitu ambacho kinasumbua kama upungufu wa chakula. Ukitaka ugomvi katika nchi hii au katika dunia hii, ugomvi namba *one* itakuwa ni njaa ambayo utapambana nayo na ambayo inaweza ikafanya hata nchi ikapinduliwa. Hii ina maana gani?

Yupo mtaalam mmoja anaitwa Thomas Masusi, wengi mnamkumbuka; alitabiri yafuatayo:-

Ninatabiri ya kwamba, watu wataongezeka sana kuliko chakula na alisema hilo makusudi mazima kwa kuwa aliona jinsi watu wanavyoongezeka, wanaongezeka maradufu; kila wakati yeye alitumia neno *geometrically* yaani ni mbili, nne, nane, kumi na sita, thelathini na mbili; ndivyo watu wanavyoongezeka. Chakula kinaongezeka *arithmetically,* yaani moja, mbili, tatu, nne, ndiyo kusema tofauti itakuwa kubwa. Watu watakuwa wengi na chakula kidogo. Midomo itakuwa ni mingi, mikono michache.

Ndiyo tafsiri yake; yaani kuna midomo ambayo inakula kila wakati, mikono haifanyi kazi na hali hiyo itafanya dunia iwe mahali pabaya.

Mheshimiwa Spika, akapendekeza mambo mengine ambayo wengi wanayafahamu wamepitia shuleni, walikuwa wanasema dawa ya kupunguza ongezeko kubwa la watu; kwanza, ni kufanya watu waonane wakati wana umri mkubwa. Mwanamume aoe akiwa na umri wa miaka 35 na mwanamke aolewe akiwa na umri wa miaka 30, siyo chini ya hapo. Akapendekeza wengine waingie Utawa, alikuwa na maana yake. Hii *trend* ya watu kuongezeka haraka, jamani tutakuja kuumia kama huna njia nyingine ya kuwahakikishia chakula utapata matatizo.

Wataalamuu wakakaa wakasema, huyu achotuambia tusikidharau, tuanze kutumia akili ya jinsi ya kuweza kujikwamua katika tatizo hilo. Wanasayansi wakaona ili tuweze kupambana na hali hiyo, tunataka tutumie sayansi na teknolojia katika uzalishaji wa chakula. Huu ukawa ndiyo mwanzo wa kutumia mbolea ya kwamba kama tutatumia utaalamuu kidogo katika mbolea, tutazalisha chakula kingi katika eneo dogo na kujibu matatizo ya huyu Thomas Marcus, mbolea zikaanza kuundwa. Zipo aina zaidi ya thelathini za mbolea.

Vilevile hakusema hilo peke yake, kwenye wanyama pia alisema tuhakikishe tunakuwa na mifugo ambayo inaweza kutoa kama ni maziwa yatoke mengi kwa kutumia utaalamuu. Ndio maana siku hizi kwa wenzetu ulaya, kwa wale ambao wamefika, ng'ombe mmoja anatoa madebe mawili ya maziwa kwa siku; asubuhi na jioni, yote ni kujibu haya ili kusiwe na matatizo. Kuku, badala ya kuku wa kienyeji ambaye ana miaka miwili ndio anaweza kuliwa; tutatumia mbinu na utaratibu mpya kuku amalize wiki sita tayari ameshafika umri wa kuliwa; ni utaalamuu, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, sasa ni nini tunafanya? Ninachoogopa, tusipoangalia matumizi ya sayansi na teknolojia yanaweza kutufikisha mahali ambapo hatutaki. Nilipokwenda Marekani kama Bwana Shamba, nilijifunza yafuatayo: Wenzetu wanasema kuna haki za msingi za mmea. Mmea hauwezi kuzungumza, lakini una haki zake za msingi na ni lazima uzingatie. Kwanza ni lazima uhakikishe mmea unapata maji, kama hakuna maji basi usiupande na kama maji ni kidogo basi tafuta mmea ambao unaweza kustahimili, usilazimishe mmea ambao hauwezekani, unaukosesha haki zake.

La pili, hakikisha mmea unaupanda kwa nafasi ili uweze kupumua. Utawakuta wakulima wanaacha shina moja lina migomba 20, unaukosesha haki yake. Lingine, hakikisha unaupa virutubisho vya mbolea ili uweze kustahimili na uishi maisha mazuri. Mmea hauzungumzi, lakini sisi tupo kwa niaba ya mimea kwa sababu utatulinda.

Lingine, wanasema kama kuna ugonjwa upe dawa, ndio maana dawa zinatumika kwa ile mimea yetu na yote hii inafanyika kwa makusudi mazima ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ni nini kinafanyika? Kwa sasa tumepata matatizo, mbolea ambayo tumekuwa tukiipata wakati mwingine kwa bahati mbaya inakuja na cheti ya kwamba inafaa, lakini huko inakotoka wakati mwingine ni kati ya mbolea ambazo

zimekaa zaidi ya miaka kumi, hii inakuwa ni kama *dumping ground*. Ndio maana nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri ya kwamba, katika Kanuni ambazo amepewa kisheria, hilo alisimamie vizuri kabisa. Tunaweza kupata mbolea mbaya ikatuharibia mazao yetu. Mbolea ukiitumia vizuri ni mkombozi wa wakulima, lakini ukiitumia vibaya ni adui mkubwa kabisa wa mkulima. Ndio maana wengine wanasema mbolea imetuharibia udongo; ni matumizi yaliyotumika.

Minjingu huwezi ukasema inaweza kutumika mahali popote, ina aina fulani ya udongo; ndio maana wataalamuu wa udongo lazima wajue Minjingu iende wapi na aina nyingine ya mbolea itumike kwenye udongo gani. Ndio maana kazi ya kujua aina mbalimbali za udongo ni lazima tuifanye kwa hali ya juu, tuijenge heshima hiyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni utaratibu wa uagizaji. Namwomba sana Waziri wa Kilimo, mwaka juzi mimi nilisema kama ukitaka bei ya mbolea iwe chini ni lazima tuagize mbolea nyingi kwa wakati mmoja. Hili tatizo la kuagiza huyu tani 3,000 huyu tani 4,000, 5,000; Mheshimiwa Waziri Mkuu, hata tukitoa ruzuku kwa serikali bado hatutajibu matarajio ya wakulima wetu. Kinachotakiwa ni kuhakikisha kwamba tuna mbolea ya kutosha na iingizwe kwa wingi.

Mwaka huo huo nilitoa maelezo mazuri kwamba, kama ningepewa uwezo wa kuagiza mbolea wakati ule, ilikuwa mbolea iingie kwa mfuko mmoja shilingi 12,000, bila hata ruzuku ya serikali, lakini kila mmoja anayeletea mbolea hapa anajipangia bei; tunamuumiza mkulima. Wakati mwingine hata kutumia ruzuku tunatumia tu bila sababu ya kutosha, lakini tungekuwa na utaratibu mzuri, tungehakikisha tuna mbolea ya kutosha kwa kusimamia sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ubora wa mbolea umeshazungumzwa na wenzangu na sitaki kurudia. Ninachoomba, tunapozalisha ziada mahali popote baada ya kuwa na mbolea, kwa mfano sisi katika Mkoa wa Rukwa, tunatumia mbolea. Tukishazalisha kwa ziada, kitu ambacho ni muhimu ni kwamba baada ya kupata ziada tunapeleka wapi? Tumekuwa na matatizo ya kwamba katika mikoa yetu ambayo ipo pembeni, watu kuja Rukwa kununua mahindi si kazi ndogo, ni karibu kilometa 1,300 kutoka Dar-es-Salaam; aje moja kwa moja na barabara yenyewe unaifahamu, eti kuja kununua tani 20 za mahindi! Bei atakayokuja kuuzia Dar-esSalaam ni kubwa. Wakati mwingine wanaokuja ni wachache, bei wanayotupa kule ni ya chini sana.

Tunaiomba Serikali iangalie, baada ya kuridhika ya kwamba imeweka tani 150,000 kama akiba ya Serikali, basi iwaruhusu wakulima wauze popote wanapotaka. Manaa yake kama tumeiweka akiba ya tani 150,000 ambayo inajulikana ndio inayotakiwa kuwa akiba ya taifa, ile *surplus* inayobaki kwa mikoa ya pembeni wapewe ruksa ya kuuza mahali popote. Hii itakuwa ndio *stimulus package* ya mkulima, ili mkulima aweze kulima zaidi. Unaweza kuweka mbolea lakini ukishapata mazao bila kujua utayapeleka wapi mazao yako, utakuwa unapoteza muda wako. Ndio maana tunaomba sana serikali iliangalie hilo ili tufanikishe katika mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ninataka niombe sana; mbolea kwa mmea ni sawa na mtoto mdogo kwa lishe. Wazungu wanapima uwezo na akili ya mtoto si kwa kupima uzito wa mtoto, kila mtoto anapokua anapimwa *size* ya kichwa. Sisi tunapima uzito, Ulaya wanapima *size of the brain*, inakua kwa kiasi gani? Lishe ya mmea ni sawa na lishe ya binadamu. Tukidharau hiyo lishe, tutapata matatizo sana kwa mimea yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na ninamtakia kila la heri. Nawaombea pamoja na msaidizi wako na timu yake, mfanye kazi nzuri ya kulisukuma Taifa letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nitoe shukrani kwa kupata fursa hii, lakini niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole nyingi kwa Wananchi wa Busanda kufuatia kifo cha Mheshimiwa Faustin Rwilomba, ambaye alikuwa mwakilishi wao. Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kalambo, nawapa pole sana na Mungu awape subira, waweze kuchagua kiongozi atakayewawakilisha kwenye chombo kikubwa hiki kinachoitwa Bunge.

Niwape pole pia Wabunge wenzetu waliofiwa na wapendwa wao; Mungu awape subira pia waweze kupata ahueni na kuweza kuendelea na maisha kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika Muswada tunaouzungumzia leo kwa siku ya pili. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Viongozi wa Wizara hii ya Kilimo, kwa kuleta Muswada huu ambao tulikuwa tunausubiria kwa muda mrefu. Madhumuni makubwa ya Muswada ni uagizaji, utengenezaji, usambazaji, uuzaji na utumiaji wa mbolea katika nchi hii.

Ukiangalia hatua zote hizi ambazo zimezungumzwa, tuna vikwazo vingi. Tunaomba Muswada huu utusaidie kuondoa vikwazo hivi katika uagizaji, utengenezaji wa mbolea, usambazaji, uuzwaji na utumiaji wa mbolea katika nchi hii. Tukiweza kuyaondoa matatizo yanayozikabili katika ngazi hizi zote, basi tutakuwa tumefanya kazi kubwa ya kuwasaidia Watanzania waweze kuipata mbolea kwa bei nafuu na kwa wakati ili waweze kuzalisha mazao mengi ambayo tunayahitaji, hasa katika mazingira ya mwaka huu, ambayo tumeona mikoa mingi imepata dhoruba ya kutopata mvua; hivyo kuna ukame ambao umekithiri.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara ya Kilimo kwa kutumia sheria hii ambayo tunaizungumza leo, upunguzwe utitiri wa vyombo vinavyoshughulikia mbolea katika nchi hii ili kupunguza gharama kwa wakulima wetu, waipate mbolea kwa bei nafuu ili waweze kuzalisha zaidi. Sheria hii imezungumzia suala la kuwa na Bodi ambayo itashughulikia mbolea katika nchi yetu ya Tanzania, lakini suala la Kamati halikuzungumzwa. Sasa hili ninachoomba labda kupata ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri, je, Bodi hiyo itasambaa na iweze kufika mpaka ngazi ya wilaya?

Kama Bodi hii itaweza kufika mpaka ngazi ya Wilaya, basi tutashukuru lakini Kamati zilizokuwepo katika Wilaya zetu zisaidie sana kusimamia suala la mbolea igawanywe vizuri na iendelee vizuri, bila hivyo kutatokea matatizo makubwa sana. Bodi

itafanya kazi vizuri katika ngazi ya Taifa; uagizaji, utengenezaji, usambazaji, lakini suala la uuzwaji wa mbolea na utumiaji wa mbolea kwa wananchi wa kawaida utakuwa na matatizo kama hakutakuwa na chombo kitakachosimamia katika ngazi hii ya Wilaya. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara izingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hiyo ili sheria hii iweze kufanya kazi vizuri, tunao ukosefu au upungufu mkubwa sana wa Maafisa Ugani wa kilimo ambao ni makini. Naomba nirudie, Maafisa Ugani ambao ni makini hatunao, kiasi ambacho wanashindwa kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima wadogowadogo au mkulima mmoja mmoja katika vijiji vetu. Kutokana na hilo, mbolea inayoletwa bila kupata elimu inayotosheleza katika kuitumia, matokeo yake yanakuwa mabaya kiasi ambacho tumemsikia Mheshimiwa Zambi akilalamikia jinsi ambavyo mbolea ya Minjingu haikuweza kuleta manufaa mazuri katika kilimo cha mwaka huu.

Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuunganisha mambo haya yaende pamoja ili mbolea hii iweze kutumika vizuri. Maafisa ugani wapewe jukumu la kueleza vizuri juu ya matumizi ya mbolea mbalimbali, hili ndilo litakalotusaidia kuweza kuondokana na matatizo ya matumizi ya mbolea katika mikoa yetu na vijiji vyetu ili tuweze kupata mavuno mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sheria hii italeta ukombozi mkubwa kwa wakulima kama tulivyozungumza; na kwa mkoa wetu wa Rukwa, tumeanzisha mpango wa MAKIRU; (Maendeleo ya Kilimo Katika Mkoa wa Rukwa). Mpango huu ni mzuri sana na umeshazungumzwa katika ngazi mbalimbali na sisi tuna uhakika kabisa mpango huu pamoja na Muswada huu, utaleta mbolea kwa wakati kwa wakulima na kuweza kutumika vizuri na wakulima tunaweza tukaleta mapinduzi ya kilimo katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa Mkoa wa Rukwa, nina uhakika kabisa tutapata mapinduzi mazuri ya kilimo kama Muswada huu utaleta mbolea kwa wakati na kuhakikisha kwamba, wakulima wanapata elimu ya kutosha kuweza kuitumia mbolea hiyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, tatizo tunalokuwanalo ni wafanyabiashara wakubwa; wafanyabiashara wakubwa wanataka walete mbolea ili wapate faida kubwa. Sasa wanapotaka kupata faida kubwa, wataleta mbolea kwa bei ya chini lakini watataka waiongeze bei ili wao waweze kumgandamiza mkulima ainunue kwa bei ya juu. Mkulima ni mtu ambaye anapata kipato kidogo, anataka apate fedha kidogo kutokana na mbolea hiyo lakini awe na uwezo wa kununua mbolea; lakini huyu akiongeza bei kubwa ndio matatizo haya ambayo tunayapata. Ndio maana tunasema, tuondoe vyombo vitakavyoongeza utitiri wa vyombo vitakavyokuwa vinashughulikia mbolea na kumpunguzia mkulima gharama ambazo atazipata katika kununua hii mbolea.

Nizungumzie sheria hii au Muswada huu pamoja na utoaji wa vocha, ambao umefanyika katika kipindi hiki cha mwaka huu wa ugawaji wa mbolea.

Mheshimiwa Spika, ugawaji wa mbolea kwa kutumia vocha umefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Wakulima wengi ambao hawakutarajia kupata mbolea kwa mwaka huu, wameweza kupata mbolea lakini haitoshi kwa sababu kumetokea matatizo. Yapo

matatizo mbalimbali ambayo yametokea na nina uhakika wenzangu waliotangulia wameyazungumza. Sheria hii iangalie ni jinsi gani mbolea itagawanywa na Serikali itasaidia vipi mpango huu wa vocha uendelezwe. Matatizo yanayotokana na ugawaji wa mbolea kwa kutumia vocha, yaangaliwe kwa makini ili tuweze kuondokana nayo. Wakulima wengi wamelalamika katika Jimbo langu la Kalambo kwamba, waepewa vocha lakini hawakupata mbolea kwasababu kuna wajanja waliokwenda kuandikisha vocha zile zikaandikishwa; mkulima akatarajia kwamba atapata mbolea lakini vocha zile zikachukuliwa kabla hajapewa mbolea. Hawa wajanja wachache wakaenda wakachukua fedha katika mabenki bila kumfikia mkulima. Hili ni tatizo ambalo safari hii limeonesha dalili.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, Wizara ya Kilimo, kwa kushirikiana na Halmashauri zetu, waangalie katika ugawaji wa vocha na ugawaji wa mbolea, mambo haya yaendane ili wale wanaoonesha ujanja wa kutaka kuchukua vocha bila kuwapatia wakulima mbolea wakamatwe washtakiwe, kwa sababu hawa ni wezi kama wezi wengine ambao wamekuwa wanaiibia Serikali. Safari hii wameiibia Serikali na wakawaibia wananchi; hivyo katika Wilaya ya Mbozi hili suala limejitokeza lakini katika Wilaya ya Sumbawanga na katika Jimbo langu, hili suala limezungumzwa na wakulima wenyewe kwa sababu watu wamedanganywa wakachukuliwa vocha na vocha hizo zikaenda zikachukua fedha benki lakini mbolea haikufikishwa. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kutumia sheria hii tuone ni jinsi gani ya kuweza kuboresha ili tusije tukapata matatizo tena yaliyojitokeza mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubora wa mbolea hili ni tatizo ambalo tunapokuwa na waingizaji wengi wa mbolea katika nchi hii, tunaweza tukashindwa kudhibiti mbolea kwa sababu hatujui wameipata kutoka sehemu gani na ilitengenezwa kutoka kipindi gani. Serikali yenyewe ndio ikisimamia uagizaji wa mbolea na kujua ilitengenezwa kipindi gani au mwaka gani, nina uhakika tunaweza tukapata mbolea ambayo ni nzuri na ikawanufaisha Watanzania. Sheria hii pia itusaidie kusimamia upatikanaji wa mbolea kwa wakati muafaka. Mbolea nyingi zinatengenezwa kutokana na mazao ya petroli. Mwaka huu tumepata mbolea ambayo ilinunuliwa kipindi kile bei ya petroli ilikuwa imepanda sana. Bei ya pipa moja ilikuwa imefikia mpaka dola 140, kipindi hicho ukinunua mbolea ambayo ni mazao yanayotokana na petroli, kwa vyovyote bei itakuwa kubwa sana na ndio maana hata pamoja na serikali kutoa vocha, lililojitokeza unaona mbolea nyingi ilikuwa na bei ya juu kwa sababu hii.

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki tunavyozungumza bei ya mafuta ya petroli imeshuka, tena imeshuka sana kiasi cha pipa linauzwa dola karibu 38 au 40. Tukinunua mbolea kwa wingi kipindi hiki ambacho bei ya petroli imeshuka, nina uhakika bei ya mbolea itashuka sana na mkulima anaweza kuipata hata kwa shilingi 12,000 au 15,000, pamoja na hiyo ruzuku ambayo inatolewa. Hivyo, naomba Serikali iwe makini, Wizara iwe makini, ihakikishe tumepata mbolea katika kipindi hiki ambacho bei ya mbolea iko chini kutokana na bei ya petroli kuwa chini. Hivyo, wakulima wataipata mbolea kwa bei ya chini na nina uhakika kabisa, mpango huu wa vocha utakuwa na manufaa mazuri zaidi kwa wakulima katika mkoa wetu wa Rukwa, Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Iringa na sehemu nyingine ambazo wanalima kwa kutegemea mvua hizi ambazo ni za uhakika.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Viongozi wote katika Wizara hii ya Kilimo, hasa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Maafisa wote wa Wizara. Wameleta Muswada huu katika kipindi muafaka na tunaomba waweze kuzingatia uipatikanaji wa mbolea na wapunguze msururu wa vyombo vinavyohusiana na upatikanaji wa mbolea ili tuhakikishe kwamba, wakulima wanaipata kwa bei ambayo ni nafuu sana. Usimamizi wa ugawaji wa vocha pia uende sambamba na matakwa ya Serikali ili wananchi wasiibiwe. Mtu akiwa na vocha ni sawasawa na fedha na mbolea ipatikane ili waweze kubadilishana na sio mtindo uliotumika na wajanja wachache, ambao wamekwenda kuchukua vocha kutoka kwa wakulima na hawakuwapelekea mbolea. Wengine nasikia tu walikuwa wanawapa shilingi 5,000 anasema chukua hizi nipe vocha. Anatoa vocha, mbolea hapati, shilingi 5,000 hazimsaidii kwa kitu chochote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii lakini naomba Wizara izingatie haya niliyoyazungumza na kusimamia ugawaji wa vocha ili wananchi wasiendelee kupunjwa au wasikose kupata mbolea wanayoihitaji. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, kwa ruhusa yako, naomba niungane na Wabunge wenzangu nami niweze kutoa rambirambi kwa niaba yangu mwenyewe na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Mpanda Kati, kwa kifo cha Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, aliyekuwa Mbunge wa Busanda; Bwana ametoa na Bwana ametwaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, pia napenda nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Wataalamuu wa Wizara ya Kilimo na Wadau wote waliohusika kuandaa na kutayarisha Muswada huu na kuuleta. Muswada huu ni muhimu sana na ni mwendelezo tu wa kutengeneza sheria ambazo tayari tunazo katika nchi yetu lakini hofu na ukweli ni kwamba, usimamizi wa sheria zilizopo ndio tatizo kubwa katika nchi yetu. Endapo hatutaweza kubadilika, tukajenga dhamira ya kweli na utashi wa kuzisimamia sheria hizi ambazo tunazitunga, basi tutaendelea kuwa na sheria ambazo haziwezi kuleta tija kwa wale ambao tunawakusudia.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naitazama sheria hii wakati nilipokuwa naupitia Muswada huu, lakini nimeridhishwa sana baada ya kuona hili jedwali la masahihisho ya marekebisho; yale ambayo nilikuwa nadhani ni muhimu yote yameingizwa. Tatizo kubwa katika suala la mbolea kama Wabunge wengi walivyochangia na kuzungumza ni bei ambapo wakulima wa kawaida wanashindwa kuimudu na mpaka ikaipelekea Serikali kutoa ruzuku ili kuwafanyia nafuu wakulima waweze kupata mbolea ili waweze kuzalisha kwa tija na kwa wingi zaidi. Kwa hiyo, nimejiridhishwa na nimefurahishwa baada ya kuingizwa kipengele ambacho kitakuwa kinatoa fursa ya kusimamia na kurekebisha bei za mbolea, kama ambavyo imeainishwa hapa. Aidha, tatizo kubwa ni elimu ya mbolea; yamekuwepo malalamiko mengi sana hasa kwa mbolea hii ya Minjingu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli baada ya kupatikana kwa mbolea hii ya Minjingu, tulidhani kwamba itakidhi matatizo na haja ya mbolea katika nchi yetu, pia tukadhani kwamba tumepata ukombozi, kwa hiyo kimbilio likawa kwenye mbolea ya Minjingu lakini bila kujali athari au kuangalia matatizo yatakayotokana na mbolea hiyo.  Mbolea ikasambazwa sehemu mbalimbali, ambapo pengine katika maeneo ilipopelekwa, haikuweza kuleta mabadiliko yoyote na badala yake imeleta malalamiko. Kwa maana hiyo, nilikuwa napenda kuishauri Wizara; ni vyema sasa zile taarifa zote ambazo wanazo pale Wizarani, zinazohusu ubora wa ardhi, kwa sababu kwa mfano, Mkoa wa Rukwa tayari ulishafanyiwa *soil test* lakini taarifa zake zimeendelea kuhifadhiwa pale Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na Wizara ya Kilimo, hazijawafikia wakulima. Kwa hiyo, bado hujamsaidia huyu mkulima ambaye unafikiri sheria hii inaweza ikamsadia bila kumpa taarifa ambazo zinaweza zikamfanya abadili kilimo chake kiwe bora zaidi na cha kisasa zaidi.  Kwa hiyo, taarifa hizi na hasa za utafiti zinazofanywa na vyuo mbalimbali kwa mazao na hata mbolea; ni lazima ziwekwe bayana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, unakuta katika sheria hii, kifungu cha 31 cha Muswada huu ambacho kinamuhusu mtumiaji wa mbolea kwamba, kila anayetumia mbolea  ni lazima awe anafahamu matumizi sahihi ya ile mbolea na namna ya kuitumia. Mkulima ni kweli anaweza kufuata masharti na maelekezo yote yaliyopo katika *package* ile ya mbolea, lakini je, kama mbolea hiyo haikutoa tija kama ilivyokuwa inatarajiwa mkulima huyu ananufaika vipi?

Kwa hiyo, lazima tuangalie ni namna gani sasa itafikia mahali na mkulima naye tumlinde. Kwa sababu zinakuja mbolea ambazo zimesha-*expire*, zimekaa kwenye mabohari kwa muda mrefu, zinasambazwa na wakulima wanazitumia, lakini hazizalishi kama ilivyokuwa inatarajiwa. Mkulima huyu anakuwa amepoteza nguvu yake na amepoteza fedha zake kununua mbolea ambayo imesha-*expire*.

Sasa anapotumia mbolea kama hii; ni nani anayemlinda Mkulima huyu ambaye ameingia hasara ya kupoteza muda wake, nguvu zake na pesa zake? Lazima pia sheria itoe kinga kwa mkulima ili atakapopata madhara yatokanayo na mbolea, basi aweze kupata fidia.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine kubwa lililopo katika nchi yetu juu ya mbolea ni suala la bei, lakini bei imechangiwa sana na hali duni ya miundombinu iliyopo nchini. Kama serikali haitawekeza katika mioundombinu ili mbolea iweze kusafirishwa kwa bei nafuu zaidi, iweze kumfikia mkulima na aweze kuimudu, bado suala la mbolea litakuwa ni tatizo kubwa katika nchi yetu, kwani watu wengi watashindwa kuitumia. Yamekuwepo maelezo mengi kuhusu mbolea za chumvichumvi na nimewahi kuona mahali kwamba mazao yanayozalishwa kutokana na mbolea hizi za chumvichumvi katika masoko ya kimataifa bei zake ni duni zaidi kuliko mazao ambayo yanazalishwa na mbolea ya asili kwa maana ya mboji.

Mheshimiwa Spika, nilipata kupata taarifa wakati fulani kwamba, mwaka 2005 Wizara ya Kilimo, ilitoa kibali kwa kampuni moja kusambaza mbolea ya mboji, kwa jina la kibiashara la *Earthfood.*  Nilikuwa napenda nijue ni kwa nini mbolea hii imeshindwa

kuingia sokoni; ilikuwa na udhaifu gani na matatizo yalikuwa ni nini; na kama Wizara ilikuwa imetoa kibali katika ufuatiliaji wake wamegundua kasoro zipi? Na kama mbolea hii ilikuwa inaweza kuwa ni mkombozi kwa mkulima maskini wa Tanzania ni kwa nini sasa Wizara isisaidie kuhakikisha inasambaa na inawafikia wakulima wengi zaidi? Yote haya yanategemea yafanyiwe utafiti wa kisayansi na wa kitaalamu ili yasije kuleta madhara kwa mkulima ambaye tumekusudia kumsaidia.

Mheshimiwa Spika, dhamira na makusudi ya kuwa na matumizi ya mbolea hizi za viwandani ni kuongeza uzalishaji. Pamoja na kuongeza uzalishaji, kama Wizara haitasimamia masoko, bado tutakuwa na matatizo; mkulima huyu atakuwa na gharama kubwa sana ya kuzalisha lakini bado hawezi kurudisha gharama zake kwa sababu bei au masoko hayapo kabisa au bei ni duni. Sasa kwa sababu Wizara inahimiza matumizi ya mbolea, basi pia Wizara iandae mikakati ya kuhakikisha kwamba, yanakuwepo masoko ya mazao yanayozalishwa kutokana na matumizi ya mbolea yalivyoongezeka.

Kama alivyosema ndugu yangu, Mheshimiwa Mwanzila kwamba, inapofikia tunapokuwa na ziada basi pia tuangalie masoko yanayotuzunguka, hasa kwa Mkoa wa Rukwa kuendelea kuwabana wakulima wake wasiweze kuuza mazao yao nje ya nchi ni tatizo kubwa sana. Nimewahi kuambiwa kwamba ni afadhali ukaagiza mahindi kutoka Mexico yatakufikia Dar es Salaam kwa urahisi zaidi, kuliko kuyaagiza kutoka Sumbawanga; tatizo ni miundombinu; hivyo, gharama za usafirishaji zinakuwa kubwa sana. Kwa hiyo, mfanyabiashara makini hana sababu ya kuja kununua mahindi Sumbawanga, atatafuta soko lingine ambalo ni rahisi zaidi. Sasa sisi tunayo masoko katika nchi zinazotuzunguka lakini tunabanwa na mahindi yanaendelea kuoza kwa wakulima. Sasa ni vizuri Wizara iangalie ni namna inaweza kuwasaidia hususan wakulima wa Mkoa wa Rukwa kutokana na uzalishaji wa ziada wa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ambalo nilikuwa nataka kupata maelezo ya ziada, nadhani suala la kutoa ruzuku na huu mpango wa vocha lilikuwa ni mpango kwa ajili ya kumsaidia mkulima. Nilikuwa nataka kufahamu kama mpango huu ni wa muda mrefu au ni wa muda mfupi; kama ni wa muda mrefu uhakikishwe kwamba unaandaliwa katika utaratibu ambao hauwezi kuzalisha malalamiko kama ilivyo hivi sasa. Vilevile ili tuweze kufanikiwa ni lazima Serikali sasa itumie uwezo wake wote wa kushawishi ilionao ili kuhakikisha kwamba, sasa tunaweza kutengeneza mbolea hapa hapa nchini; hii itapunguza gharama maradufu. Suala hili la kuwa na kiwanda cha mbolea, Serikali ya Awamu ya Kwanza iliona umuhimu wake, wakatengeneza kiwanda cha kuzalisha mbolea pale Tanga, lakini kwa sababu ambazo sijui kama zilikuwa haziwezi kuzuilika; kile kiwanda kimekufa.

Umuhimu wa kuwepo kiwanda kile wakati ule mpaka sasa bado upo; sasa nilikuwa naishauri tena serikali kwamba, ihakikishe kwa mfano sasa tunayo gesi asilia kule Mtwara, juhudi za makusudi za kushawishi makampuni makubwa yaweze kuanzisha kiwanda cha kutengeza mbolea hapa nchini, zinaweza kuwa ni suluhisho na ukombozi kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kibinadamu, kwa niaba ya Wapiga Kura wa Bariadi Mashariki, natoa rambirambi kwa kifo cha ndugu yetu Rwilomba, ambaye tuliupokea mwili wake na nilienda kwenye ibada yake; Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Aidha, nataka kutumia nafasi hii kutoa rambirambi zangu kwa Wakili aliyeweka haki mbele kuliko fedha, naye ni Moses Maila, ambaye amefariki Texas Marekani. Roho yake iwekwe mahali pema peponi na pia Mungu awape faraja wafiwa. Amen.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mzuri na mbolea ni lazima iwekwe. Kitu ambacho nataka kukizungumzia kwanza ni kwamba, yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza, hasa juu ya ubora wa mbolea ya Minjingu, jambo hili lisifanywe la kisiasa, kwamba kwa sababu ni yetu, kwa hiyo, mambo yanayohusu ubora au *technical aspects* za mbolea hii yasizingatiwe. Ninashauri kwamba, suala hili litiliwe maanani ili hii mbolea iweze kuangaliwa sehemu mbalimbali za nchi ili kuhakikisha udongo wake kama alivyosema mwalimu wa kilimo, ufanane na vitu ambavyo viko katika mbolea ya Minjingu. Kama tutaenda kichwa kichwa tu kwa sababu ni ya Minjingu, *therefore,* lazima iende mahali popote pale; tutaharibu mazao ya wananchi na zaidi ardhi.

Jambo la pili, ukishaanza kutumia ni sawa sawa na mtu anayetumia dawa za kulevya; ni lazima uendelee la sivyo huwezi kupata mazao ya aina yoyote. Ushahidi huu umetolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi, ambao kwao wametumia mbolea kwa muda mrefu. Nalifahamu hili kwa sababu nilikuwa mwanafunzi wa kilimo. Zamani Isimani iliweza kupata mahindi lukuki bila kutumia mbolea, lakini leo bila mbolea hupati mahindi. Ndiyo maana natoa tahadhari, tuuzingatie ukweli kwamba, Serikali haina fedha za kutosha kuagiza mbolea ya kutosha nchi nzima. Hata ile tuliyokuwa tunasema kwamba tumepata gesi kule Mtwara, lakini kwa hali halisi ya kuyumba kwa uchumi duniani, kuna taarifa kwamba hata mipango ya kutengeneza mbolea kule ARTUMAS ni hati hati.

Kwa hiyo, uwezo wa kuweza kumpa kila mkulima mbolea ni ndogo sana kwa Serikali. Kwa hiyo, kama tunajua hilo, basi tusieneze hii dini ya mbolea kila mahali au tukapeleka mbolea kidogo kidogo ambayo hatuna uwezo wa kuweza kuiendeleza. Zaidi sehemu kama ya kwetu kule Sukuma Land, kama hakuna mbolea ya kutosha achaneni na haya mambo ya mbolea, acha tuendelee kutokupata mahindi na pamba. Kwa utaalamuu tulioonao sasa; pale ninapoishi mwaka huu tutapata mahindi kibao kwa sababu mvua zimekubali, lakini kama tungekuwa tumezoea kuweka mbolea na zaidi hii ya chumvi chumvi, nina hakika mwaka huu kwa ufinyu wa bajeti tungelikuwa tunalia. Kwa hiyo ni tahadhari ambayo nilikuwa nataka kuiweka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunahitaji mbolea, basi tuangalie ndani na kuweza kupata mbolea ambayo sasa hivi inashabikiwa na wale ambao wanawaagiza kama vile chakula ambacho hataki kitumie *chemical*. Tuhimize zaidi matumizi ya samadi na mboji, ndiyo inaweza kutuhakikishia kwamba wakulima wetu wataweza kupata chakula kingi

zaidi na mazao. Kitu cha kusikitisha ni kwamba, tunao ng'ombe milioni 18 na inavyoonekana sasa hivi ni vita kati ya Serikali na ng'ombe. Nasikia hii vita inaendelea na leo kusema kweli lazima nikubali, wale waliomsikiliza Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema, hawezi kusitisha zoezi ambalo limefanyika vibaya Kilosa, ambapo jana tu tulikuwa tunaangalia mtu alikuwa na ng'ombe 180 leo amebakiza ndama watatu ambao tumeangalia picha tumemwona mtu analia; ana wake kumi na watoto ishirini hana njia ya kuwapeleka shule, leo yote hii haiwezi ikapeleka mionzi ya kugusa mioyo ya Serikali kwamba zoezi hili kwa sasa hivi lisitishwe?

Kusema kweli imenisikitisha sana, nakubaliana na utaratibu aliosema kwamba, atafanya utafiti sehemu mbalimbali na ataweka baraza ambalo litatuunganisha na sisi Wabunge tuzungumzie juu jambo hili.

Nilifikiri kabla haya majibu hayajatokea, jambo hili sasa lingesimamishwa ili watu wa Ulanga na Mahenge wasiishi kwa wasiwasi. Tuna uhakika na tuna majina ya watu ambao pia wamekaa Mpanda tangu 1974 na wao wanafukuzwa; sijui Mheshimiwa Spika kwako hali iko namna gani, lakini najua kwa jirani yako tunapata barua za kila aina za jinsi wafugaji wanavyonyanyaswa? Hawa ndiyo ambao wangeweza kutusaidia kupata mbolea ambayo itatusaidia kuwa na mazao yanayouzika ulimwenguni kote, kwa sababu yako *basic on organic matter* ndiyo tunavyotaka.

Kwa hiyo, ombi langu Serikali hili jambo ingeliangalia ili tuhakikishe kwamba, hao wanyama wanatusaidia kupata samadi ambayo tunahitaji, badala ya kutegemea kemikali kwa ajili ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, kama kweli tunasukuma matumizi ya mbolea, maana yake ni kuongeza gharama kwa mkulima. Sasa kama unaongeza gharama ya mkulima, basi umtengenezee mazingira ambayo anaweza kumudu gharama hizo. Mimi natoka katika eneo la pamba, gharama ya mkulima wa pamba ni karibu shilingi mia tatu kwa sasa hivi bila mbolea kwa kilo moja. Juzi Mheshimiwa Waziri anayehusika na kilimo alipokuwa anapita Bariadi, nasikia alizungumzia juu ya minong'ono ambayo imewatisha sana wakulima. Kwamba, pamba ya mwaka huu kwa sababu bei imeteremka kiulimwengu, huenda ikawa shilingi 200 kwa kilo; shilingi 200 kwa kilo kwetu tunaita bodo mbili. Bodo mbili au shilingi 200 haziwezi kununua hata gazeti alasiri.

Sasa huyu mtu ambaye unamuandaa sasa hivi auze kwa bodo mbili ambayo hawezi kununua hata alasiri, ataweza kuwa na uwezo wa kununua mbolea; iwe mbolea ya samadi au iwe ya kemikali. Nina hakika Serikali ina uwezo kabisa wa kuweza kumsaidia mkulima wa pamba; kwanza, mkulima wa pamba kwa muda mrefu mno amepunjwa. Kwa mtazamo wa namna ya kukokotoa bei ya pamba, mkulima amepunjwa kwa muda mrefu sana. Mkulima wa pamba anafaa kuonwa kama mkulima wa mbegu ya mafuta na mafuta ya pamba yanaliwa hapa hapa nchini. Mafuta na mbegu ya pamba inatoka keki ambayo inalisha ng'ombe wetu hapa mjini. Pamba pia inatoa sabuni ambayo wanunuzi wako hapa mjini, kwa hiyo, ndiyo kusema kwa miaka mingi tutegemee theluthi moja ambayo ndiyo nyuzi, itumike kukokotoa bei ya pamba; tumewapunja wakulima kwa muda mrefu sana.

Mimi nina uhakika, Waziri anayejua pamba akiamua kuwasaidia hawa wakulima wa pamba wasipate bodo mbili badala yake wapate angalau shilingi mia tano, uwezo huo wanao. Kwanza, bei ya mbegu ambayo inaenda kutengeneza mafuta isiwe chini ya shilingi 400. La pili, bei ya pamba iliyoshuka kwa ajili ya nyuzi basi iweze kuongezea shilingi mia moja; uwezo wa kupata shilingi mia tano upo kabisa.

Tumeelezwa tulipokuwa tunaenda katika mikutano mbalimbali kama ile ya IMF juzi na mambo kama hayo kwamba, kuna *shop funds*, yaani kuna fedha zitakazosaidia nchi kama zetu kutikisika na mfumo wa uchumi kiulimwengu. Fedha hizo zitumike, tunafahamu kwamba, katika nchi kwa muda mrefu tumekuwa na Stanbic’s Fund, yaani fedha ambayo inasaidia mmomonyoko wa bei; kwa nini hizi fedha zinatumika tu kwa zao moja ambalo labda ni kahawa?

Hizi fedha zinaweza pia zikatumika kwa kujua kwamba, bei ya mkulima mwaka huu inabakia shilingi mia tano kwa kilo. Namwomba Waziri alishughulikie jambo hili. Zaidi ya yote, juzi amepita Mheshimiwa Waziri, badala ya kuwaambia watumie mbolea anawaambia wakulima wote; kwa mfano, Bariadi itabidi wauze kwa mnunuzi mmoja, mnunuzi mwenyewe ni ushirika aliyefilisika. Sasa huku bei zinateremka, halafu unaleta tena ajenda nyingine; hivi ajenda ya Wizara hii kwa upande wa pamba ni kitu gani? Upande wa ng’ombe tunafilisika na upande wa pamba tunafilisika; ajenda yenu ni nini?

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata majibu kupitia mazungumzo haya leo ili wakulima wa pamba wasianze kukata pamba yao na wasiache kupalilia. Ukisema bei itakuwa bodo mbili, mimi nina uhakika wakulima watakata pamba yao. Ukisema ni lazima watu wakakope kwenye maghala, stakabadhi ghalani, wakulima watatengeneza magodoro badala ya kupeleka hii pamba kwenye maghala hayo.

Zao la pamba liangaliwe, usipopata majibu hata Benki ya CRDB nayo itafilisika. Kwa hiyo, nalizungumzia hili ili watu wafikishwe mahali ambapo wanaweza kutumia mbolea. Lazima tuwatengenezee mazingira ambayo wanaweza kuwa na uwezo wa kununua mbolea ili kuboresha mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumzia hili.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye Muswada huu muhimu sana kwa maendeleo ya kilimo ya katika nchi yetu na hasa ukizingatia madhumuni yake. Kabla sijachangia, naomba niungane na Wabunge kutoa pole kwa msiba mkubwa uliotupata; na hasa nikupe pole wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Rwilomba. Ninaomba Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema peponi roho yake. Ninawaombea ndugu wa Marehemu, hususan mkewe na watoto, Mungu awape nguvu na faraja katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nichangie hoja iliyo mbele yetu. Ni wazi kwamba, nchi yetu inahitaji sana mabadiliko hasa ya kilimo. Nazungumzia hili hasa tukizingatia matatizo makubwa yaliyotikisa uchumi wa dunia hii na ndiyo sababu watu wengi sasa hivi wanasema njia pekee ya kujikwamua na tatizo hili la mtikisiko wa dunia, hasa kwa nchi maskani na zinazoendela kama Tanzania ni kuwekeza katika kilimo. Kwa kuwa udongo wa Tanzania umechoka na kwa maana hiyo, kama wenzangu walivyosema, unahitaji mbolea.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba, Muswada huu umechelewa kwa sababu ukiangalia toka mwaka 1962 ambapo kulikuwa na Sheria ya Mbolea, kumekuwa na mabadiliko mengi sana, hasa ukizingatia wakati ule bado udongo ulikuwa na rutuba, lakini muasisi wa taifa hili, Mwalimu Nyerere, aliona umuhimu wa kuwa na mbolea.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ambalo naliona katika Muswada huu ni suala zima la maafisa ugani au wale wataalamuu wa kilimo. Pamoja na kwamba, tuna chuo kimoja cha kilimo hapa nchini, tulikuwa tumeomba sana, wanafunzi walioko pale wanaochukua shahada za kilimo ni wachache lakini tulikuwa tunaomba pia wapatiwe asilimia 100 kama ilivyo kwa madaktari ili tuweze kuwa na wataalamuu wengi, waweze kwenda kuwasaidia wakulima wetu kule vijijini. Ni wazi kwamba, mbolea hasa ile ya *chemicals,* yaani *inorganic fertilizers* au ya chumvi chumvi, inahitaji sana utaalamuu wa hali ya juu hasa tukizingatia madhara iliyonayo. Kwa mfano; ni wazi kwamba, mkulima kama hana utalaamu akaweka mbolea zaidi ya kipimo; ni wazi kwamba mazao yale yataungua na hili pia limekuwa linajitokeza. Kibaya zaidi kama itatokea mvua kubwa ni kwamba, ile mbolea chembechembe zake zitakwenda moja kwa moja kwenye mizizi na madhara yake ni kwamba, mimea ile inaweza ikaungua au ikadumaa. Vile vile tunaona ina athari kubwa katika udongo au mazingira.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, hizi mbolea za chumvi chumvi mara nyingi zinafanya udongo uwe na *chemicals* nyingi na *water table* inapanda. Hii ndiyo sababu nchi nyingine kama Austria wamepiga marufuku, kutokana na athari zake kimazingira. Hivyo basi, kwa kuwa Mungu ametujalia Tanzania tuna mifugo mingi lakini vilevile tuna majani ambayo yangeweza kutuletea mbolea ambayo wanaiita *organic* au zisizokuwa na *chemicals*.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, kwanza, mbolea hii ambayo ni *organic* haihitaji hata utalaamu wa hali ya juu. Nakumbuka siku za nyuma, mimi nikiwa mdogo, tumekuwa tukitumia mbolea za mboji na samadi kule Kilimanjaro, ambayo inasaidia sana kurutubisha udongo tofauti na mbolea nyingine hizi za chumvichumvi ambazo naona ni aghali. Vile vile tunajua kwamba, wakulima wetu hawana uwezo mkubwa wa kuweza kupata mbolea hizi.

Kibaya zaidi, mbolea hizi hazifiki kwa wakati. Pamoja na kutokufika kwa wakati, unakuta zinaingia kwa uchache sana, kiasi kwamba ukija kwenye ile *principle* ya *demand and supply* tunapata matatizo. Kwa hiyo, matokeo yake, wale wafanyabiashara wanaoleta mbolea hizi wanaamua kujipangia bei, kwa sababu mbolea ile ni kidogo. Kwa hiyo, tulikuwa tunategemea kwamba, kwa kuwa madhumuni haya ni pamoja na

usambazaji na uuzaji, lakini vile vile kuwe na uhakika wa *accessibility;* ni muda gani wakulima wanapata mbolea hii. Tunajua kwamba mvua za kwanza ni kupandia, lakini vile vile uwe na mbolea. Haina maana kuleta mbolea wakati tayari mazao yameshafikia kimo ambacho hakistahili mbolea. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni jukumu la Muswada huu kuhakikisha kwamba, Mheshimiwa Waziri unapanga taratibu au *guidelines* ambazo zitasaidia sana kuhakikisha mbolea zinafika kwa wakati na kwa wingi ili wananchi waweze kuchagua.

Mheshimiwa Spika, ukiuangalia huu Muswada wenyewe, nimejaribu kuupitia lakini sijaona popote panapoelezea *quality* ya *assurance* ya mbolea; inaelezea tu *licence registration.* Ni nani anahakiki ubora wa mbolea katika Muswada huu?

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba, kuna Mkemia Mkuu wa Serikali, tuna *Bureau of Standards,* vilevile tuna *TFDA*, lakini bado wakulima wanalalamika. Malalamiko yao makubwa ni suala zima la mbolea hasa hii ya Minjingu. Wenzagu wameliongelea, sitaki kuliongelea kwa kina, lakini nilikuwa naomba kujua katika huu Muswada mzima, suala *quality* liko wapi; na nani ana-*control quality* ya mbolea? Itakuwa haina maana, mkulima anatoa fedha zake ananunua mbolea kwa gharama kubwa, lakini matokeo yake anapofikisha shambani mazao yale yanaungua. Sasa hivi ukipita maeneo mengi utakuta mtu ameweka mbolea lakini mahindi bado ni ya njano, lakini siku za nyuma tulikuwa tunaona kabisa jinsi gani mahindi yanakuwa bora na watu wengine walifikia hata kupata zaidi ya magunia 40 katika eka moja. Sasa hivi mtu anaweza akapata magunia mawili au asipate. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ubora ni muhimu sana kuliko jambo lingine lolote. Tuwaonee huruma wakulima wetu, wanateseka sana kupata mbegu lakini vilevile katika suala la mbolea haitakuwa na maana kabisa tuwe na mbolea ambayo haina tija.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu; kama ambavyo ilivyo kwa binadamu, tunahita virutubisho ili kuwa na afya bora kupambana na maradhi; tunahitaji *carbohydrate;* tunahitaji protein na kadhalika. Vilevile na mimea kuwa na afya bora inahitaji *nutrient* kama *potassium, nitrogen* na *phosphate*. Kwa hiyo, tuangalie ni jinsi gani na sisi wakulima tunaweza kuwa na tija kama ambavyo nimesema awali, tutakuwa taifa la ajabu kama kila leo tutakuwa tunaomba misaada na hakuna kitu kibaya katika taifa ambacho kinaleta *insecurity* kama kutokuwa na chakula.

Labda niseme tu wakati tulipokuwa kwenye mkutano wa IPU kule Adis Ababa, pamoja na kwamba kulikuwa na ajenda nyingi, lakini watu wote na nchi zilizoendelea kama Canada na nchi za Ulaya, waliona hoja ya msingi ya kujadiliwa katika mkutano ule ni suala zima la mtikisiko wa dunia na athari zake; hasa ikizingatiwa kwamba, nchi zinazoendelea zinategemea zaidi kilimo na wakasema kwamba, sasa hivi tuelekeze nguvu zetu zote katika kilimo.

Sote tunajua kwamba, kilimo chetu bado ni duni, lakini vilevile mbolea isipokuwepo, kuna uwezekano wa sisi kutokupata chakula unakuwa mkubwa zaidi. Niseme tu tuna ardhi yenye rutuba, lakini bado hatujaweza kuwekeza kisawasawa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Muswada huu uende sambamba na kuhakikisha kwamba, kilimo

sasa kinakuwa na tija na tunakuwa na mageuzi ya kilimo au *Green Revolution* na nchi yetu iache kuwa omba omba. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani tuna uwezo huo, Mheshimiwa Waziri ufanyie kazi Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye Muswada wenyewe, kwenye *functions* za hii *committee* iliyoundwa, ukurasa wa tisa, ukiangalia zile *functions* zinaelekeza kabisa katika masuala mazima ya mbolea. Ukiangalia wale wajumbe ndiyo hapo nilikuwa napata tatizo kidogo, wote wanahusika na masuala hayo hayo ya mbolea, lakini huyu anayetoka Wizarani anahusika na masuala ya *finance.* Sasa nilikuwa nataka kujua jukumu la huyu mtu anayehusika na masuala ya fedha katika *committee* hii ambayo inahusika na masuala ya mbolea. Vilevile nilikuwa nataka kujua katika *fine* kama ambavyo nimesema, wakulima wanapata matatizo hasa mazao yao yanapoungua, lakini ukiangalia faini inayotolewa pale ni shilingi laki mbili tu.

Mimi nadhani wanaohusika wapitie waone wazi kwamba, faini hii ni ndogo na hawa watakuwa wanafanya makosa kwa makusudi wakijua kwamba hawa wanaoagiza mbolea ni watu wenye uwezo mkubwa. Laki mbili kwao *is penalty.* Kwa hiyo, nilikuwa nadhani wabanwe *fine* iwe kubwa ili waweze kuleta vitu ambavyo ni bora.

Mheshimiwa Spika, labda kwa kumalizia nisisitize tu kwamba, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kuhakikisha tunapata maafisa ugani ambao wanajituma na wanaweza kufanya hizo kazi, hasa tukizingatia kwamba, wakulima wetu wengi ambao ni zaidi ya asilimia 70 mpaka 80 wengi wao hawana utaalamu wa kilimo. Maafisa ugani ambao Serikali inawasomesha wahakikishe kwamba wanaenda vijijni wasikae mijini, kuhakikisha kwamba wanatoa utaalamuu wao kwa wakulima wetu ambao ndiyo tegemeo kubwa la uchumi wa nchi, hasa tukizingatia kwamba, tuna matatizo makubwa ya mtikisiko wa uchumi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia mwenendo mzuri wa kuendesha shughuli zetu, jumla ya Waheshimiwa Wabunge watatu walichangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na nina hakika wengine wamechangia kwa maandishi. Sasa muda ambao Wizara imepewa kwa mujibu wa kanuni ni saa moja na robo ambayo itapita. Sasa hivi ni takriban saa sita; sasa itakuwaje, itabidi tuendelee tu mpaka muda uliopangwa kikanuni utakapofika.

Kwa sababu hiyo lakini pia kwa sababu huwa ni vizuri hatua ya Bunge kukaa kama Kamati ya Bunge ifuatane hapo hapo na tumemsikiliza Mheshimiwa Waziri anavyojibu hoja zetu; vinginevyo unapozitenganisha inakuwa haina ufanisi sana na isitoshe leo Kamati tano zinakutana. Kwa sababu zote hizo, naamua sasa kusitisha shughuli za Bunge kabla ya wakati wake hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.03 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilipokuwa nasitisha shughuli za Bunge pale mchana, ilikuwa tayari wachangiaji wote kuhusu Muswada huu wamekwishachangia. Kwa hiyo, kama ulivyo utaratibu wetu, sasa ukiacha mmoja ambaye ni Naibu Waziri, ana haki yake ya dakika kumi na tano, baada ya hapo nitamwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, aweze kutoa maelezo au kama wamegawana tofauti pia tutaruhusu ilimradi ni saa moja na robo ndiyo muda wenu; sasa kama Naibu Waziri atachukua nusu saa basi Waziri atachukua dakika 45.

Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Ningependa kuchukua nafasi hii pia, kuungana na Wabunge wenzangu, kuipa pole familia ya Marehemu Mheshimiwa Faustine Rwilomba, aliyekuwa Mbunge wa Busanda, aliyetutoka hivi majuzi na Wananchi wa Busanda. Nawatakia kila la kheri katika uchaguzi, waweze kuchagua kiongozi atakayewafaa.

Mheshimiwa Spika, nitakwenda moja kwa moja kwenye hoja kwa kuzingatia kwamba, muda wenyewe siyo mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa inazungumzia umuhimu wa kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi ya mbolea. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Benito W. Malangalia, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Diana M. Chilolo na Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 8 miongoni mwa majukumu ya Mamlaka ya Mbolea ni pamoja na kuhamasisha na kutoa elimu ya masuala yanayohusu mbolea ili kuongeza matumizi ya mbolea nchini kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 8(1)(k) kama kilivyorekebishwa katika *schedule of amendment*, yaani katika jedwali; elimu juu ya mbolea ni muhimu sana hasa katika kuwajulisha wananchi aina gani ya udongo ambayo wanalima na ni aina gani ya mbolea ambayo itafaa kwa udongo huo; yaani kwa maana ya kupandia na kukuzia na ni virutubisho gani hasa ambavyo vimekosekana na ambavyo ndivyo vinatakiwa viwepo kwenye udongo huo ili mimea iweze kukua na kuzaa inavyotakiwa. Pia njia za kusambaza ile mbolea ama za kuweka katika yale mazao au mashambani ni muhimu sana. Elimu hii Wizara inaendelea kutoa, vyuo vyetu vya utafiti vinaendelea kutoa na Maofisa wetu wa Ugani waliopo Wilayani na Mikoani wanaendelea kuitoa. Sasa hivi tuna programu ya kusomesha Maofisa Ugani 11,703 ili ifikapo mwaka 2011 tuwe tumefikia Maofisa Ugani 15,000.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa inazungumzia umuhimu wa kujua sifa za udongo ili kutumia mbolea kulingana na aina ya udongo. Hii ni muhimu sana, kwa sababu tumeshasikia baadhi ya wakulima wakilalamika kwamba, mbolea fulani haifai au mbolea fulani inaharibu udongo.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu kifungu cha 8(q) kimezingatia suala hili na vyuo vyetu vya kilimo, kwa mfano, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Chuo Kikuu cha Mlingano cha Research na Uyole, vyote hivi na vingine ambavyo sikuvitaja, vinashughulikia utafiti wa udongo na kujua udongo huu unahitaji madini gani na una ukosefu wa madini gani. Wakati Sheria hii inaanza kutumika, vyuo hivi tutavitumia kwa ukamilifu kabisa kusudi viweze kutupa majibu ambayo yatatupa aina gani ya mbolea ya kutumia.

Kwa mfano, hii mbolea inayoitwa Minjingu Phosphate yenyewe inahitaji udongo wenye *acid.* Mbolea hii ukiiweka kwenye udongo ambao PH yake iko juu, yaani kuanzia 5.5 maana yake ni kwamba, haitaleta mafanikio yanayotarajiwa kwa sababu Minjingu Phosphate ina *Phosphate* na *Calcium.* Kwa hiyo unaongeza vitu ambavyo vipo vyote kama PH ipo. Udongo ambao ni *acidity* maana yake PH iko chini, basi huo unaweza ukaweka Mbolea ya Minjingu, lakini udongo wenye alkali au PH ikiwa juu, basi unaweka DAP ambayo inashusha ile alkali; kwa maana hiyo mazao yanaweza yakaota vizuri.

Mbolea hii ya Minjingu inahitaji pia maeneo ambayo yana mvua ya kutosha. Maeneo ambayo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumza kwamba Minjingu haifanyi kazi ni kwa sababu yenyewe inahitaji maeneo yenye mvua ya kutosha; kwa hiyo, maeneo hayo ambayo yalikuwa na mvua kidogo, kwa kweli Minjingu haikuleta matokeo mazuri.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Dkt. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Martha J. Umbulla na Mheshimiwa Juma H. Killimbah.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwamba, mbolea ya chumvichumvi huharibu ardhi. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Teddy L. Kassela-Bantu, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Martha J. Umbulla na Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah.

Mheshimiwa Spika, mbolea ya chumvichumvi ni kemikali, kwa hiyo, isipotumika vizuri kulingana na ushauri wa wataalamuu hususan maeneo yanayopendekezwa na mgao sahihi wa mbolea ile, basi mbolea ile haitaleta mafanikio na pengine ikaleta madhara zaidi. Kwa hiyo, ni muhimu kama tunavyosema, elimu itolewe kwa watumiaji wale ili tuweze kujua tabia ya udongo kama udongo huu unahitaji mbolea inayohitaji udongo wa asidi au udongo wa alkali kwa maana ya *high PH.*

Kwa hiyo ni muhimu kufuata masharti ya mbolea husika, maana mbolea hizi zinatofautiana. Vilevile ni vyema tuelewe ni kiasi gani cha mbolea ambacho kinawekwa na njia za kuweka; maana kwa mfano, mbolea ya Minjingu njia yake ambayo inaleta matokeo mazuri ni ile ya *broadcasting*, ambayo unasambaza kwa mikono bila kuchimbia ile mbolea. Pia ni muhimu kuweka wakati ambao zipo mvua nyingi kama hakuna mvua maana yake haitaleta matokeo yanayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine ilisema kwamba, mbolea ya Minjingu imeonekana kutofaa; nadhani nimeshatoa majibu kwamba inafanya kazi vizuri kwenye maeneo yenye mvua nyingi. Maeneo yenye upungufu wa *phosphorus*, maeneo yenye tindikali ya chini, yaani PH na maeneo tofauti na haya, hayaonyeshi matokeo mazuri kama alivyosema Mheshimiwa Godfrey Zambi kwamba, kwenye maeneo yake haikuleta matokeo mazuri. Hili ni dhahiri kabisa kwamba, Halmashauri za Wilaya hazikufuata maelekezo yaliyotolewa na Wizara kwamba, wajue aina ya udongo walionao kabla ya kutumia mbolea ya Minjingu. Wizara iliandika barua tangu tarehe 15 Februari kwamba, Mikoa yote na Halmashauri zote ziainishe aina za udongo ili waweze kujua kama mbolea ya Minjingu itaweza kutumika au haitaweza kutumika kutokana na bei yake kuwa ya chini.

Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria hii ama Muswada huu, inapendekezwa kuwa kutakuwa na Kanuni zitakazokuwa zinathibitisha pia mbolea mpya na zitafanyiwa utafiti bila kutumiwa hapa nchini na zitatumika kutokana na maeneo ya kijiografia; jinsi tabia ya udongo ilivyo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ya mbolea ya Minjingu kuonekana kutofaa, imechangiwa na Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Christant Mzindakaya, Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Benito Malangalila.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa inazungumzia bei ya mbolea kuwa kubwa na kulikuwa hakuna *control*. Napenda kusema kwamba, kifungu cha 8(1)(u) katika *schedule of amendment*, kama kilivyofanyiwa marekebisho, kinaipa uwezo Mamlaka ya Mbolea kusimamia pia bei ya mbolea, kwa kuzingatia utaratibu utakaokuwa umeainishwa kwenye Kanuni. Kama wanavyofanya wenzetu wa EWURA na taasisi nyingine ambazo zinasimamia bei, basi Mamlaka hii imepewa uwezo huo wa kuweza kusimamia bei na bei hizi zitatokana na *factors* nyingi, zikiwemo bei ya soko la dunia. Kwa mfano, DAP ilivyokuwa ghali ni kwa sababu mafuta ya *petrol* ambayo yanahusika katika kutengeneza mbolea hii yalikuwa aghali, lakini mafuta yaliposhuka DAP nayo ikashuka bei.

Sasa kuna wafanyabiashara wengine ambao siyo waaminifu, bado wanauza DAP kwa bei ya juu pamoja na kwamba bei imeshuka. Kwa hiyo, Mamlaka hii itapewa uwezo wa kuhakikisha kwamba, bei za mbolea zinakuwa *regulated* vizuri ili zisimuumize yule mtumiaji; kama nilivyosema, wata-*consider* soko la dunia lakini usafiri pia wa kutoka maeneo kama Dar es Salaam kama imeshushwa bandarini, bei ya Morogoro haiwezi kuwa sawa na bei ya Mbeya ama Songea; ni lazima kutakuwa na tofauti kidogo kwa

sababu ya gharama za usafiri. Aina ya mbolea pia itakuwa ina-*determine* bei ya mbolea ile; kuna mbolea zinazotengenezwa na *petroleum product* na mbolea nyingine zinatengenezwa kwa madini kama Minjingu Rock Phosphate, zinatofautiana gharama za kutengeneza. Kwa hiyo, hata bei zake pia zitakuwa za chini. Mbolea za kupandia na kukuzia, bei zake zina tofauti kubwa.

Ujazo wa vifungashio kwa sababu katika Muswada huu tumezingatia sana kuwepo na kifungu ambacho kinazungumzia masuala ya vifungashio, tunaelewa kabisa wananchi wana uwezo tofauti katika kutumia mbolea; wengine watahitaji kilo 50, lakini wengine wana uwezo wa kununua kilo 5 za kutumia kwenye bustani zao. Kwa hiyo, ujazo nao utakuta unataja bei.

Mheshimiwa Spika, hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Margreth A. Mkanga, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia na Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza kwamba, vifungashio pia ni muhimu sana na kwamba, Muswada huu uzingatie vifungashio kama nilivyosema kwamba wakulima wana uwezo tofauti.

Kanuni ya 55(2)(h) ya Muswada, imezingatia suala la vifungashio ambavyo nimeshazungumza mifano yake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Said Amour Arfi, alizungumzia suala la mbolea inayoitwa *Earthfood* kwamba mbona hairuhusiwi kutumika. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaitambua mbolea hii inayoitwa *Earthfood*. Serikali ilishapata taarifa hizi tangu mwaka 2005 na ililetwa na kampuni inayoitwa *Tanzania Investment Group* na ikafanyiwa utafiti na Chuo cha Kilimo cha Sokoine, Chuo cha Uyole Kibaha na Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti huu ni kwamba, mbolea hii ina sifa zinazofanana na zile za mboji na kwa maana hiyo ina kiasi kidogo cha viinilishe. Kwa hiyo, itakuwa inahitajika kwa kiasi kikubwa sana ili iweze kuleta matokeo ya kilo 50 za mbolea ya viwandani; basi inabidi tani tatu za mbolea hii ndiyo zinaweza kukidhi mahitaji hayo. Hata hivyo, kwa sababu mbolea hii inaongeza uwezo wa udongo wa kuhifadhi unyevu unyevu basi na virutubisho vipo japo si kwa kiasi kikubwa. Serikali iliruhusu tangu tarehe 28/2/2005.

Kampuni ambayo inaleta mbolea hii ilipewa masharti kwamba, iitangaze mbolea hii na iandae vifungashio ambavyo vinaandika asilimia ama viwango vya virutubisho vilivyomo humo ndani; kwamba, *nitrogen* iko kiasi gani, *phosphorous* iko kiasi gani na

*potassium* iko kiasi gani ama madini mengine ambayo yamo humo ndani. Bila ya kuandika kwenye mifuko virutubisho ambavyo vilipatikana baada ya uchunguzi wa mbolea hii, mbolea hii haitaruhusiwa kuuzwa. Nasema waliruhusiwa na walipewa masharti ya kawaida kama mifuko hii ya DAP asilimia zinavyoandikwa pale *Diamonium Sulphate* kwamba, *nitrogen* iko ngapi, *phosphate* iko ngapi, NPK nayo ni hivyo hivyo. Kwa hiyo na wao walitakiwa waeleze ni nini kimo humo ndani kwa maandishi yasiyofutika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila pia alizungumzia suala la utitiri wa vyombo kwenye Muswada huu. Nadhani akiangalia kwenye jedwali, yaani *Schedule of Amendment,* atakuta kwamba Kamati ya Ushauri ya Taifa na Kamati ya Ushauri ya Wilaya vimeondolewa; kwa maana hiyo Bodi ya Mamlaka hii ya Udhibiti wa Mbolea itaunda *technical committee* ambayo ndiyo itakuwa na ushauri na itakuwa na wataalamuu wa mbolea kutoka kwenye maeneo mbalimbali.

Ile Kamati ya Wilaya ya Ushauri ni kwamba, badala yake Mamlaka hii ya Usimamizi wa Ubora wa Mbolea itakuwa na matawi yake na ofisi zake kule Wilayani kama ilivyo katika Mamlaka nyingine za TBC, EWURA na kadhalika. Kwa hiyo, wale watakuwa wanaangalia ubora wa mbolea, lakini Kamati ya Pembejeo ya Wilaya ambayo inahusika kwenye mbolea, dawa au kwenye mbegu. Kazi ya kugawa ruzuku itaendelea kuwa yake, kwa hiyo haikuondoka, tusichanganye kati ya Kamati za Ushauri za Wilaya na Kamati ya Pembejeo ya Wilaya, ile itaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Susan Lyimo alizungumzia *composition* ya Kamati ya Ushauri wa Taifa. Napenda kumfahamisha kwamba, akiangalia kwenye jedwali atakuta Kamati hiyo haipo tena. Angesoma vizuri, maana alisema amesoma Muswada wote lakini nadhani hapo hakupasoma.

Mheshimiwa Spika, alizungumzia pia *quality assurance*. Napenda kumjulisha kwamba, ubora wa mbolea umesisitizwa. Akiangalia kifungu cha 36 cha Muswada huu, ataona tumezungumzia masuala mazima ya ubora. Chanzo cha kuandaa Muswada huu ni kwa sababu ya kuhakikisha ubora wa mbolea inayoingia nchini na ndiyo maana tukazungumzia masuala ya ku-*register* ile mbolea, ku-*permit* na ku-*test* ile mbolea ikiwa bandarini. Kuna masuala ya kuifuata kule kwenye *premises* au *store* ambapo mbolea ipo, yote haya ni ku-*assure quality* au ubora wa mbolea hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa William H. Shellukindo ametupa ushauri; kuna baadhi ya maneno ambayo yanahitaji kuwekewa koma; kuna baadhi ya sentensi zinatakiwa kuwa na *full collon* ama kuwekewa alama zile kwa ujumla. Kwa hiyo, masuala yote hayo aliyoyasema tutayazingatia. Wanasheria wetu wakiandika Sheria hii watakuwa wamezingatia masuala yote hayo ili maneno hayo yote yaweze kuleta maana kamili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri na sasa nitamwita mtoa hoja; Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa maelezo ya kuhitimisha hoja hii, kabla Bunge lako tukufu halijafanya kazi ya mwisho ya kuidhinisha Muswada huu wa Sheria, baada ya kupitia hatua nyingine zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa maelezo, ningependa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, walioshiriki katika mjadala huu na nawashukuru sana kwa kutuunga mkono; ni wawili tu ndio walisema wanawasilisha bila kuunga mkono, lakini walio wengi wamesema wanaunga mkono. Hata wale waliosema wanawasilisha ni kawaida yao tu kusema hivyo, lakini kwa kawaida huwa wanaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, ningependa nitambue wale ambao wameshiriki katika mjadala kwa kusema hapa na vilevile wale ambao wameandika.

Mchangiaji wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Benson M. Mpesya; yeye alisema kwa niaba ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anatoka Mbeya Mjini. Mheshimiwa Salim Hemed Khamis - Msemaji wa Kambi ya Upinzani kutoka Chambani, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Tatu M. Ntimisi, Mheshimiwa Dkt. Getrude Mongella, Mheshimiwa Yono S. Kevela wa Njombe Magharibi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Bujibu Sakila, Mheshimiwa Luka Siyame, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo na Mheshimiwa Dkt. David M. David, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula Ushirika. (*Makofi*)

Waliochangia kwa maandishi wapo 20 nao ni Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Bernadetha K. Mushashu, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Dkt. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Margreth A. Mkanga, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia na Mheshimiwa George M. Lubeleje.

Mheshimiwa Spika, hao ndiyo waliochangia, nawashukuru sana. Nawashukuru vilevile waliokuwa wamenyamaza na huku wanatuunga mkono; wote nawashukuru sana.

Baada ya kutambua watu waliochangia, ninapenda sasa kujibu baadhi ya hoja. Kwanza, namshukuru Naibu Waziri, kwa sababu amejibu hoja sehemu kubwa kwa kweli ya zile ambazo zilizokuwa zinahusiana moja kwa moja na vifungu mbalimbali vya Muswada tunaouzungumzia. Kwa hiyo, nitazungumza mambo ya jumla zaidi, lakini baadaye nitakwenda kwenye mambo ambayo yamemhusu Mbunge mmoja mmoja ambaye ametaka maelezo.

Maanza na maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Benson M. Mpesya kwa niaba ya Kamati. Kwanza, naishukuru sana Kamati kwa ushauri mzuri, pamoja na kwamba narudia kwa haraka walichosema, lakini kwa kweli naunga mkono na tunachukua kama ushauri kutoka kwenye Kamati ambayo tunafanya kazi nayo siku zote kwa ushirikiano mkubwa.

Ilitaka Serikali iendelee kuhamasisha na kutoa elimu kwa wakulima; Naibu Waziri amelieleza vizuri jambo hili na kwa kweli moja ya kazi yetu kubwa ambayo inakwenda sambamba na Muswada huu ni kuhakikisha ya kwamba, wakulima wanaelewa kutumia mbolea na kama hawawezi kuelewa kutumia mbolea tutakuwa tunafanya kazi nusu. Muswada huu una makusudio ya kuhakikisha ya kwamba, mbolea zinazoingizwa kwanza zitakuwa na ubora, lakini vilevile ziwe zinatumika kwa namna ambayo itawawezesha wakulima kufaidika. Kwa hiyo, hili tunalichukua.

Serikali iandae mipango ya kutengeneza mbolea nchini; mipango hii inaendelea sasa hivi na kwa kweli ipo katika hatua nzuri. Tunayo malighafi kule Kusini mwa Tanzania ambako kuna gesi na kuna makampuni kadhaa ambayo yameonyesha nia ya kutaka kuwekeza yapo katika mchakato. Matumaini ni kwamba, mchakato huo utakapomalizika, baada ya muda si mrefu Tanzania inaweza kutengeneza mbolea yake ya na aina nyingine hapa hapa nchini.

Vilevile tunajivunia kuwepo kwa Minjingu, pamoja na matatizo madogo ambayo yametolewa maelezo na mengine tutayatoa hapa; lakini kusema kweli ni vizuri nchi yetu ianze kujiandaa kuwa na mbolea inayotengenezwa hapa nchini ili kupunguza gharama na kuwa na uhakika; kwa sababu hakuna Mapinduzi ya Kilimo bila kuwepo na pembejeo muhimu ikiwemo mbolea.

Kamati vilevile imetoa ushauri kwamba, Serikali ijizatiti kupunguza utitiri wa vyombotumeshalieleza. Kuhusu kujaribu kutazama utaratibu wa kusimamia bei, chombo hiki kitasimamia bei, kitatazama na kitafanya kama vinavyofanya vyombo vingine kama SUMATRA na EWURA ili kuhakikisha ya kwamba, mbolea ile inamfikia mkulima kwa bei nafuu, kwa sababu hii isiposimamiwa wakulima wengi wataathirika. Tumeshaanza kuona kwamba, kila mtu akiuza kwa bei anayotaka, mbolea ya DAP ilifika shilingi 100,000; kwa mkulima hata kama angekuwa anapata nini ingelikuwa ni gharama kubwa. Kwa hiyo, tutatazama na chombo hiki tutakitumia na kuhakikisha ya kwamba, tunaweka utaratibu ambao mbolea itakuwa inafika kwa bei ambayo ni ya makubaliano ya chombo hiki na wafanyabiashara bila kuumiza upande wowote.

Suala la vifungashio limeshaelezwa vizuri na Naibu Waziri na Serikali ihakikishe inatengeneza Kanuni mapema. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, mara tu mkipitisha sheria hii, kazi ya kutengeneza Kanuni inaanza mara moja ili wakati tunasubiri sheria hii kuidhinishwa na Mheshimiwa Rais, basi tutakuwa tupo katika kutengeneza Kanuni ili ianze kutumika pamoja na Kanuni zake.

Ili kuwezesha matumizi sahihi ya mbolea, Serikali ifanye uchambuzi wa udongo. Hili limeelezwa na tumesema vituo vyetu vyote vya utafiti vikiongozwa na Mlingano, ambayo ndiyo kituo chetu kinachoshughulika na mambo ya udongo, pamoja na Chuo Kikuu SUA, vitatumika katika kufanya kazi hii na kuhakikisha kwamba udongo unaendana na mbolea inayotumika katika maeneo hayo.

Mamlaka hii itashughulika na kuweka vivutio, lakini itashirikiana na TIC ambayo ndiyo chombo kinachoshughulika na kusimamia mambo ya uwekezaji hapa nchini. Hayo ndiyo maoni yaliyotolewa na Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo.

Kambi ya Upinzani ilikuja na hoja, pamoja na maswali. Safari hii maswali ya Kambi ya Upinzani hayakuwa magumu ni rahisi kidogo kwa sababu swali la kwanza lilikuwa je, kuna umuhimu wa kuwa na Sheria ya Mbolea na itakuwa na manufaa kwa wakulima? Kwa kweli ningeweza kusema kwanza, kuna umuhimu wa kuwa na sheria na kila mtu sasa anaona upo umuhimu na itakuwa na manufaa. Kwa sababu mkulima huyu tukimwachia awe anapokea mbolea kiholela tu bila udhibiti na bila utafiti, anaweza kuuziwa chochote na katika mazingira ya soko huria mtu anaweza akauza chochote kwa jina la mbolea na hiyo itawaathiri sana wakulima wetu. Ndiyo maana nikasema, maswali ya safari hii ya rafiki yangu Khamis, hayakuwa magumu sana, yalikuwa rahisi.

Halafu ameuliza je, Muswada huu unazingatia Sera ya Kilimo na Mifugo? Nasema ndiyo. Amesema sera ile imenyamaza; mimi nasema siyo kweli, huwezi kuweka Sera ya Kilimo ambayo haisemi mbolea, haisemi mbegu; sasa itakuwa inasema nini! Kwa hiyo, sera hii inafanana kabisa na mahitaji ya sheria hii.

Je, wakulima wamehusishwa? Nasema ndiyo wamehusishwa, lakini wakulima wetu ni mamilioni huwezi kuwaita wote, isipokuwa wamehusishwa kwa namna moja au nyingine. Ndani ya sheria hii tumeweka Bodi; kutakuwa na wakulima wawili ambao watateuliwa kuingia kwenye Bodi hii ili kuwashirikisha na wao kuelewa kinachoendelea kwenye Bodi hii.

Suala la ukiritimba Bandarini haliwezi kuhusishwa na Sheria hii, linashughulikiwa na watu wa Wizara ya Miundombinu. Kwamba, Muswada huu unazingatia kupeleka madaraka kwa wananchi; ndiyo na shughuli hizi ni za Serikali za kupeleka madaraka kwa wananchi, maana yake siyo kwamba Serikali Kuu inabaki haina kazi hapana. Kwa hiyo, tunafanya na Serikali za Mitaa ambako madaraka yapo kule kwa wananchi na sisi tunafanya huku tunashirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, utengenezaji wa mbolea nchini nimekwishaueleza. Kuwepo kifungu cha sheria kinachoelezea jinsi ya kuharakisha utoaji wa mbolea inapoingia, hili ni suala la Bandari ambalo linashughulikiwa na wenzetu pale. Serikali itadhibiti vipi

wafanyabiashara kuhodhi mbolea? Sheria hii inataka biashara hii ifanywe kwa uwazi. Kwa hiyo, inakataa kabisa kutengeneza mazingira, ndiyo maana hata bei zitakuwa zinatazamwa na gharama zinatazamwa ili kuhakikisha kwamba, hakuna mtu anayehodhi na kwamba wakulima hawaonewi wala kuuziwa kwa bei kubwa zaidi bila kuwa na udhibiti.

Serikali iendelee kuhamasisha makampuni makubwa duniani kuleta mbolea; tumekwishaanza. Tumehamasisha YALA na YALA ni moja ya makampuni makubwa duniani, yanayotengeneza mbolea. Tumewapa eneo la ardhi Bandarini na wanatengeneza *warehouse* pale, watakuwa wanaingiza mbolea kwa wingi hapa nchini. Kazi hiyo ya kujenga *warehouse* itaanza wakati wowote kuanzia sasa. Kwa hiyo, tunayashirikisha makampuni makubwa ya dunia yalete mbolea.

Mheshimiwa Spika, neno *commit* liondolewe; limekwishaondolewa. Katika kifungu cha 25 baada ya kufuta neno Bodi na kuweka *Directors*, neno *itself* lifutwe na badala yake liongezwe neno *himself;* tumekwishalifuta. Vilevile katika kifungu cha 31 cha Muswada, sehemu ya pili, kinachosema *any person* kitazamwe upya kwa sababu wamesema likiendelea hivi litamuumiza mkulima hapana, *any person* ni *any person* ambaye ni mdau katika hiyo; anaweza kuwa mfanyabiashara au mkulima, lakini ni *any person*.

Kuhusu kifungu cha 34(7) amesema kina mkanganyiko, lakini kwa kusoma hatukuona mkanganyiko wowote na wala hakuna *section* 34(7). Kifungu cha 44 anasema kinamnyima haki mtu kueleza, lakini sheria nyingi hapa nchini zina vifungu vya namna hiyo, ambavyo vinasema kutokujua sheria haiwezi kuwa kinga *(ignorance of the law is not a defence);* na hii ina maana hiyo hiyo. Unaweza kusema mimi sikujua lakini hiyo haijatosha mpaka uthibitishe kuwa hukujua.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa mbolea kwa vocha uwekwe kwenye sheria. Hatuwezi kuweka utaratibu huu kwa sababu huu ni mradi tu na si kitu cha kudumu; ni kwamba tunawapa wakulima mbolea ya ruzuku, lakini wakati fulani wanaweza waka-*graduate* badala ya ruzuku sasa ukawapa mkopo. Sasa hivi huwezi kuiweka kwenye sheria, hizi ni programu za utekelezaji, kwa hiyo, haziwezi kuwekwa kwenye sheria hii ambayo ni ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, baada ya majibu hayo ya Kambi ya Upinzani, yapo maelezo machache ambayo ningependa kuyatoa ya baadhi ya wachangiaji ambao wamezungumzia samadi. Wengi sana wamezungumzia samadi, mboji na marejea.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kusema ya kwamba, Serikali na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, tunahimiza sana matumizi ya samadi. Tungependa kwa kweli samadi, marejea na mboji zitumike. Tatizo ambalo lipo ni upatikanaji tu, samadi inapatikana katika maeneo fulani fulani ya nchi yetu. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, kwenye samadi unahitaji kiwango kikubwa sana kuweza kupata virutubisho vinavyohitajika kama vile vilivyopo kwenye mbolea za kemikali. Kwa hiyo, ukitaka tuseme hakuna kemikali sasa ni samadi, unaweza ukarudisha nyuma kilimo hiki

kwa sababu hiyo samadi yenyewe inapatikana katika baadhi ya maeneo, kuna maeneo mengine ipo lakini haitoshi.

Kwa hiyo, nataka kusema tu kwamba, tuendelee na kasi hii na tunawatia watu moyo kutumia mbolea hii ya samadi. Labda hapa ningependa nitumie muda mfupi kumsaidia rafiki yangu Mheshimiwa John Cheyo; kwa sababu anasema tuwaachie watu wake wasitumie mbolea hii. Mimi ninamwambia hapo hapo kwamba, huwa tunakubaliana na mambo mengi, lakini katika hili hatukubaliani. Bahati mbaya na mambo haya ya kukubaliana ni hiari tu kwa siku moja moja, haiwezekani muwe mnakubaliana kila siku itakuwa ngumu, maana hata wewe na mama watoto siku nyingine hamkubaliani sasa sembuse mimi na wewe wote wazee itakuwa ngumu kidogo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nasema hivi; ni kweli katika maeneo ya pamba kuna mbolea ya samadi kwa sababu wafugaji wa ng'ombe wapo kule na samadi ipo. Nimekwenda Shinyanga nimetembelea *Projects* zinazoendeshwa DASP, nimekwenda katika Wilaya ya Maswa ambako kuna majaribio ya kuweka samadi, lakini yule ambaye ameweka samadi bila kuweka mbolea ya urea anapata kilogramu 750 kwa kilo na yule aliyeweka samadi halafu aka-*apply* mfuko mmoja tu wa urea anapata kilogramu 1,250 katika kijiji kimoja cha Maswa.

Kwa hiyo, upo ushahidi kwamba, kutumia samadi ni jambo linalokubalika; lakini kitaalam kutumia samadi halafu ukatumia na ongezeko la mbolea inayoingiza *nitrogen*, inasaidia ukuzaji wa mimea kwa haraka na inaweka matunda kwa wingi zaidi na huu ni utaalamuu ambao unathibitisha kisayansi. Sasa kwa sababu sayansi haitaki ubishi sana, maana matokeo yake ni mahesabu, tunaweza tukamsaidia tu Mheshimiwa John Cheyo kwenda kuona mahesabu yale yanavyofanya kazi ili awe sehemu ya viongozi wanaotoa elimu kwa wakulima kule Bariadi.

Mheshimiwa Spika, waliozungumzia suala hili wamekwishatajwa ilikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Getrude Mongella, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Luka Siyame, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Meryce Emmanuel na Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

Lilikuwepo suala lingine la utengenezaji wa mbolea kwa kutumia malighafi hapa nchini. Hili lilisemwa sana na Mheshimiwa Dkt. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Yono Kevela na Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia. Hili tumekwishalielezea kwamba, Serikali ipo kwenye mchakato wa kujaribu kupata wawekezaji wa kuwekeza katika sekta hii ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, wasemaji wengi sana wamesema kwamba, utaratibu wa vocha ni mzuri wanaomba uboreshwe. Mimi ninakubaliana na wote waliosema hivyo, kwa sababu huu ni mfumo ambao tumeuanza na una mwaka mmoja tu. Tumefanya majaribio mara ya kwanza, tumewafikia kama wakulima 700,000 kwa mwaka wa kwanza. Sasa katika mazingira hayo huwezi kusema mara moja tu mfumo huu ni kamili,

utakuwa na matatizo ya hapa na pale. Kwa hiyo, waliopendekeza kwamba, tutazame uwezekano wa kuufanyia marekebisho wote, nakubaliana nao. Waliozungumza hili walikuwa ni Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na Mheshimiwa Savelina Mwijage.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutumia nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, hasa kwa maeneo yale ambayo tumetumia mfumo wa stakabadhi, kama kuna mtu ana mawazo ambayo anafikiri yanaweza kutusaidia kubadilisha na kurekebisha mfumo na kuufanya uwe bora zaidi, mimi nitashukuru sana kuyapokea mawazo hayo. Nia yetu ni kuuboresha. Kitu kinachotia matumaini ni kwamba, mfumo ule kwa mara ya kwanza ni kweli tumefikisha mbolea kwa mkulima, lakini yametokea matatizo ya hapa na pale.

Mkulima ameipata ile vocha na akaenda kwa muuza mbolea akapata mbolea, yule ambaye hakwenda alikuwa ana lake jambo. Wale ambao ni wakulima hasa katika Nyanda za Juu Kusini, ambao wanajua bila mbolea hawawezi kuvuna wamekwenda na wamenunua mbolea kuliko mfumo wetu wa zamani ule ambao ulikuwa unampa mfanyabiashara anaenda kusambaza halafu tunakuja kumlipa. Hatuna uhakika ni mkulima gani amepata, lakini katika mfumo huu tuna uhakika mkulima yule ambaye tumempa vocha ndiye aliyepata mbolea.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa nitazame hoja mahususi ambazo zimesemwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, tena kwa madai kwamba, wanataka Waziri lazima nijibu. Sasa ukiambiwa lazima ujibu, halafu wewe usijibu unakuwa unakataa madai halali kabisa.

Moja ya hoja ilikuwa inatoka kwa rafiki yangu, Mheshimiwa Godfrey Zambi. Kwanza, nataka niseme, nilikwishapokea malalamiko ya Mheshimiwa Godfrey Zambi siku nyingi, juu ya jambo hili na tulichukua hatua kujaribu kujua *problem* hasa iko wapi mapema kabla hajaja; leo kusema hapa wakati mimi na yeye huwa tunaongea sana mambo haya ya mbolea kwa sababu huko ndiko tumefanyia majaribio na ndiko matumizi makubwa ya mbolea yalipo; kama unataka kupata *feedback* utasema na wale wanaoitumia kule kule.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachoweza kusema ni kwamba, kwanza, Mwezi Februari, 2008 tuliandika barua Mikoa yote nchini tukawaeleza kwamba, mbolea ya DAP wakati huo ilikuwa aghali sana, ilikuwa imefikia tani moja dola 1,250 ukilinganisha na dola 250 mpaka 300 ilivyokuwa mwaka 2007. Kwa hiyo, hata kama ungelitoa ruzuku kwa mbolea hiyo, usingeweza kutoa ruzuku kwa mbolea nyingi sana kwa sababu gharama yake ingekuwa kubwa. Bunge hili lilikuwa limetupatia ruzuku ya bajeti ya shilingi milioni 27 pamoja na ruzuku za mambo mengine jumla shilingi milioni 31, hiyo isingetosha kama tungetaka kutoa ruzuku kwa mbolea yenye bei ya shilingi 100,000 maana ingelibidi tutoe kama shilingi 50,000 kwa kila mfuko mmoja, ambapo gharama yake ingekuwa kubwa sana.

Kwa hiyo, tukawaeleza kwamba itatumika Minjingu, lakini barua hii niliyonayo, bila kupoteza muda wa Bunge hili, inaeleza Minjingu inafaa kutumika katika maeneo gani. Naibu Waziri amekwishaeleza kwamba, kitaalamu inatumika katika maeneo ambayo tindikali yake ipo chini ya HP 5.5, lakini kama ipo 5.5 na kwenda juu, huwezi kutumia Minjingu; ndivyo wataalamuu wanavyotuambia. Kwa hiyo, tuliwaambia wahakikishe maeneo ambayo yanapingana na vipimo hivyo vya kitaalamu yasipelekewe Minjingu na kwa maeneo hayo tulipeleka DAP, pamoja na ughali wake ili itumike katika maeneo hayo na wala siyo Mbozi peke yake.

Ninafahamu Mkoani Iringa kuna maeneo kama Isimani, ambapo mvua zake ni chache hatukuwaambia watumie Minjingu au maeneo ya Wilaya ya Njombe maeneo ya Wanging'ombe, tulikubali watumie DAP kwa sababu matokeo ya Minjingu yasingekuwa mazuri. Mbeya vilevile mfumo ni ule ule wa kutazama ni eneo gani wapeleke na eneo gani ambalo haliwezi kufanyika.

Baada ya kupokea malalamiko ya Mheshimiwa Godfrey Zambi, tuliwataka wataalamu wa Mbozi watoe maelezo; kilichotokea wametujibu na tunayo barua ndefu kidogo, ambayo siwezi kuisoma, lakini nitainukuu tu wanasema; matumizi ya mbolea ya MRP Wilayani Mbozi siyo mageni, kwani wakulima kwa miaka kadhaa wamekuwa wakiitumia kwenye mazao ya kahawa, maharage na viazi mrivingo. Kwa hiyo, kusema kweli siyo kwamba, mbolea hii haitumiki kabisa huko. Wamekuwa wanaitumia ila hii ndiyo itakuwa mara ya kwanza wao kutumia kwa zao la mahindi na hii ni kweli kwa sababu hata Mheshimiwa Mbunge mmojawapo hapa analima kahawa Mbozi na anaitumia Minjingu miaka yote na anasema mambo yake yanamwendea vizuri. Mambo haya yapo na ushahidi upo.

Mheshimiwa Spika, lakini tulipoanza sasa kuzungumza habari ya kutumia Minjingu kwa ajili ya mahindi, wataalamu wetu walitoa ushauri kule kwamba, kiasi cha MRP ndiyo Minjingu hiyo kinahitajika kwa eneo la ekari moja iwe ni mifuko miwili. Katika hii mifuko miwili, lazima iongezewe kilo 25 za urea kabla hujapanda. Kwa hiyo, vocha yetu ile ilikuwa inaenda kwa eka moja na ukipewa mifuko miwili ya urea unatumia nusu mfuko wa urea unaweka pamoja na ile Minjingu. Kwa hiyo, hiyo inasaidia ile mimea kukua, hatuna uhakika kama maeneo yaliyopata matatizo kama kweli utaratibu huu ulifuatwa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupanda kiasi cha urea kinachotakiwa kuchanganywa na MRP kwa ajili ya kutosheleza eneo la ekari moja ni kilo 25 za urea. Ushauri huu tulitegemea ufikishwe kwa wakulima, siwezi kuwa na uhakika kama kweli ulifikishwa kwa sababu wakati mwingine tuna matatizo sana na *extension services* zetu mahali pengi; kwa hiyo, ni tatizo linalowezekana vilevile kuwa limetokana na elimu yetu kutowafikia wakulima kwa urahisi.

Tatizo kubwa lililolalamikiwa ni kwamba, mahindi yalipokuwa yanaota hayakuwa na afya nzuri na rangi ya kijani kama yalivyokuwa yale wanayotumia DAP. Haya ndiyo malalamiko tuliyopata kutoka kwa wakulima na wataalamu wetu kule wanasema nini?

Wataalamu wetu wanasema ni kweli mahindi yaliyopandiwa mbolea aina ya MRP katika hatua za awali za kukua yalikuwa ya njano, ikilinganishwa na mahindi yaliyopandwa kwa DAP. Hata hivyo, baada ya wiki tatu hadi nne mahindi hayo yalibadilika rangi na kuwa ya kijani na kukua kwa kasi. Huu ndiyo utafiti ambao umefanywa na wataalamu. Maeneo ambayo wakulima walipanda kukiwa na unyevu kidogo, matokeo hayakuwa mazuri kwa sababu hii mbolea inatumika zaidi kwenye unyevu mwingi, ndiyo maana inatakiwa itumike kwenye mvua nyingi.

Wapo wakulima ambao hawakupata tatizo kabisa, lakini wametumia hii mbolea. Hizo ni *findings* za wataalamu kutoka kule Mbozi. Baadhi ya wakulima hawakufuata maelekezo na kuna wengine walipopata mifuko miwili badala ya kuweka kwa eka moja wakaweka kwa eka mbili wakiona ile ni nyingi, kumbe hii ni tofauti na DAP ambayo unaweka mfuko mmoja kwa eka moja. Hii hapa unahitaji miwili kupata DAP moja. Kwa hiyo, hiyo nayo imetokea.

Matokeo ni kwamba, hali si ya kutisha au ni mbaya sana, lakini tumefanya utafiti mbolea hii imetumika katika kata 13 katika Wilaya ya Mbozi na watafiti wetu kule wametuletea asilimia ya mafanikio; karibu kata zote zimevuka kiwango cha asilimia 60 ya mafanikio, isipokuwa kata moja tu ambayo inaitwa Nambizo, sijui kama ninaitamka vizuri. Kata hii ipo chini ya *average* ni 32. Kwa hiyo, hapa tuna tatizo, ambalo wataalamu waliotafiti hawawezi kutuambia jibu kwa nini. Kwa hiyo, tumechukua hatua tunawatuma wataalamu wetu wa Uyole washirikiane na Chuo Kikuu cha Sokoine Morogoro, wafanye utatifi kwa nini hali imekuwa hivyo kabla hatujapata jibu la mwisho la kisayansi. Inawezekana eneo hili si katika maeneo yale ambayo yalitakiwa kutumia Minjungu, labda ni maeneo yale ambayo HP yake iko 5.5 au zaidi ambayo haiwezi kufanya kazi.

Kwa hiyo, pamoja na kumwonea huruma sana rafiki yangu, lakini sasa nilisema mambo haya yametokea ngoja kwanza tuendelee na utafiti. Kitu ambacho tunafanya kwa ajili ya Mbozi na ambacho tumeshaamua leo ni kwamba, Wilaya ya Mbozi udongo wake ufanyiwe utafiti wa kina ili tuweze kujua haraka iwezekanavyo ni maeneo gani yanafaa kwa mbolea gani ili tusije tukarudia kosa na tukapata matatizo kama ambayo yametokea katika kata niliyoisema.

Mheshimiwa Godfrey Zambi, alikuwa anasema usimamizi na ubora wa mbolea ni mbaya; umeshaelezwa kwamba sheria hii itajibu hili tatizo. Serikali inashughulikiaje tatizo la mazao ya Wakulima wa Mbozi; ndiyo hatua hizo tunazozichukua kujua kilichotokea katika hiyo kata, maana nyingine zinaonekana zime-*perform* vizuri.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, amezungumzia juu ya usambazaji wa mbolea uzingatie muda. Sisi tunakubaliana na ushauri huu, kwa sababu muda ni muhimu sana katika kilimo. Ukikosea muda, msimu unaisha maana yake unaisha bila mazao. Kwa hiyo, tunakubaliana na ushauri wake na tunamshukuru sana, alishirikiana vizuri na wataalamu wetu kule Songea wakati kulipokuwa na tatizo kubwa. Mtalaamu wetu alikwenda na alikuwa anafanya naye kazi kwenye *field* kuhakikisha ya kwamba, matatizo ya wakulima yanapatiwa majibu pale pale na wataalamu wakiwepo.

Napenda kutumia nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kujitahidi kufanya kazi yake hiyo. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunataka kumuahidi ya kwamba, tutazingatia Azimio la Mlale. Lipo azimio kule linaitwa Azimio la Mlale, tumepewa lile azimio ni la siku nyingi kidogo, lakini linafanya kazi kama ilivyo siasa ni kilimo; ukisoma leo inakuwa kama ilivyokuwa na Azimio la Mlale nalo liko *valid.* Kwa hiyo, tutalitumia lile kwa ajili ya ku-*serve* Mkoa wa Ruvuma. Amesema sheria nyingine ziangaliwe ili ziweke mfumo shirikishi katika mfumo wa utekelezaji wa sheria kama ile ya *Agriculture Inputs Trust Fund;* tunakubali na tunajaribu kuitumia hiyo kuona jinsi tunavyoweza kuhuisha hizi sheria ili ziweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Dkt. Chrisant Mzindakaya alihoji ni watu wa aina gani ambao watakuwa *inspectors*; hawa watakuwa ni wataalamu wa kilimo lakini watapewa mafunzo maalumu ili waweze kuwa na uwezo wa kufanya kazi hii ya *inspection* kwa ajili ya viwanda vinavyotengeneza mbolea, maghala yanayohifadhi na kadhalika. Aliuliza sheria itawekaje misingi kuhakikisha kwamba haitaathiri TFC? TFC itaendelea kuwepo wala haina uhusiano na hii. TFC ni chombo cha Serikali, ambacho kinasambaza mbolea na hiki ni chombo cha Serikali ambacho kina-*regulate* biashara ya mbolea. Kwa hiyo, kazi ya TFC inaendelea bila matatizo.

Tuweke mkazo katika maamuzi ya gesi asilia; nimekwishasema tutaweka mkazo na mchakato unaendelea. Alisaidia kueleza kwamba, mbolea ya Minjingu haiharibu kama ambavyo inasemwa, kinachotakiwa ni kuitumia vizuri. Mimi nakubaliana na ushauri wake na tutaendelea kufanya kazi yetu kwa kuzingatia utaalamu zaidi ili tuhakikishe ya kwamba, elimu inawafikia wakulima ili uamuzi wetu na nia yetu ya kuwasaidia iwape matunda badala ya kuwapa matatizo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ningependa kuitolea maelezo ni ya Mheshimiwa John Cheyo, ambayo nilikuwa nimeianza mwanzoni kwa kueleza kwamba; mbolea ya samadi ni nzuri lakini kusema kweli ina upungufu wa virutubisho ambavyo vinahitajika kuongezewa hasa *nitrogen*.

Vipo virutubisho mbalimbali katika zile mbolea, lakini vyote ni pungufu; kwa hiyo, ukiviongezea mbolea kama ile iliyo na *nitrogen* kama urea au mbolea nyingine ya namna hiyo au can, basi unasaidia mimea iliyopandwa katika maeneo hayo kuweza kukua kwa haraka. Kwa hiyo, virutubisho vinavyotakiwa kuongezewa mle ni pamoja na *nitrogen, phosphorus*, *potassium*; hivyo vyote ambavyo vinahitijika kuongezewa katika kuifanya mbolea ile iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kama ilivyo kawaida ya rafiki yangu Mheshimiwa Cheyo, aliamua kuzungumza jambo ambalo halina uhusiano wowote na mbolea nalo ni bei ya pamba. Akatumia nafasi hiyo, kwa sababu unajua wanasiasa wakipata *platform* wanaitumia namna yoyote. Sasa akatumia kunisema na kunisingizia ambapo ni kinyume cha Kanuni za Bunge hili. Nitaelezea alivyonielezea; kwanza, alisema nimekwenda

Bariadi nikasema bei ya pamba itakuwa shilingi 200. Mimi nimetembea Shinyanga siku saba; Mheshimiwa Luhahula tulikuwa naye kule kwake Bukombe, yale niliyoyasema Bukombe ndiyo niliyoyasema Maswa, ndiyo niliyoyasema Meatu na ndiyo niliyoyasema Bariadi.

Niliwaambia yafuatayo na najinukuu mwenyewe nilisema: "Uchumi wa dunia una matatizo na matatizo ya dunia ya uchumi yameathiri zao la pamba kwa sababu mahitaji *(demand)* ya pamba imeshuka na hiyo bei imeshuka. Nikawaambia wakulima wa pamba, huu hauwezi kuwa mwisho wa dunia, kwa sababu Serikali ipo pamoja na wao." Ndiyo nilivyosema na narudia hivyo hivyo kwamba, wasing'oe pamba wala wasiache kuitunza, kwa sababu Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha pamba ile inanunuliwa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia kwamba, hivyo ndivyo nilivyosema na leo ndivyo ninavyosema; waitunze kwa sababu tutahakikisha inanunuliwa. Nilipofika Bariadi nilinong'onezwa kwamba, Mheshimiwa Cheyo alikuwa amewaambia watu wake akija Waziri wa Kilimo muulize bei itakuwa ngapi?

Nikawa-*pre-empty* nikawaambia nimejua mnataka kuniuliza bei, mimi sina bei leo. Hivyo ndivyo nilivyosema, nilikuwa kwenye uwanja kilomita nne kutoka Mjini Bariadi tena siyo katika Jimbo lake, lilikuwa Jimbo la Mheshimiwa Chenge. Mambo ya kweli ndiyo hayo. Sasa yale aliyoyasema Mheshimiwa Cheyo, kwa umri wake siwezi kusema ni uongo lakini si ya kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu simtegemei Mheshimiwa John Cheyo aseme uongo; ni mtu mzima huyu, watu wanaosema uongo kwa kawaida huwa ni watoto na mimi niliongopa nilipokuwa mtoto. Watoto wote huwa wanasema uongo, wakishakuwa watu wazima wanaacha hiyo kazi ya kuongopa, ndiyo maana sina hakika kabisa kama haikuwa bahati mbaya.

Nataka niseme la mwisho; wakulima wa pamba lazima tukubalia kubadilika. Maana maswali mengine ambayo nasema ya mfumo wa kununua, tuna mifumo mingi; huko Mara kuna kitu kinaitwa *contract farming* wameanza kwamba huyu anakuwa na mkataba na wakulima, wanalima anawapa pembejeo halafu wanamuuzia; huo nao ni mfumo.

Uko mfumo mwingine unaitwa stakabadhi ghalani, umefanya kazi nzuri kule kwenye korosho. Mifumo yote hii hatuwalazimishi wakulima, tunawashawishi wale wanaokubali wanaofuata.

Umefanyiwa majaribio katika Mkoa wa Shinyanga na kwa mwaka juzi ukiondoa mwaka huu ambao umekuwa na bahati mbaya kwa sababu ya uchumi wa dunia, bei waliyopata wale walioingia kwenye mfumo ule wa stakabadhi ghalani ulifikia shilingi 800, ambazo hakuna mkulima wa pamba Tanzania aliyepata.
Sasa huwezi kusema mfumo unaowapa Sh. 800/= ni mbaya unaowapa Sh. 500/= ndio mzuri. Mimi nadhani tuwaambie ukweli wakulima wa Tanzania, tusiwadanganye maana

Mzee Nyerere kabla hajafa alituambia ukikuta mtu mzima anadanganya watu wazima wenzake ana matatizo mawili, moja inawezekana ameanza kupata matatizo huku juu, lakini pili inawezekana anawadharau wale anaowadanganya. Mimi siamini kama Mheshimiwa Cheyo ana sifa zote hizo, kwa hiyo, mimi nadhani ilikuwa ni *oversight. (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*
*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Mbolea wa Mwaka 2008 *(The Fertilizer Bill, 2008)*

**MWENYEKITI:** Maana ya Kamati ya Bunge Zima ni kwamba tunaupitia sasa Muswada kifungu kwa kifungu hasa taarifa hii kwa wale wageni.

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Samahani Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Kwenye kifungu cha tano eeh!!!!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Nilikuwa tu nashangaa kidogo wakati tunaendelea kwa sababu imesomwa kifungu cha tatu, *clause* ya tatu inasema kwamba tumeipitisha, lakini kwenye *amendment* inaonekana imefutwa pia.

**MWENYEKITI:** Ya tatu eeh, ni kweli kimefutwa? Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ibara ya 3, 4, 5, na 6 vyote vimefutwa. Ibara ya 7 ambayo inakuwa kifungu cha tatu kipya

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu ambao niliupeleka kwa Mheshimiwa Waziri nilitaka tu kuweka maelezo sawa, ni kwamba katika maandishi yote kuna alama ambazo zinatumika *fullstop, comma, semi colon, colon, apostrophe, hyphen.* Sasa katika kifungu hiki cha saba, kifungu kile cha pili, kidogo nadhani mmekiona pale baada ya kusema: "*The authority established under subsection one shall be a Board Corporate and shall*" alama inayotakiwa pale ni *hyphen*, yaani *fullstop* mbili ambazo zinatazamana. Sasa ukiweka kale ka-mstari hakapo katika *dictionary* lolote lile au kwa msitari. Sasa nilikuwa naomba huko sehemu zote zile ziko sehemu nyingi niliwapa waziweke hizo badala ya hako ka-mstari ambako katika utungaji wa sheria kwa kweli hakaelezi. Maana yake hiyo inaonyesha orodha inayofuata ndio inayowekwa hivyo vi-doti viwili vi-*colon* sio *hyphen, colon* mbili hizo. Huu ni ufafanuzi nautoa kwa sababu Waziri aliukubali watakwenda kutengeneza huko. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante na tulipokea karatasi hii ya marekebisho hayo anayoyasema na tumeifikisha kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye sasa anataka kufafanua.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, uandishi wa sheria ni taaluma. Ile *dash* iliyowekwa pale ndiyo sahihi katika sheria hii na katika sheria zote zilizopitishwa na Bunge. Nasema hivyo kwa sababu gani? Kwa ujumla ile *full colon* na hii *hyphen* zinatumika kuunganisha au kufungua mahusiano yaani ya maelezo ya utangulizi yaani *opening words* au *umbrella words* na maneno yanayoainishwa katika aya zinazofuatia baada ya hapo katika mtiririko wa herufi za (a), (b), (c) au namba za kirumi ya (i), (ii),(iii) au ya (iv) na kadhalika *full colon* ambalo anaizungumzia Mheshimiwa Shellukindo inatumika pale tu ambapo maelezo ya utangulizi lugha yanafikishwa ujumbe uliokamilika lakini unatoa maelezo yanayoendana nayo yanaendelea kufafanuliwa katika aya zinazofuatia, yaani katika mtiririko ule wa (a),(b) au ya Kirumi (i),(ii), (iii) na (iv) *dash* au *hyphen* ambayo ndiyo iliyoko kwenye sheria hii inatumika pale ambapo maelezo ya utangulizi yanafikisha ujumbe ambao ili uweze kuleta maana kamili ni lazima usome na maelezo yanayofuatia ambayo yanaainishwa katika aya zinazofuatia, yaani *paragraph* kama (a) ,(b), (c) au ya Kirumi (i) ,(ii), (iii) ,(iv)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo maelezo ya matumizi ya neno hilo *dash* ambalo liko kwenye sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa William Shellukindo sasa.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Nilitaka tu kutoa maelezo kidogo, nimesoma kwenye *Oxford dictionary of current English*. Ndiyo! Kwa hiyo, haya natoa kama kuna mwongozo wa kisheria, basi tuupate sisi maana ndio tunaotunga sheria. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Katika mazingira haya kwa kawaida mwongozo wa kitaaluma unaongoza hatuwezi kufuata *Oxford English* inaweza kuwa ni ya kuzungumza, kwa hiyo, naukubali ufafanuzi wa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, ingawa namwona Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo aliyoyasema Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ni mamlaka aliyopewa Mwandishi Mkuu wa Sheria na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sura ya kwanza. Wabunge na wananchi wote ambao wangependa kupata tafsiri sahihi ya lugha inayotumika wangesoma kwa makini sana sura ya kwanza ya Sheria yaani *Interpretation clause.*

**MWENYEKITI:** Basi ni vyema nadhani tumeelewa kwamba aliyoyatoa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kuelezea namna ya vituo hivyo vinavyotumika ndivyo inavyotoka kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali na ndio tafsiri sahihi ya uandishi wa sheria zetu. Sasa inaweza kuonekana kwa sisi tuliosoma sarufi miaka ya 1960 na 1970 inaweza kuwa taabu lakini hatuna njia, inaweza kuwa inakera lakini hiyo ndiyo sheria kwa hiyo tunaendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8 sasa kinakuwa ibaru cha 4

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika aya hii ndipo kuna kazi ambazo zimeorodheshwa kwa ajili ya ile Mamlaka. Mojawapo ya hizo kazi ni kumshauri Waziri katika *technical issues*. Sasa nataka kukitumia kifungu hiki kumwuliza Mheshimiwa Waziri.

Najua Mheshimiwa Waziri alishanitaarifu tulipomaliza kikao kwamba atanitukana atakapokuja, kwa hiyo, nimekuja nimejiandaa kabisa kutukanwa. Lakini kwa nia njema kabisa hata akinitukana mimi nipo hapa kutetea wananchi wangu walionipeleka hapa. Mtu mkubwa akitanguliza matusi ujue kwamba amefilisika kihoja, kwa hiyo, tumemaliza. Sasa narudi kwenye *technical* issue. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Sasa na wewe unatukana?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ah! sijamtukana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye samadi. Nilipokuwa nazungumza natoa hoja hapa nilikuwa na hoja mbili. Ya kwanza nilikuwa nasema yule mnyama tunayemtegemea kutupatia samadi ni ng'ombe. Jibu nililokuwa nategemea hapa yeye akijua kwamba ng'ombe ndio plau, ndio kilimo, mavi ya ng'ombe ndio mbolea na hayana *importation* kwamba nimnong'oneze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, bwana acha huyu mnyama wangu usimhamishehamishe, usigombane nayo, ndio jibu ambalo nilikuwa nategemea lakini sikulipata, badala yake nimepata matusi.

La pili, pia nimesoma kilimo, nimejua wazi kabisa kwamba ukiongeza *urea* kwa samadi utapata mazao mengi zaidi, najua, ile haikuwa ndiyo ninayoizungumza. Kitu ambacho Mheshimiwa hajatueleza na tumeelezwa na watu wote hapa ardhi ukishaanza kuipatia mbolea ya kemikali ni lazima uendelee kutumia na unajenga usugu, ukiacha hupati mazao kabisa. Hii imesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wanatumia mbolea. Kwa hiyo, hoja yangu hapa ilikuwa imesema kwamba kama hatujawa na uhakika wa mbolea hiyo ya kemikali, basi tusiwahamasishe watu kuendelea katika njia hiyo tuwahamasishe watu zaidi kutumia samadi mpaka tutakapojenga uwezo wa kuwa na mbolea nyingi na hela nyingi za kuweza kuwapa watu wote.

Kwa hiyo, yeye amenifanya mimi sina akili, nimeambiwa kwamba sielewi mahesabu. Mimi nafikiri nina akili ya kutosha, ajibu hoja: Je, usugu huu ataufanyaje katika hali halisi ambayo iliyopo. La pili, Mheshimiwa ameniambia kwamba pamba haihusiani na hoja tuliyonayo. Pamba inahusiana kabisa na hoja tuliyonayo kwa sababu ukishazungumzia juu ya mbolea unazungumzia juu ya kuongeza gharama ya … (Hapa kengele ililia)

**MWENYEKITI:** Bahati mbaya uzingatie kwenye kanuni ni dakika 5 tu katika kuchangia hii.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kwa hiyo, naomba nihitimishe.

**MWENYEKITI:** Ndiyo zimeisha, hivyo ulizitumia mwanzoni kwa malumbano sasa.

**MHE. JOHN M. CHEYO**: *No problem.*

**MWENYEKITI:** Hukwenda kwenye samadi, ng'ombe na kadhalika, *point* zako nzito umezileta mwisho bahati mbaya Mheshimiwa Cheyo. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo hasa hili suala la usugu na wewe usijibu mapigo, hapana.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Hapana, nitajibu mapigo kwa mbolea tu na usugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala tunalozungumza hapa ni suala la uchumi, unaweka samadi na unakubali kwamba ukitumia mbolea ya kemikali hasa *urea* unaongeza uzalishaji, sasa hapa sio kwamba ukiweka ile unaongeza gharama tu, lakini unawekeza. Kama unaweka mfumo mmoja ambao unagharimu kama Sh. 40,000/= katika ekari moja halafu unatoa uzalishaji wako toka eka moja kilo 300 mpaka Sh. 1,000/= au Sh. 1,200/= mimi nadhani pale hujaongeza gharama isipokuwa umewekeza ukapata faida, hili ndilo tunalolizungumza wala halina ugomvi hata kidogo ni suala la kuwekeza tu na nadhani kwa hili tunakubaliana na Mheshimiwa Cheyo naye anakubali ukiweka *urea* unapata zaidi. Kwa hiyo, ni mahesabu ukiweka *urea* ya bei ghali unapata faida zaidi ya shilingi ngapi?

**MWENYEKITI:** Bado la usugu sasa. Ule udongo ardhi inakuwaje katika kipindi cha muda mrefu? Hilo ndilo lijibiwe.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeshalijibu hilo swali, alilijibu Naibu Waziri wakati anaeleza kwamba matumizi ya mbolea yoyote ile ukiyatumia vizuri haiharibu udongo, ukitumia vibaya hata dawa tu ukiitumia vibaya unapata madhara, kwa hiyo ukweli ndio huo. Lakini kwa sababu kilimo cha zao lolote kitakuwa kinaendelea na tunakubaliana kwamba ukitumia samadi, ukiweka mwaka mmoja unaweza usiweke mwaka wa pili, lakini ile *urea* unaweza ukaweka mfuko mmoja mmoja kwa eka kila mwaka kwa sababu ndiyo inakuwa kazi yako na inakupa mapato. Lakini uweke kwa kuzingatia kanuni ili usije ukaharibu ubora wa ardhi.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hajanijibu. Mimi nasema hivi, kwa hali halisi ya Taifa letu haizungumzii mkulima mmoja mmoja, nafikiri wengi kwa hali halisi ya nchi yetu kama tusipokuwa na fedha ya kutosha na mwaka huu tukaleta mbolea halafu mwaka kesho hakuna mbolea na ukishaanza kutumia mbolea ni lazima uendelee tutakuwa hatuwasaidii wakulima, hiyo ndiyo hoja yangu ambayo yeye anasema ukitumia vibaya kutumia *no,* ebu i-*link* hii na hali halisi ya uchumi wetu na hali halisi ya fedha tulizonazo katika bajeti yetu hiyo ndiyo ambayo ninayotaka. Sio mbaya mbaya na kadhalika.

**MWENYEKITI:** Tatizo hapa nadhani tunaweza tukaendelea muda mrefu bure ni suala la mtazamo. Serikali ina mtazamo ulio chanya *(positive)*, Mheshimiwa John Momose Cheyo ana mtazamo Kiingereza wanaweza kusema *pessimistic negative* kwamba nchi hii itashindwa tu kumudu kununua mbolea za kutosha au kutengeneza za kutosha. Hasa hayo ni maoni tu, hatuwezi kufikia uamuzi hapa. Kwa hiyo, sidhani kama kuna jibu ni suala la mtazamo unaweza kusema mimi ninavyoona Serikali haiwezi. Huku upande wa Serikali wanasema tunafanya jitihada ili hayo yawezekane, sasa unafikia wapi? Tumalize kwa kupitisha kifungu hicho ili kuiachia Serikali ifanye kazi yake.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

Ibara ya 6

*(Ibara z ilivyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 7

Ibara ya 8

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 10

Ibara ya 11

Ibara ya 12

Ibara ya 13

(*Ibara ilivyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15

Ibara ya 16

Ibara ya 17

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa John Cheyo amechoka kabisa anaondoka. Demokrasia ni kusikiliza mambo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kujibu takriban zote za Upinzani pamoja anasema ni hoja rahisi.

Kifungu cha 21 ambacho kinahusu *importation*, nadhani ndicho hicho baada ya marekebisho. Tulipendekeza kuwa katika kifungu hiki tunasema Serikali inaagiza mbolea kwa wingi sana, lakini mbolea ile inabaki bandarini kwa muda mrefu. Kwa hiyo, kwanza inaongeza gharama ile *gross period* ya *seven days* na gharama ile inakwenda moja kwa moja mpaka kwa mkulima. Maana ukiongeza gharama ya Pwani itamuathiri mlaji mkulima.

Lakini vile vile inapoteza *quality* tunasema ina-*expire* kama muda ni mrefu naona kweli unakuwa mrefu. Sasa tukasema hiki kifungu pamoja na juhudi zote ambazo zinafanywa na Wizara za Muswada huu au sheria hii mpya ya mbolea. Lakini kama hatukuweza kuondoa mbolea hii mapema, basi itakuwa hatujamsaidia mkulima kwa sababu bei ya mbolea kwa mkulima itapanda. Lakini Mheshimiwa Waziri alijibu kwamba hilo sisi halituhusu ni suala la vyombo vingine. Sasa nasema lazima pawe na *collective responsibility*. Hapa *issue* kubwa ni kupunguza gharama kwa ajili ya mkulima, lakini anasema Mheshimiwa Waziri hilo halituhusu, mimi nasikitika sana.

Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri labda atoe maelezo ya ziada watafanyaje ili hii mbolea ifike mapema kwa mkulima na bei iwe nafuu na *quality* ya mbolea ibakie pale pale. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Sikumsikia Waziri wala Naibu Waziri akisema haliwahusu, lakini pengine hii ndiyo nafasi nzuri ya kufafanua hilo na kuchelewa kwa mbolea lazima kuhusu Wizara ya Kilimo.

**WAZIRI WAKILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nadhani umenisaidia, sikusema hatuhusiki ila tulisema hili linahusiana na ufanisi wa bandari ambao unashughulikiwa na wenzetu wa Miundombinu. Hii ni kweli kabisa! Lakini anachosema Mheshimiwa Khamis ni kweli kwamba hata sasa huwa tunapata matatizo ya ucheleweshaji wa mbolea bandarini. Lakini tunafanya kazi kwa ushirikiano na bandari ili kuhakikisha kwamba inapofika kabla hata ufanisi wa bandari kwa ujumla haujakamilika, tunaiomba bandari iitoe ile mbolea kwa haraka zaidi ili kukwepa athari ya kupanda kwa bei, kwa hiyo, tunashirikiana namna ile.

Halafu vile vile kama nilivyosema watu wa *AR* tumewapa eneo ambalo watajenga *warehouse*. Kwa hiyo, ikija ile meli inaweza ika-*discharge* moja kwa moja kwenye *warehouse* yao ambayo inaweza ikapunguza ucheleweshaji wa meli ya mbolea bandarini. Lakini tunalitambua na tunajua ya kwamba ucheleweshaji ule una gharama. Tungependa kwa kweli kufanya kazi na wenzetu kuzipunguza gharama hizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 26

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27
Ibara ya 28

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 29

Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

Ibara ya 34

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 37

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 39

**MHE GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 39(k) neno la kwanza nadhani lilipaswa lisomeke "*tempers*" badala ya "*tampers*" linavyosomeka sasa hivi sijaliona kwenye marekebisho.

**MWENYEKITI:** Bado hatujafika.

Unachosoma wewe kiko ukurasa 28 bado tuko ukurasa wa 27. Tunakuja.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 40

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho cha 40(k) neno "*tampers*" nadhani lisomeke "*tempers*" kuliko inavyosomeka sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Hapana, sijui wewe unataka "*temper*" ile ya ghadhabu. Hii ndio sahihi mimi naona "*tampering".* Ni (a), *can you spell it*? Hebu tupe *spelling* unayotaka.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Kwa maana hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti nakubaliana na wewe.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 50
Ibara ya 51

*(Ibara zilizotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 52
Ibara ya 53

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1
Jedwali la 2

*(Majedwali yaliyotakwa hapo juu yalifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima umeupitia Muswada wa Sheria ya Mbolea wa mwaka 2008 (*The Fertilizer Bill, 2008)* ibara kwa ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mbolea wa Mwaka 2008 sasa ukubaliwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hujatoa hoja. Maneno matatu ya mwisho *"naomba kutoa hoja."*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu sasa umesomwa kwa mara ya tatu na kwa mujibu wa Kanuni zetu, sasa Muswada umeiva, umepitishwa na Bunge hili na utapelekwa katika taratibu za kawaida hadi tuweze kupata kibali cha Mheshimiwa Rais ili Sheria ikamilike. Nawatakia kheri Serikali katika utekelezaji ili Muswada huu muhimu sana uweze kuzaa matunda kwa kuinua kilimo katika nchi yetu. Ahsante sana.

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba nitoe maelezo yafuatayo kwamba maazimio yote mawili yanashabihiana. Kwa hiyo, nimeruhusu Mheshimiwa Waziri ayaelezee kwa pamoja na

hatimaye Mwenyekiti wa Kamati atafanya hivyo hivyo kwa kuyasoma maazimio yote mawili, Uongozi wa Kambi ya Upinzani hivyo hivyo, wachangiaji vilevile, ila nitakapowahoji nitawahoji kwa azimio kila moja peke yake, ndiyo utaratibu. Lakini naona kwa sababu yanafanana, basi tuweze kuyazingatia kwa utaratibu niliyoieleza.

Kabla sijamwita Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ambaye ndiye Mtoa Hoja, Waheshimiwa Wabunge naomba mtambue kuwepo kwa wageni mahususi kwenye *gallery,* wamealikwa na wenzetu Mheshimiwa Margaret Mkanga na Mheshimiwa Zulekha Haji. Sasa naomba wale wageni wetu kadiri nitakavyowatamka wale wenye uwezo wa kusimama waweze kusimama na wale ambao hawawezi kusimama kwa sababu zilizo dhahiri, basi wanaweza kutupungia mkono. Wapo Wawakilishi wa Vyama vya Wenye Ulemavu Idadi yao ni thelathini, naomba msimame na kupunga mikono. Ahsante sana, nawashukuru sana najua mmepata shida kwa wale mliotoka mbali kama Dar es Salaam na kwa hali yenu mmepata shida, lakini jambo hili ni muhimu, nashukuru sana uwepo wenu hapa.

Wapo Wawakilishi wa Walemavu wa Mkoa wa Dodoma, idadi yao ni 25 wale pale, ahsante sana. Wapo Wawakilishi wa Walemavu kutoka Zanzibar wako tisa, ahsante sana. Mmekuwa na safari ndefu kabisa kuvuka bahari hadi hapa, tunawashukuru sana uwepo wenu na tunaheshimu sana na tunawaenzi sana. Wapo Wawakilishi wa Walemavu kutoka Mkoa wa Tanga wapo kumi na wawili, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya utambulisho wa wadau hao muhimu, sasa namwita Mtoa Hoja Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

### Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Watu wenye ulemavu
### *(The Convention on the Right of the Persons with Disabilities)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Hoja ya Mazimio Mawili ya Bunge Kuhusu (1) Tanzania Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu wenye ulemavu, yaani *The Convention on the Rights of Persons with Disabilities* na azimio la pili, Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu wenye ulemavu, yaani "*The Optional Protocol to The Convention on The Rights of Persons with Disabilities"* kama ilivyoorodheshwa katika shughuli za leo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha hoja yangu, naomba kwanza nilishukuru Jukwaa la Uchechemuaji wa Masuala ya Ulemavu Nchini – *The Tanzania Forum for Disability Advocacy (TAFODA)* kutokana na maoni yao waliyoyatoa wakati nilipowasilisha Maazimio haya mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii Mjini Dar es Salaam tarehe 16 Aprili, 2009.

Mheshimiwa Spika, upitia Bunge lako Tufuku, napenda kulihakikishia jukwaa hili kuwa, maoni yote waliyoyatoa tumeyapokea na tutayafanyia kazi kwa kadri ya

uwezo wetu pindi Mikataba hii itakaporidhiwa na kuanza kufanya kazi hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niishukuru Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma za Jamii kwa kuyapitia mapendekezo ya Maazimio ya Kuridhia Mikataba hii miwili kwa kutoa Maoni na hatimaye kukubali kwamba Maazimio ya Kuridhia:-

(i) Mkataba wa kimataifa kuhusu Haki za Watu wenye ulemavu; na

(ii) Mkataba wa Nyongeza wa Kimataita Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu, yawasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuweza kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, watu wenye ulemavu ni miongoni mwa makundi katika jamii yenye uwezo mdogo wa kujimudu au kujitosheleza katika mahitaji muhimu kutokana na kuathirika kimwili au kiakili na mtizamo hasi wa jamii dhidi yao. Kulingana na takwimu za Umoja wa Mataifa, asilimia kumi ya watu hapa duniani wanaishi na ulemavu wa namna moja au nyingine. Hii ni sawa na watu nusu bilioni duniani ambao wanakadiriwa kuwa na ulemavu au kuathirika baadhi ya viungo au mifumo ya fahamu kutokana na sababu mbalimbali. Kwa mujibu wa sensa iliyofanyika hapa nchini mwaka 2008, idadi ya watu wenye ulemavu ni 2,547,362. Kati ya idadi hiyo, 1,242,650 ni wanaume na 1,304,713 ni wanawake.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwapo juhudi mbalimbali za Kimataifa za kuhamasisha jamii ili zijumuishe watu wenye ulemavu katika maisha ya kila siku na kuboresha maisha yao. Hata hivyo tathmini ya utekelezaji iliyofanywa na Umoja wa Mataifa ya Mwongo wa watu wenye ulemavu (1983 – 1992) ilibainisha kwamba, bado kuna unyanyapaa katika jamii nyingi na pia kuna vikwazo vinavyowazuia watu wenye ulemavu kutumia fursa zilizopo kujiletea maendeleo yao na ya Taifa kwa ujumla.

Tathmini hii ilikuwa ni chachu kwa Umoja wa Mataifa kuwezesha kuanza mchakato wa kuandaa Mkataba unaohusu Haki za Watu wenye ulemavu *(The Convention on the Rights of Persons with Disabilities).* Sanjari na hilo, nchi wanachama pia ziliandaa na kupitisha Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Watu wenye ulemavu *(The Optional Protocol to the Convention on the Rights of Persons with Disabilities*). Katika mchakato wote huo, Tanzania ilishiriki kwa ukamilifu kupitia Ubalozi wetu *New York*, Idara ya Ustawi wa Jamii chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na vile vile wawakilishi wa vyama vya watu wenye ulemavu. Mikataba yote hii ilipitishwa na Baraza la Umoja wa Mataifa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Mkataba wa Haki za Watu wenye ulemavu pamoja na Mkataba wa nyongeza, unatokana na kwamba mbali na Mikataba mbalimbali ya kimataifa iliyopitishwa Kuhusu Haki za Binadamu na Kuzuia Ubaguzi, ni Mkataba wa Haki za Mtoto tu ndiyo unaotambua suala la watu wenye ulemavu. Hivyo, Mkataba huu kuhusu Haki za Watu wenye ulemavu na ule wa Nyongeza ni wa kwanza katika karne hii

ya 21 ambayo iko mahususi kwa ajili ya watu wenye ulemavu ambapo nchi mbalimbali zitatakiwa kuchukua hatua mahsusi kwa lengo la kuhakikisha kuwa, haki za watu wenye ulemavu zinazingatiwa ipasavyo. Hatua ya Umoja wa Mataifa kupitisha Mikataba hii ni ya Kisheria katika kutambua nafasi ya watu wenye ulemavu katika Jamii, nchi husika na Ulimwengu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye ulemavu ya mwaka 2004 inashabihiana na vipengele vya Mikataba hii. Vilevile, ibara za 11 na 13 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazungumzia umuhimu wa Nchi kuweka taratibu ambazo zitawezesha makundi mbalimbali wakiwemo watu wenye ulemavu, kwenye masuala ya haki ya kufanya kazi, kupata elimu ya kujitegemea, kutobaguliwa kutokana na hali ya mtu na kutoa fursa sawa ya kupata elimu na elimu ya ufundi kwa watu wote. Aidha, Ibara ya 23 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, 2005 inasisitiza umuhimu wa Serikali kuweka misingi na taratibu zinazoleta maendeleo na maisha bora kwa watu wenye ulemavu. Kwa kuridhia, Mikataba hii tutakuwa pia tunatekeleza azma ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yake katika kuwahudumia Watu wenye ulemavu hapa nchini

Mheshimiwa Spika, hatua ambazo Serikali ya Tanzania imezichukua. Baada ya Mikataba hii kupitishwa na Baraza la Umoja wa Mataifa, nchi wanachama zilipewa muda wa kuweka saini katika Mikataba hii. Kwa upande wa Tanzania, Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za watu wenye ulemavu ulisainiwa na Valois wetu wa Kudumu wa Umoja wa Mataifa Mheshimiwa Agustine Mahiga tarehe 30 Machi, 2007. Aidha, Mkataba wa Nyongeza ulisainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 29 Septemba 2008. Hii inadhihirisha nia ya Tanzania katika kukubali na hatimaye kutekeleza vipengele vya Mikataba hii na vilevile Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano na wadau, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kuandaa mapendekezo ya kuridhira Mikataba hii, ilishirikisha wadau mbali mbali ambao walitoa maoni yao. Wadau walioshirikishwa ni pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Vyama vya Watu wenye ulemavu, Asasi Zisizo za Kiserikali *(AZISE)* na Sekta Binafsi. Wadau wote waliafiki pendekezo la kuridhia Mikataba hii kwani itakuwa na manufaa makubwa kwa nchi na kundi maalumu la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mikataba hii kutakuwa na gharama ambazo zitahitajika katika kuitekeleza. Fedha hizo zitahitajika kwa ajili ya kutafsiri na kusambaza mikataba, kuhudhuria mikutano husika, kutoa Elimu kwa Umma, na Fedha hizo zitatengwa katika bajeti ya kila mwaka ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu. Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za watu wenye ulemavu una jumla ya

Ibara 50. Ibara hizo zimeainisha masuala mbalimbali yanayohusu Haki za watu wenye ulemavu. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na:-

(i) Masuala ya Ujumla ambapo Nchi wanachama zitatakiwa kuchukua hatua za kiutawala na za kisheria kuhakikisha kuwa Haki Stahiki za watu wenye ulemavu zinatekelezwa;

(ii) Uhuru wa Kujieleza, kutoa Maoni na kupata taarifa mbalimbali;

(iii) Haki ya Kuishi na Kupata Huduma muhimu kama Elimu na Afya;

(iv) Usawa wa Kutobaguliwa wanawake na watoto wenye ulemavu;

(v) Uhuru na Ulinzi kwa watu wenye ulemavu;

(vi) Umuhimu wa Kuhakikisha ujongeaji *(accessibility)* na nyenzo za kujimudu;

(vii) Uhamasishaji kwa jamii kuhusu haki za watu wenye ulemavu;

(viii) Haki ya kufanya kazi na kupata ajira;

(ix) Kulinda utu wa watu wenye ulemavu;

(x) Utekelezaji wa kitaifa na tathmini; na

(xi) Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyobainisha hapo awali, vipengele vya Mkataba huu vinashabihiana na maudhui yaliyomo kwenye Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma Kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004 pamoja na baadhi ya Ibara za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa nyongeza wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu. Baada ya kupitisha Mkataba huu wa Kimataifa, Umoja wa Maifa uliunda Kamati ya kutatibu utekelezaji wa Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu.

Kazi ya Kamati hii ni kupokea na kujadili malalamiko kutoka kwa au kwa niaba ya watu au makundi ya watu ambao wanatuhumu kuwa ni waathirika wa uvunjaji wa Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu uliofanywa au unaoendelea kufanywa na nchi iliyoridhia Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu.

Mkataba huu wa nyongeza una jumla ya Ibara 18. Maeneo Muhimu ya Mkataba huu wa Nyongeza ni pamoja na:-

(i) Nchi kutambua mamlaka na uwezo wa Kamati ya Kimataifa Kuhusu Utoaji wa Haki za Watu wenye ulemavu;

(ii) Nchi kutambua nafasi ya Kamati ya Kimataifa kuhusu utoaji wa Haki za Watu wenye ulemavu pamoja na kanuni za kujiendesha;

(iii) Serikali kutoa haki kwa mtu au watu au taasisi inayotoa malalamiko au ukiukwaji wa haki za watu wenye ulemavu; na

(iv) Serikali kutoa ushirikiano endapo itabidi malalamiko dhidi yake kuchunguzwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa Kuridhia Mikataba hii. Mikataba yote miwili inaeleza bayana kwamba Mikataba hiyo itatakiwa kuridhiwa na nchi wanachama. Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu utaridhiwa kwa kuzingatia ibara za 42 na 43 za Mkataba.

Aidha, Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu utaridhiwa kwa kuzingatia ibara za 10 na11 ya Mkataba wenyewe. Vilevile, ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalitaka Bunge letu kuridhia Mikataba ya Kimataifa ambayo masharti yake yanahitaji kuridhiwa. Hivyo, Maazimio haya ya Bunge yanalenga kutekeleza matakwa haya ya kisheria na kikatiba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, kwa kuwa faida za kuridhia Maazimio haya ni kubwa, na hasa kuwa chachu kwa Serikali na Nchi kwa ujumla katika kuhakikisha kuwa tunatekeleza na kusimamia kikamilifu Haki za Watu Wenye Ulemavu nchini, hivyo, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge watafakari na kukubali mapendekezo haya ya Kuridhia (1) Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu; na (2) Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kusoma Maazimio hayo Ulemavu:-

Azimio la kwanza ni:-

**AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA MKATABA WA KIMATAIFA KUHUSU HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU (*CONVENTION ON THE RIGHTS OF PERSONS WITH DISABILITIES)***

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) ambao ulianzishwa mwaka 1945 na Tanzania kujiunga mwaka 1961;

NA KWA KUWA nchi wanachama zimekuwa zikishirikiana katika kupanga mikakati ya kuboresha maisha ya Watu wenye ulemavu, kulinda haki zao ikiwa ni pamoja na kupambana na ubaguzi na vitendo vya kikatili dhidi yao;

NA KWA KUWA Umoja wa Mataifa ulifanya tathmini ya Muongo wa Kimataifa wa Watu wenye ulemavu (1983 – 1992) na kubaini kwamba licha ya juhudi za kimataifa za kuhamasisha jamii zijumuishe Watu wenye ulemavu katika maisha ya kila siku ili kuboresha maisha yao, bado kuna ubaguzi, unyanyapaa na vitendo vya kikatili dhidi yao vinavyowazuia Watu wenye ulemavu kutumia fursa zilizopo kujiletea maendeleo yao na ya Taifa kwa ujumla;

NA KWA KUWA Tanzania imekuwa ikishiriki katika kuendeleza malengo na madhumuni ya kuundwa kwa Umoja wa Mataifa (UN) pamoja na kushiriki kwa ukamilifu katika kuandaa mikataba mbalimbali ya umoja huo ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu wenye ulemavu hivyo kuhitaji kuuridhia;

NA KWA KUWA Mkataba huu unahusu Haki za Watu wenye ulemavu na unalenga katika kulinda na kuhakikisha kwamba Watu wenye ulemavu wanapata haki zote za msingi ikiwa ni pamoja na kuheshimu utu wao;

NA KWA KUWA Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu wenye ulemavu umepitishwa na Umoja wa Mataifa na unazitaka nchi wanachama kuweka mikakati madhubuti ya kulinda haki za Watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kutunga sheria mahsusi ya kulinda haki zao;

NA KWA KUWA Mkataba huu umejikita katika misingi ya Kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu Haki na Usawa wa Fursa kwa Watu Wenye Ulemavu zilizopitishwa mwaka 1993 na kukubaliwa na Serikali mwezi Desemba 2006;

NA KWA KUWA Mkataba huu unahusu usawa na kutobaguliwa kwa watu wenye ulemavu katika masuala ya ajira na kazi, haki ya kuishi na kupata huduma muhimu ikiwa ni pamoja na elimu, afya, kinga ya jamii, ujongeaji na nyenzo za kijimudu, kulinda utu wao, uhuru wa kujieleza, kutoa maoni na kupata taarifa mbalimbali, uhamasishaji wa jamii, ushirikiano wa Kimataifa na utekelezaji wa Kitaifa na tathmini;

NA KWA KUWA vipengele vya Mkataba huu vinashabihiana na vipengele vilivyopo kwenye Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 na havina athari yoyote kisiasa, kiuchumi, kimazingira na kiteknolojia;

NA KWA KUWA Serikali itawajibika kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mkataba huu katika kipindi cha miaka miwili baada ya kuuridhia na kila miaka minne baada ya hapo;

NA KWA KUWA Mkataba huu ulipitishwa rasmi na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika kikao chake cha 61 cha mwezi Februari, 2007 mjini *New York*, Marekani kupitia Azimio Na. 61/106;

NA KWA KUWA Kwa kuridhia Mkataba huu Serikali italazimika kugharimia kazi mbalimbali kama kutafsiri mkataba katika Kiswahili na kuusambaza, uhamasishaji

wadau na jamii na kuhudhuria vikao vinavyohusu masuala ya Watu Wenye Ulemavu vya nchi wanachama. Wizara itatenga fedha katika bajeti yake ya kila mwaka chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii katika kutekeleza kazi zilizotajwa pamoja na malengo ya Mkataba huu;

NA KWA KUWA Ibara ya 42 ya Mkataba inatoa nafasi kwa nchi wanachama kuweka saini na Tanzania kama nchi mwanachama iliweka saini katika Mkataba huo tarehe 30 Machi 2007, kama hatua ya kwanza kuelekea kuuridhia;

NA KWA KUWA Kwa kuuridhia Mkataba huu na kuutekeleza, Tanzania itanufaika na mambo yafuatayo:-

(a) Kulinda na kudumisha haki na usawa wa fursa kwa Watu wenye ulemavu;

(b) Kuwawezesha Watu wenye ulemavu kupata huduma muhimu katika jamii kama afya, elimu, vifaa vya kujimudu na ujongeaji;

(c) Kushiriki kwa ukamilifu katika kazi na ajira inayoendana na mahitaji ya soko katika kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu katika jamii;

(d) Kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa ubaguzi, unyanyapaa na vitendo vya kikatili dhidi ya watu wenye ulemavu;

(e) Kushirikiana na nchi wanachama na ubadilishana utaalam katika masuala yanayohusu utekelezaji wa malengo na madhumuni ya Mkataba huu;

(f) Kupata nafasi ya kushiriki katika Kamati ya Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu ambayo itasimamia utekelezaji wa Mkataba huu;

(g) Kuhuisha masuala ya Watu Wenye Ulemavu katika Wizara za Serikali na Taasisi zake; na

(h) Kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu kushiriki kwa ukamilifu katika nyanja za kisiasa na kiuchumi sawa na wasio na ulemavu.

HIVYO BASI, Kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Mkataba huu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wa 15 na kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuuridhia Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu wenye ulemavu, yaani *"The Convention on the Rights of Persons with Disabilities."(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nisome azimio la pili.

**AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA MKATABA WA NYONGEZA WA KIMATAIFA KUHUSU HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU *(OPTIONAL PROTOCOL TO THE***

***CONVENTION ON THE RIGHTSOF PERSONS WITH DISABILITIES)***

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa *(UN)* ambao ulianzishwa mwaka 1945 na Tanzania kujiunga mwaka 1961;

NA KWA KUWA Nchi wanachama zimekuwa zikishirikiana katika kupanga mikakati ya kuboresha maisha ya Watu Wenye Ulemavu, kulinda haki zao ikiwa ni pamoja na kupambana na ubaguzi na vitendo vya kikatili dhidi yao;

NA KWA KUWA Umoja wa Mataifa ulifanya tathmini ya Muongo wa Kimataifa wa Watu Wenye Ulemavu (1983 – 1992) na kubaini kwamba licha ya juhudi za kimataifa za kuhamasisha jamii zijumuishe Watu Wenye Ulemavu katika maisha ya kila siku ili kuboresha maisha yao, bado kuna ubaguzi, unyanyapaa na vitendo vya kikatili dhidi yao vinavyowazuia watu wenye ulemavu kutumia fursa zilizopo kujiletea maendeleo yao na ya Taifa kwa ujumla;

NA KWA KUWA Tanzania imekuwa ikishiriki katika kuendeleza malengo na madhumuni ya kuundwa kwa Umoja wa Mataifa (UN) pamoja na ushiriki kwa ukamilifu katika kuandaa mikataba mbalimbali ya umoja huo ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu wenye ulemavu hivyo kuhitaji kuuridhia;

NA KWA KUWA Mkataba huu unahusu Haki za Watu wenye ulemavu na unalenga katika kulinda na kuhakikisha kwamba Watu wenye ulemavu wanapata haki zote za msingi ikiwa ni pamoja na kuheshimu utu wao;

NA KWA KUWA katika utekelezaji wa Haki za Watu Wenye Ulemavu na kuwapa uhuru zaidi wa kudai haki hizo kisheria, Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye ulemavu ulipitishwa sambamba na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu;

NA KWA KUWA Mkataba huu umejikita katika misingi ya Kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu Haki na Usawa wa Fursa kwa Watu Wenye Ulemavu zilizopitishwa mwaka 1993 na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2005;

NA KWA KUWA katika kuhakikisha haki za watu wenye ulemavu zinalindwa, Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu unaruhusu mtu binafsi au vikundi vya watu au taasisi kufikisha malalamiko kwenye Kamati ya Kimataifa mara baada ya taratibu zote za kisheria za kupata haki katika nchi kushindikana;

NA KWA KUWA Mkataba huu unahusu usawa na kutobaguliwa kwa Watu wenye ulemavu katika masuala ya ajira na kazi, haki ya kuishi na kupata huduma muhimu ikiwa ni pamoja na elimu, afya, kinga ya jamii, ujongeaji na nyenzo za kujimudu, kulinda utu wao, uhuru wa kujieleza, kutoa maoni na kupata taarifa

mbalimbali, uhamasishaji wa jamii, ushirikiano wa Kimataifa na utekelezaji wa Kitaifa na tathmini;

NA KWA KUWA vipengele vya Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Watu Wenye Ulemavu vinashabihiana na vipengele vilivyopo kwenye Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye ulemavu ya mwaka 2004 na havina athari yoyote kisiasa, kiuchumi, kimazingira na kiteknolojia;

NA KWA KUWA Serikali itawajibika kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mkataba huu katika kipindi cha miaka miwili baada ya kuuridhia na kila miaka minne baada ya hapo;

NA KWA KUWA Mkataba huu ulipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika kikao cha 61 cha mwezi Februari, 2007 mjini *New York*, Marekani kupitia Azimio Na. 61/106;

NA KWA KUWA Ibara ya 10 ya Mkataba inatoa nafasi kwa nchi wanachama kuweka saini katika Mkataba huo na Tanzania kama nchi mwanachama iliweka saini katika Mkataba wa Nyongeza *(Optional Protocol)* tarehe 29 Septemba 2008, kama hatua ya kwanza kuelekea kuridhia Mkataba huo;

NA KWA KUWA kwa kuridhia Mkataba huu na kuutekeleza, Tanzania itanufaika na mambo yafuatayo:-

(a) Kudumisha demokrasia na kutoa uhuru na nafasi ya kuhoji utendaji wa Serikali katika kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu;

(b) Kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu;

(c) Kupata nafasi ya kushiriki katika Kamati ya Kimataifa kuhusu Haki za Watu wenye ulemavu ambayo itasimamia utekelezaji wa Mkataba huu;

(d) Kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa ubaguzi, unyanyapaa na vitendo vya kikatili dhidi ya watu wenye ulemavu hivyo kulinda utu wao;

(e) Kushirikiana na nchi wanachama na kubadilishana utaalam katika masuala yanayohusu utekelezaji wa malengo na madhumuni ya Mkataba huu;

(f) Kulinda na kudumisha uhuru kwa watu wenye ulemavu wa kujieleza, kutoa maoni, kupata taarifa mbalimbali na kuwasilisha malalamiko yao katika ngazi ya nchi na kimataifa;

(g) Kuhuisha masuala ya Watu wenye ulemavu katika Wizara za Serikali na Taasisi zake; na

(h) Kuwawezesha Watu wenye ulemavu kushiriki kwa ukamilifu katika nyanja za kisiasa na kiuchumi sawa na wasio na ulemavu.

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Mkataba huu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wa 15 na kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuuridhia Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu yaani *"The Optional Protocol to the Convention on the Rights of Persons with Disabilities"*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Huduma za Jamii ya Kudumu ya Bunge Azimio la Kuruidhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu pamoja na Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii inatambua kuwa miongoni mwa matatizo yanayowakabili watu wenye ulemavu ni unyanyapaa, ubaguzi, ukosefu wa mafunzo, ajira na vifaa vya kuwasaidia kama vile baiskeli za watu wenye ulemavu, vitabu kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa kuona, magongo ya kutembelea, viuongo bandia na miundombinu kwenye majengo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii ilipata fursa ya kusikiliza madhumuni ya Serikali kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye ulemavu na Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa kuhusu Haki za Watu wenye ulemavu uliowasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Prof. David Homel Mwakyusa - Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii siku ya tarehe 16 Aprili, 2009 Ofisi ya Bunge Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilijadili kwa kina yaliyomo katika Kauli hizo ambazo zilihusu zaidi kuboresha, Kulinda na kuhakikisha kwamba Watu wenye ulemavu wanafaidika na kupata haki zote za msingi ikiwa ni pamoja na kuheshimiwa utu wao.

Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya Azimio la Kuridhia Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu ni dhahiri kuwa yamelenga kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata haki sawa za msingi kama vile Elimu, Afya, Kinga ya Jamii, nyenzo za kujimudu, uhuru wa kujieleza, kutoa Maoni na kupata taarifa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii inaunga mkono Maazimio haya na kwamba vipengele muhimu vya Mkataba vimezingatiwa ikiwa ni pamoja na:-

(i) Usawa na kutobaguliwa wanawake na watoto wenye ulemavu;

(ii) Haki ya kuishi na kupata huduma muhimu kama vile Elimu na Afya;

(iii) Ajira;

(iv) Uhuru wa ulinzi kwa watu wenye ulemavu;

(v) Kulinda utu wa watu wenye ulemavu;

(vi) Ujongeaji/nyenzo za kujimudu;

(vii) Uhuru wa kujieleza, Kutoa maoni na kupata taarifa mbalimbali;

(viii) Uhamasishaji wa Jamii;

(ix) Ushirikiano wa Kimataifa; na

(x) Utekelezaji wa Kitaifa wa tathmini.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunaunga mkono kwa kuwa vipengele hivi vinashabihiana na vipengele vilivyopo katika Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaipongeza Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuweza kuwasilisha Maazimio haya yenye lengo la kuboresha, kulinda na kuhakikisha kwamba Watu wenye ulemavu wanafaidika na kupata haki zote za msingi.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu na Nyongeza yake itasaidia kuboresha maisha ya Watu Wenye Ulemavu na kuondoa vikwazo mbalimbali vinavyowakabili Walemavu hasa unyanyapaa. Hali hii itasaidia Watu wemue Ulemavu kutumia fursa zilizopo katika kuleta maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tumeona Jamii ya Watu Wenye Ulemavu haipewi nafasi au kipaumbele katika ajira, shule na huduma za Afya. Kuridhiwa kwa maazimio haya, kutasaidia Watu Wenye Ulemavu kupata huduma muhimu za kijamii bila kubaguliwa.

Mheshimiwa Spika, Kuridhiwa kwa Maazimio haya itakuwa ni hatua muhimu kwa Serikali kuandaa mkakati wa uwasilishwaji wa Muswada wa Sheria ya Watu Wenye

Ulemavu ambayo itasimamia mambo yote ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ambayo yanahusu watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kuridhia na kutekeleza Maazimio ya mikataba hii kutasaidia kupunguza na hatimaye kuondoa vitendo vya ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu ikiwemo kuuawa ambavyo vimekuwa vikiambatana na mila potofu hasa kwenye jamii mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Mikataba hii itasaidia kuelimisha na kutoa uelewa kwa jamii nzima kuhusu umuhimu wa kuhusisha watu wenye ulemavu katika kuleta maendeleo ya Taifa hili. Pia itadumisha haki, usawa na uhuru wa Watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa mara baada ya Bunge kuridhia Maazimio haya ni muhimu ikabiliane na changamoto zifuatazo mapema iwezekanavyo:-

(i) Kutunga Sheria inayohusu watu wenye ulemavu;

(ii) Kuweka mikakati na kuhimiza sekta binafsi, Asasi na Mashirika ya kidini kuwekeza katika utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kwa Watu wenye ulemavu;

(iii) Kuongeza ubunifu wa Stadi na upatikanaji wa fursa kwa watu wenye ulemavu; na

(iv) Kuanzisha hatua na mikakati ya usalama wa kijamii kwa watu wenye ulemavu na wale wanaoshughulikia matatizo ya Watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha Maoni na Ushauri, sasa napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia Maoni na Ushauri wa Azimio hili ni kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' – Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhil, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mheshimiwa Fatma Abdullah Tamim, Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale na mimi mwenyewe Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji – Makamu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashilillah kwa kuiwezesha Kamati katika kutekeleza majukumu yake, pamoja na Katibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John, kwa kuhudumia Kamati hii wakati wote.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Naibu Waziri wa Afrya - Mheshimiwa Dr.

Aisha O. Kigoda, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndugu Blandina Nyoni na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kuandaa na kuboresha Maazimio haya. Vile vile navishukuru Vyama na Vikundi vyote vya watu wenye ulemavu kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni kuhusu kuridhiwa kwa Mkataba wa Haki za Watu Wenye Wlemavu.

Mheshimiwa Spika, Shukrani za pekee ziwaendee Mtandao wa Jukwaa la Uchechemuaji wa Masuala ya Ulemavu Nchini *(Tanzania Forum for Disability Advocacy – TAFODA)* kwa kuwasilisha maoni yao mbele ya Kamati. Tunawahakikishia ushirikiano wetu katika kupambana na changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu pamoja na Nyongeza yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii. Baada ya kusikia kutoka kwenye Kamati husika kama inavyohitajika kwa mujibu wa kanuni zetu, sasa tusikie kutoka Kambi ya Upinzani.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI (MSEMAJI WA UPINZANI WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII):** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu pamoja na Itifaki yake ya nyongeza *(The Convention on the Rights of Persons with Disabilities and with its Optional Protocol*, kwa mujibu wa kanuni za Bunge, kanuni ya 86(6) toleo la mwaka 2007. Nianze kwa kuunga mkono hoja! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu pamoja na nyongeza yake vinalenga kuongeza usawa na kutokubaguliwa watu wenye ulemavu katika masuala mbalimbali kuanzia sekta ya ajira, elimu, afya na kupata uhakika wa kinga ya kudhuriwa utu wao. Vilevile kulindwa kwa uhuru wao wa kujieleza, kutoa maoni na kupata taarifa mbalimbali kama watu wengine wanavyopata.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haina pingamizi kwa Bunge hili kuridhia Mkataba ulioletwa na Mheshimiwa Waziri ili kupata ridhaa ya Bunge hili. Kama ambavyo kauli mbiu yetu siku zote kuwa Demokrasia ya kweli ndio suluhisho pekee katika kuhakikisha kuwa fursa sawa kwa wanajamii wote inafikiwa na kwa mantiki hiyo na wale wote wenye ulemavu wa aina yeyote nao watapa kile ambacho ni stahiki kwa kila mwanajamii bila ya upendeleo wa ubaguzi wa aina yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo Kambi ingependa kuweka msisitizo ni kwamba nchi yetu kweli iwe imejiandaa kutekeleza ibara zote kama mkataba unavyotaka. Vinginevyo itakuwa tunawahadaa walengwa wakuu wa mkataba huu, kwa maana nyingine Serikali itengeneze *action programme* ya kutekeleza mkataba huu wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naunga mkono hoja hizi za Mheshimiwa Waziri. Nashukuru sana kwa kunisikiliza. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali kwa maoni ambayo mmewasilisha kwa ufupi kwa sababu hili si jambo ambalo tunaweza kuwa na upinzani wowote dhidi yake.

Waheshimiwa Wabunge, ninao walioomba kuchangia Wabunge saba. Kwa kuzingatia ratiba, nitawasihi sana waweze kuzungumza kwa ufupi, kesho tuna Muswada wa Bima. Jambo hili ni kubwa, kwa hiyo nitatoa fursa wafuatao waweze kupata nafasi: Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Riziki Lulida. Hao ndio muhimu sana hao kwa kuchangia hili. Hawa wengine kesho hawa:- Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Prof. Idriss Mtulia na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, inategemea muda utakaotumika kwa wale wanne wa kwanza. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Margreth Mkanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu kwetu na tuliyoisubiri kwa siku nyingi. Mwanzo, nianze na kuipongeza Wizara, nikianzia na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kuandaa sawa sawa Maazimio haya yote mawili. Kwa kweli yamesomeka bila matatizo na yameeleweka, pamoja na kwamba Maazimio yenyewe *book* lake ni kubwa, lakini ule ufafanuzi uliotolewa na ile *summary*, kwa kweli ni nzuri sana, tunawashukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza tu niseme ukweli kuonyesha furaha niliyo nayo na furaha hii siyo yangu peke yangu, nadhani ni kwa niaba ya wenzetu wenye ulemavu nchini na inajionyesha jinsi walivyojitahidi kuhudhuria kwa wingi kwa uwezo wao, tena kwa ghafla, kwa sababu ratiba hii ilikuwa kesho, lakini asubuhi tukakuta *Order Paper* imebadilika, lakini tukawasiliana, tunashukuru mitandao, haraka haraka, Dar es Salaam, Dodoma, Tanga na kwingineko. Kwa kweli hiyo yote ni kuonyesha jinsi tulivyothamini suala hili na ambavyo tumefurahi kwamba leo Serikali imeweza kutuletea mikononi mwetu tuweze kujadili na ninaamini Bunge wala halina wasiwasi, Mkataba huu utaridhiwa kwa sababu ni muhimu sana. Kama sio muhimu kwa wewe leo, lakini kumbuka kwa kesho Mkataba huu unaweza ukawa muhimu sana kwako kwa sababu hujui nini kitaendelea.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchache wa fadhila na shukrani nisipotambua mchango mkubwa uliotolewa na Vyama vya Watu Wenye Ulemavu nchini katika maandalizi ya Mchakato wa Mkataba huu na hapa siendi mbali, namkumbuka sana Mheshimiwa Marehemu Malim Khalfan toka Umoja wa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar na yeye ndiye alikuwa Mkurugenzi wa Chama cha Umoja wa Walemavu huko Zanzibar. Mungu amuweke pema mahali pazuri, kwa sababu ni kama wiki tatu ametutoka katika macho yetu. Lakini mchango wake, sio Tanzania tu, mtu huyu alikuwa ni *figure* ya kidunia kwa masuala ya Watu Wenye Ulemavu, Mwanaharakati hasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwingine ambaye alituwakilisha huko katika harakati hizi na vikao mbalimbali alikuwa ndugu Gideon Mandes, bahati nzuri yuko hapo juu. Yeye ni Mwanaharakati mkubwa, aliungana na Serikali mbalimbali huko *New York* kuhakikisha kwamba Mikataba hii miwili inaundwa na leo inafika hapa ilipotufikia. Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, siwezi kukusahau, mwaka 2006 uliweza kugharamia safari ya Wabunge watatu wenye uelemavu humu ndani kwenda kushuhudia mchakato huu ulipokuwa unamalizika kutengenezwa kwa mkataba huu. Siwasemei, lakini mimi lile niliona kwamba uko pamoja nasi kuweza kufanya yale uliyoweza kuyafanya na wenzetu walikwenda kutuwakilisha. Tunakushukuru sana! *(Makofi)*

**SPIKA:** Tena mlikwenda mbali, mlikwenda *New York*, siyo hapa!

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, eeh, naam *New York* - Marekani kwa wiki mbili na uligharamia safari hiyo. Kingine, napenda kuwashukuru viongozi na wanachama wa Vyama vyote vya Watu Wenye Ulemavu nchini na Taasisi na Asasi mbalimbali zinazohudumia watu wenye ulemavu kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wanatupatia sisi wawakilishi wao humu Bungeni kuweza kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali yanayowahusu kama hivi mnavyoona leo, wametuunga mkono kuja kusikiliza, huu ni ushirkiano. Ingekuwa tuko shaghalabaghala, wala wasingehangaika kuja.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizi, naomba tu nichangie machache kwa sababu, kwanza muda ndio huo, lakini mikataba yote miwili yenyewe hii imekaa vizuri mno, imeeleweka. Kwa hiyo, moja kwa moja naunga mkono. Kwanza, kwa sababu ni kitu ambacho kimesubiriwa muda mrefu sana na umuhimu wake unafahamika sana, kwa hiyo, wala hakuna haja ya kupindapinda na kubabaika babaika.

Mheshimiwa Spika, kilichonifariji sana katika mikataba hii miwili yote ukijumuisha, ni kwamba tumekumbushwa katika ibara mbalimbali Serikali na Jamii ulazima wa ushiriki wa watu wenye ulemavu katika kuandaa na kutekeleza sheria na sera mbalimbali zinazohusu nchi husika katika maeneo mbalimbali. Hii imedhihirisha kwamba, kuna usemi sisi watu wenye ulemavu tunaoutumia kwamba “bila sisi wenyewe kuwepo hakiwezi kufanyika kitu” Kwa Wazungu wenyewe wanasema *“nothing about us without ourselves”*.

Kwa hiyo, hilo tumekumbushwa na nashukuru katika nchi yetu hii, kabla hata ya mkataba huu au mikataba hii hatujaipitia kutokana na Katiba yetu na hali halisi ya maisha yanavyokwenda sasa hivi, kwa upande fulani, ushiriki wa watu wenye ulemavu umeanza kushika kasi. Ombi langu ni kwamba mkataba huu unaendeleza hilo na kusisitiza kwamba ushiriki lazima uwepo kwamba tushirikishwe katika kila hali kama ambavyo imeanza kufanyika hivyo.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa pia kwa sababu mkataba huu umejaribu kusisitiza kwamba nchi husika mwanachama zitakaposaini, ziendelee kufanya utafiti wa

teknolojia muafaka na rahisi ambao zitaweza kutumika vizuri na watu wenye ulemavu; haya yanajitokeza kwenye ibara ya nne sehemu ya kwanza ya mkataba huu.

Katika hili, naomba tu kukumbusha kwamba, kama tulivyoanza kuwa na kasi nzuri katika mengine hayo niliyoyazungumzia hapo juu, naomba hili la kurahisisha bei za teknolojia mbalimbali, vifaa mbalimbali kwa watu wenye ulemavu na huduma za afya, kweli ziwe zile ambazo watu wengi wanaweza kumudu kwa sababu mpaka sasa hivi watu wenye ulemavu wengi wanashindwa kumudu huduma hizi, sio vifaa, sio mahospitalini. Kwa hiyo, hilo tuongeze kasi na ninaamini kwamba kasi hiyo itapatikana baada ya mkataba huu na mengineyo kuweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, hapo nimefurahi, kwamba lazima pawe na mpango mahsusi wa makusudi sana kuandaa watalaam ambao kweli watasaidia katika utekelezaji wa mkataba huu. Mpaka sasa hivi nchini hatuna Maafisa Ustawi wengi hata kidogo. Ninaloomba wawe wengi, waandaliwe wengi, wafike hata kwenye ngazi za Kata kwa sababu kule kwenye Kata ndiko walemavu waliko. Sasa hivi utakuta Mkoani tu, Wilayani wako wachache, Halmashauri wala hazina hawa watu, ni matatizo matupu. Ninaomba watalaam wa viungo na mazoezi tunaowaita akina Mama Cheza wawepo katika hospitali zetu hata zahanati kwa sababu ulemavu fulani unaweza ukazuiliwa taaluma hizi zikitumika. Wao wanajua, wanaweza kumtibutibu mtu kwa kunyoosha viungo tu, mtu akapata nafuu kuliko akapata ulemavu mwingine.

Mheshimiwa Spika, watalaam wengine ambao ni muhimu sana kuandaliwa kwa wingi ni watalaam wa lugha ya alama, kwa sababu hawa kwa upande wa wenzetu wenye ulemavu, viziwi, kwa kweli inakuwa ni matatizo. Mnaona pale yanayofanyika, yuko mmoja yule, tangu saa hizo peke yake. Kwa kawaida anapaswa kusaini kwa dakika 30 halafu apokelewe na mwingine, lakini sasa atapokelewa na nani pale? Ili wale wenzetu waweze kuelewa, ni huyo huyo peke yake kwa masaa. Kwa hiyo, kwa kweli kuna umuhimu na mikataba hii imeshauri na kusisitiza kwamba pawe na maandalizi ya watalaam ambao watamudu kuhudumia watu wenye ulemavu na haya yako katika ibara ya nne. Ninaamini Serikali yetu itaweza kutekeleza hayo.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa na mkataba huu na yote yaliyosemwa na Kamati nayaunga mkono kwa upande wa ujongeaji *(accessability)*. Jamani ni tatizo, jamani ni tatizo kwa nchi hii. Hapa ninadhani lazima sheria nyingine pia ziangaliwe upya ili kuweza kukidhi haja ya mambo haya:- majengo yetu, barabara zetu, njia za usafiri zetu, sehemu za matibabu, sehemu za kuabudu, sehemu za mahakama ambazo ndipo haki inapatikana, mawasiliano ya aina gani, visaidizi gani vitapatikana, haya yote yanapaswa kuangaliwa kwa undani kuanzia sasa na hizo fedha ambazo ninaamini zitatengwa wakati wa bajeti ya mwaka huu, nadhani kuanzia bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, suala la haki ya kuishi limesisitizwa humu kwamba ni muhimu kwa raia wote. Tunafahamu hapa nchini dhahama tuliyonayo ya wenzetu Albino kuuwawa hovyo hovyo kikatili. Ninaamini kwa mikataba hii kuweza kuiridhiwa leo na sheria inayokuja, itakazia kikamilifu mambo haya ili mauaji haya yaweze kukomeshwa.

Hapa naiomba Serikali na wote wanaohusika kushirikisha kikamilifu Albino wenyewe katika harakati za kukomesha mauaji haya hapa nchini, kwa sababu mwenye chake anaelewa. Kwa hiyo, washirikishwe kikamilifu kabisa katika mchakato mzima wa kuondoa tatizo hili tulilonalo.

Mheshimiwa Spika, muda ndio huo unakwenda, niwaachie wenzangu. Lakini nimefurahi sana na mkataba wa nyongeza uliotoa uhuru wa watu kuweza kulalamika kimataifa huko kwamba tunaonewa hivi na hivi, ni uhuru. Ninaloomba tu, sisi ambao tumepewa uhuru huo, tuutumie uhuru huo vizuri, kwamba tufuate zile taratibu za humu ndani, pindi zitakaposhindikana, ndiyo tupandishe bendera kupeleka mbele ya safari kwamba aah, tumeonewa. Tusikurupuke tu kwamba umeonewa leo, kesho kwa sababu mkataba umesema, haya tunakwenda kimataifa, kwa nchi yetu tena ninaamini hilo wala halitaweza kufikiwa kwa sababu tuna taratibu zetu, tuna mambo yetu ambayo yanaweza yakatukumbusha.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na Mheshimiwa Waziri kutuhakikishia kwamba rasilimali za kutosha zitatengwa ili utekelezaji wa mkataba huu na mengineyo yaweze kufanyika. Mheshimiwa Spika, ninalolisisitiza ili mkataba huu uweze kuwa na maana na utekelezeke, naungana na maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii, sheria ile ambayo mchakato wake ulikwishaanza, ikamilishwe haraka ili ikiwezekana Oktoba, jamani tulipitishe suala hili, mambo ya walemavu sasa yaweze kukaa sawa sawa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono tena hoja hii na kwamba nimeendelea kufurahishwa na kupata faraja kwangu mimi binafsi kwamba mpango wangu wa kazi wa uwakilishi ndani ya Bunge, niseme kweli, unakwenda vizuri. Nilianza kuhangaika na sera, sera tayari. Tumeendelea kuhangaika na mkataba huu, leo tayari, imebaki sheria tu.

Kwa hiyo, hiyo ni hatua fupi tu iliyobaki kwa sababu tulikotoka ni mbali zaidi. Baada ya kusema haya, kwa niaba ya wenzangu wenye ulemavu, kwa kweli tumefurahishwa sana. Bunge liridhie, Mheshimiwa Rais akamalizie huko ili sheria na kila kitu kiweze kukaa vizuri na kanuni ziandaliwe mapema kwa utekelezaji. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Margreth Mkanga, ahsante sana. Daima tunakutambua na nchi nzima na hata nje ya nchi unatambulika kwa utetezi wako shupavu kuwatetea watu wenye ulemavu nchini na Afrika Mashariki yote. *(Makofi)*

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo kuchangia Maazimio haya mawili ya Haki za watu wenye ulemavu duniani.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara kwa kuweza kufikisha Maazimio haya leo ili Bunge letu na nchi yetu iweze kuridhia, nami furaha yangu na shukrani zangu ni kubwa sana kwani siku zote nilikuwa nikigombana na Mheshimiwa Waziri wa Afya na

Ustawi tukikutana baada ya kusalimiana namwuuliza habari hii, kwa hiyo, leo ugomvi wangu na Waziri umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nawashukuru viongozi wa vyama vya walemavu Bara na Visiwani ambayo kwa kushirikiana na mwenzangu Mheshimiwa Mkanga wapo ukumbini hapa, tumefanya juhudi ili waje kushudia kuridhiwa kwa Maazimio haya.

Mheshimiwa Spika, najua sana ni jinsi gani nchi yetu inavyotuthamini watu wenye ulemavu na ninashukuru kwa misaada hapa Bungeni tunayosaidiwa, ushirikiano uliopo kwa kweli hata wakati mwingine mimi hujisahau kama kumbe nina kasoro, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi kuishukuru Serikali yetu Tukufu inayoongozwa na Chama chetu cha Mapinduzi kwa kutuwezesha watu wenye ulemavu kuwepo katika Bunge letu hili Tukufu kupitia *UWT*, nina imani leo tupo wawili lakini labda 2010 baada ya mabadiliko mbalimbali bila shaka kutakuwa na wawakilishi wengi wa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na ilani ya uchaguzi ya 2005 Ibara ya 106 na 123 imezungumzia sana masuala ya watu wenye ulemavu na leo tunaona yanaendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile sina budi kulishukuru Bunge letu Tukufu chini ya uongozi wako, kwani mimi ni miongoni mwa hao ambayo tulishiriki *NewYork* - Marekani mwaka 2006 katika ku-*finalise* mkataba huu, nashukuru sana, vile vile mwaka 2007 kulifanyika Mkutano wa Chama cha Walemavu Duniani na baadhi ya gharama tulisaidiwa na Ubalozi wa Korea Mkutano ambao ulifanyika *Korea South* na baadhi ya gharama Bunge lilikubali kuchangia, kwa kweli tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile mwaka uliokwisha nilibahatika kupata mwaliko kutoka Shirikisho la Vyama vya Walemavu Ethiopia, waliandaa mkutano kama Kampeni kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa Ethiopia kwa sababu nchi yao haijaridhia na hawana Mbunge mwenye ulemavu katika nchi yao. Kwa hiyo, nilibahatika kupata mwaliko ule na kila kitu, walifadhili wenyewe lakini nilipoijulisha Ofisi ya Bunge kuhusu suala hilo, Ofisi ya Bunge ikamfadhili msaidizi wangu ili niende naye kushiriki, kwa hiyo, sina budi kushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu uliandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Wenye Ulemavu Ethiopia kama kampeni yao kwa sababu nchi yao haijaridhia na pili tulizungumzia kuhusu wabunge wenye ulemavu katika nchi zetu za Ukanda wa Afrika Mashariki. Mimi nilipopata huo mwaliko na kujua malengo walitaka kujua nchi ambazo zina wawakilishi wenye ulemavu tumeingiaje, tupo vipi na tumepata zile nafasi, kwa hiyo, tulijadili na wakataka kujua kwa nini hazijaridhia huu mkataba. Wenzetu Kenya walikuwepo, wao hawana Mbunge mwenye ulemavu Bungeni kwao lakini Mkataba wameridhia, Uganda wameridhia, Sudan pia walikuwepo walisharidhia na walialikwa Afrika Kusini na Madagascar.

Mheshimiwa Spika, leo ni furaha kwamba sijamaliza hata mwezi niliporudi kwenye Mkutano ule tayari Mikataba hii inaletwa na kuridhiwa, bila shaka kesho itabidi mapema nitume barua pepe kuwajulisha na mimi nchi yangu imesharidhia, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono yote yaliyozungumzwa kwenye mikataba yote miwili na Waziri na Kamati ya huduma za Jamii na kwa upande wa upinzani, mengine mwenzangu ameshaongea.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kuhusu Maazimio haya na Mikataba hii, kama haujaletwa Muswada wa Sheria bado itakuwa hakijafanyika kitu. Ninasisitiza Wizara husika kwamba Muswada wa Sheria kuhusu haki za watu wenye ulemavu uletwe haraka kabla ya mwaka huu kwisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Zuleikha kwa niaba ya watumishi wa Bunge na mimi nazipokea pongezi zako kwa kazi nzuri wanayofanya kuweza kuangalia ninyi wenzetu.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii angalau na mimi niseme machache kuhusiana na mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, mimi pia nilikuwa mmoja wa wabunge walioshiriki katika kuandaa mchakato wa mikataba hii kule Marekani, kwa hiyo, nakushukuru wewe binafsi na ofisi yako kwa kutupatia nafasi hii, nafasi hii imenifundisha mambo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu tunaoupitisha kweli si kwa ajili ya walemavu wa leo lakini ni kwa walemavu wote na hata miaka ijayo na tunafanya kazi ya kiroho zaidi, kazi ya upendo. Mimi naomba Waheshimiwa Wabunge tusisite kupitisha mkataba huu kwa sababu ni kitu cha msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sikuwa hivi nilivyo miaka ya nyuma, nilikuwa ni mtu ambaye nilikuwa nakimbia sana, nilikuwa napigana ngumi sana, hayo yote leo siwezi kuyafanya, kama alivyosema Mheshimiwa Mkanga, lolote linaweza kutokea kwa mtu yeyote kwa wakati wowote, kwa hiyo, hiki kitu tunachofanya sasa hivi ni kitu cha msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliposhiriki katika kikao hicho kulikuwa na tatizo la tafsiri, iwe ni kwa ajili ya walemavu au watu wenye ulemavu. Baadaye likapita hili la watu wenye ulemavu, kwa nini? Tunaongelea juu ya mtu ambaye anaupungufu Fulani. Ukisema tunaongea juu ya walemavu unaondoa utu, mtu mwenye ulemavu ni mtu ambaye ana utu wake, haki zake na ana stahili zake, hilo ndilo chimbuko la tafsiri hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu mtu ambaye tunamwongelea hapa ni mtu ambaye amepungukiwa na kitu fulani katika uwezo wake wa kutekeleza mambo Fulani. Kwa hiyo, tunachofanya hapa ni kupitisha mkataba wa kumwezesha aweze kutekeleza mambo yake. Hapo ni suala hapo la uwezeshaji, kumwezesha mtu aweze kufanya kitu fulani.

Mheshimiwa Spika, jaribu kufikiria kwa mfano kama hatungekuwa na miwani wale mnaotumia miwani mngesomaje? Ni uwezeshaji tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wenye ulemavu wanachohitaji sio misaada ni kuwezeshwa waweze kutekeleza mambo fulani, mimi naomba sana tukubali kuipitisha hii ili sheria itungwe tuweze kuangalia tunawasaidiaje na kuwapatiaje uwezo watu wenye ulemavu waweze kushiriki katika uzalishaji na kushiriki katika uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa bado nakumbukakumbuka kipindi kulichopita kile, tumejitahidi kujenga shule kwa ajili ya vijana wetu wote, lakini shule hizi zote zinaweza kutumika vizuri kwa watu wenye ulemavu? Bado kuna tatizo la kuingia madara sana, bado kuna tatizo la lugha kwa mtu asiyesikia, ataingia kwenye darasa la mwalimu anayeongea, huo ndiyo uwezeshaji tunaouhitaji.

Mheshimiwa Spika, bado tuna matatizo katika maeneo ya afya. Juzi tulikuwa tunapitisha sheria ya *DNA*, sasa inawezekana kuona kwa mama mjamzito kufahamu kwamba mtoto anayetarajiwa kuzaliwa anaweza kuwa mlemavu, tunafanya nini? Tunamwandaliaje mazingira mtoto huyo, katika kikao hicho kulikuwa na mvutano mkubwa sana: Je, waruhusiwe kutoa hizo mimba kabla ya mtoto kuzaliwa, hatimaye ikakubalika kwamba tuache madaraka hayo kwenye Serikali husika.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na tatizo la haki za makazi, haki za kuwa na familia, mlemavu anashindwa kupenda mtu wa jinsia tofauti, anashindwa kuolewa, anashindwa pia kuoa afanyeje na anataka kuwa na mji wake na familia yake? Je, turuhusu wanaume kwa wanaume waoane au wanawake kwa wanawake waoane, kulikuwa na mvutano mkubwa sana, lakini hatimaye ikakubalika kwamba kila nchi iendelee na sheria zake. Hapo ndipo ilipokuja wale wanaoruhusu *homosexuality* waendelee na sehemu ambazo haturuhusu tusiruhusu mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, nimeyasema hayo ili pamoja na utekelezaji wa mkataba huu vilevile tusiache utamaduni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dakika mbili zilizopita hizi, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wale walionifikisha hapa ma-*physiotherapist* wangu Dr. Ibra wa Bugando na Dr. Dennis wa Muhimbili na Dr. Machaga wa *MOI*; Waheshimiwa Wabunge, mimi nisingekuwa hapa zaidi ya kitandani masaa 24, hao ndiyo walionitoa kitandani wakaniwezesha kuanza kutembea, sasa hivi mnaniona ninahangaika kutembea lakini baadaye naweza kukimbia, lakini kwa sababu ya watu hawa.

Mheshimiwa Spika, kuna kipindi fulani niliiomba Wizara ya Afya iongeze *maphysiotherapist* katika hospitali zetu, ulemavu mwingine ni kwa sababu ya kukosa watalaamu hawa, tukiwa na watalaamu wengi tutasaidia sana watu wengi.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia rai yangu, naomba sana Wizara ya Afya itoe mafunzo kwa *physiotherapist* wengi ili waweze kufika hata kwenye vituo vya afya. Naomba pia jamii baada ya kupitisha mkataba huu, wananchi wakubali kuutekeleza mkataba huu kwa matendo, wananchi ndiyo wanaokaa na watu weye ulemavu.

Waheshimiwa Wabunge, hapa inawezekana hapa hatukai na walemavu katika familia zetu, lakini wananchi wajitahidi sana kuupokea mkataba huu na wautekeleze kwa vitendo ili jamii ya watu wenye ulemavu wawezeshwe katika kutekeleza mambo yao na katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Sakila na hasa kwa maelezo uliyoyatoa, sisi tunaokufahamu tangu zamani haya yamekuja kukutokea baadaye. Kwa hiyo, ni kweli kabisa kwamba jambo hili halichagui wala si jambo la kusema tu, basi mtu uko hivyo ulivyozaliwa utaendelea mpaka mwisho.

Waheshimiwa Wabunge, muda umefika wa kuahirisha shughuli za Bunge, nina wachangiaji wanne katika maazimio haya, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Rished Abdallah, Profesa Idris Mtulia na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Tutajaribu kuona kama wote wanaweza kuchangia kabla hatujakwenda katika shughuli nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo huku nikiwatakia jioni njema, sasa ninaahirisha shughuli za Bunge hadi hapo kesho asubuhi saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.46 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 24 Aprili, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*